# UCHANGANUZI WA WATOTO KATILI KATIKA FASIHI YA WATOTO

**NYARIKI ENOCK NYARIKI**

**C50/ CE/34456/2016**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA ILI KUKIDHI BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI YA CHUO KIKUU CHA KENYATTA**

**MEI, 2023**

# UNGAMO

Tasnifu hii ya utafiti ni kazi yangu asili wala halijawahi kuwasilishwa katika chuo kingine kwa madhumuni yoyote.

**MTAFITI**

Sahihi:.......................................... Tarehe:....16.5.2023........................

**Nyariki Enock Nyariki**

**C50/CE/34456/2016**

**MSIMAMIZI**

Tasnifu hii limetolewa kwa idhini yangu kama Msimamizi aliyechaguliwa na Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Sahihi:.......................................... Tarehe:....16.5.2023........................

**Pamela M. Ngugi**

**Idara ya Kiswahili**

**Chuo Kikuu Cha Kenyatta**

## TABARUKU

Kakangu Dkt. Thomas Manyibe Nyariki. Udhamini wako masomoni umenisaidia kuvuta hatua kiasi hiki.

## SHUKRANI

Ninamshukuru Mungu ambaye alinijalia akili razini na afya njema wakati wote nilipokuwa nikiufanya utafiti huu. Aidha, shukrani tele kwa msimamizi wangu Dkt. Pamela Ngugi kwa ushauri na uelekezi wake mwema ulioniwezesha kuiboresha kazi hii na kuikamilisha kwa wakati unaofaa.

Fauka ya hayo, ningependa kumshukuru mke wangu Rose Kiliru Nyariki kwa mapenzi yake ya dhati kipindi chote nilipokuwa masomoni. Aidha, ninamshukuru kakangu Naftal Nyariki ambaye nyumbani kwake kulinipatia mazingira mwafaka ya kuifanyia kazi hii. Ninaishukuru idara ya Kiswahili ikiongozwa na mwenyekiti Profesa Githinji na wahadhiri wote wa Kiswahili kwa msaada iliyonipa wakati nilipokuwa nikiufanya utafiti huu. Wote walionitilia pondo katika mchakato mzima wa kuufanya utafiti huu na ambao sikuyataja majina yao hapa, shukran jazila.

## IKISIRI

Utafiti huu uliazimia kutathmini suala la wahusika katili ambao ni watoto katika vitabu teule vya fasihi katika kategoria ya vijana. Ulichunguza na kuhakiki aina za ukatili wa watoto, sababu zinazochangia matendo ya ukatili, athari kwa wahusika wengine na jinsi matendo yenyewe yanavyoweza kudhibitiwa. Riwaya zilizochanganuliwa ni: *Tumaini* (Momanyi, 2006) *Siku Njema* (Walibora, 1996) *na Lulu ya Maisha* (Habwe, 2013) ambazo zinalenga hadhira ya vijana. Utafiti ulibainisha kuwa japo jamii humtazama mtoto kama mhanga wa matukio ya ukatili**,** baadhi ya watoto pia ni katili. Ukatili uliobainika miongoni mwao ni ule wa kimatendo, kimatamshi na wa kuwaziwa. Utafiti uliongozwa na nadharia ya ujifunzaji wa kijamii ya Bandura (1977) ambayo waitifaki wake ni pamoja na Baltes na Reese (1984) na nadharia ya uhalisia ambayo waasisi wake ni pamoja na Gustav Flaubert (1850), Rene Wellek (1963) na Lazaro Carreter(1970). Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii ilisaidia kueleza jinsi watoto huiga tabia za watu wazima. Nayo nadharia ya uhalisia ilisaidia kuonyesha jinsi ukatili katika jamii ulivyoakisiwa na waandishi wa fasihi. Utafiti ulijikita maktabani. Data ya msingi ilipatikana kwa kuvisoma vitabu vilivyotajwa kisha kuigawa na kuichanganua kulingana na malengo ya utafiti. Utafiti ulinufaishwa kwa kuzisoma na kuzihakiki kazi zinazohusiana na mada hii kwenye majarida, makala ya magazeti yaliyouangazia ukatili wa watoto, tasnifu, vitabu na machapisho kuhusu nadharia. Maelezo ya kina yalitumiwa kuwasilisha matokeo ya utafiti. Baadhi ya mikakati ya kuyakabili matendo ya ukatili wa watoto iliyobainika ni pamoja na kuyapunguza mambo yanayoweza kusababisha ukatili katika familia, shule na jamii. Matokeo ya utafiti yatawafaidi waandishi, watafiti na wadau wa kazi za fasihi kuliangazia suala la ukatili kwa mtazamo mpana: kwamba mtoto si tu mhanga au mwathiriwa wa matukio ya kikatili bali pia anaweza kuwa mhusika katika kutekeleza ukatili dhidi ya wanajamii wengine. Aidha, yanaweza kuwafaa wahusika wa masuala ya watoto kuibuka na njia mwafaka za kukabiliana na matendo ya kikatili miongoni mwa watoto.

## ABSTRACT

This study aimed at assessing cruel children characters in selected literature books in the youth category. It investigated and analysed the types of cruelty of these children, the reasons that contribute to their being cruel, the effects of this cruelty on other characters and how it can be managed. The following novels which target the youth audience were examined: *Siku Njema* by Ken Walibora (1996),*Tumaini* by Clara Momanyi (2006), and *Lulu ya Maisha* by John Habwe (2013). The study showed that although a child is usually viewed as a victim of cruelity, some children are perpetrators of cruelty and therefore the community needs to come up with ways of controlling their actions. The study found that children commit physical, verbal and emotional types of cruelty. The study was guided by the social learning theory by Bandura (1977) whose proponents include Baltes and Reese (1984) and the realism theory whose proponents include Gustav (1850), Rene Wellek (1961)and Lazaro Carreter (1970) among others. Social learning theory assisted the research in explaining how children learn by observing role models within their environment. The theory of realism assisted the research in showing how cruelity in the community is reflected by writers of literary work. The study was conducted through desktop research. Primary data was obtained by reading the novels mentioned above, dividing the data thematically and analyzing it according to the research objectives. The study compared and cross-validated the research findings with those in journals, news papers, theses, books and other online publications on the subject matter. The research findings were presented in descriptive form. Some of the strategies to address cruelty among children that the study found included reducing potential causes of cruelty in children in families, at school and in the society.The research findings will benefit authors, researchers, editors, publishers and other stakeholders of Literature in highlighting cruelity in a broader percipective of the child not only as a victim of violent situations but also as one capable of acting violently towards other members of the community. Besides, the findings could help those dealing with children issues to device best ways of curbing violent acts in children.

## UFAFANUZI WA DHANA

**Katili:** Kwa mujibu wa utafiti huu, mtu katili ni yule ambaye matendo yake yanadhihirisha utovu wa huruma.

**Tanbihi:** Kitendo kinachokusudiwa kupasha adhabu katika jamii fulani katika wakati fulani kinaweza kufasiliwa kuwa ukatili katika jamii nyingine au hata jamii ile ile kutegemea mitazamo, kiwango, nia ya mtumiaji, sera ibuka miongoni mwa mambo mengine. Kwa mfano, utumiaji wa kiboko kumwadhibu mtoto ulikubalika nchini Kenya kabla ya sera mpya iliyoupiga marufuku kwa sababu ya kutumiwa vibaya au kupindukia pamoja na masuala mengine ibuka kuhusu haki za watoto. Hali hii ndiyo inayosababisha utata katika kueleza kwa yakini iwapo adhabu ni sawa na ukatili ingawa maana ya msingi inaonyesha kuwa hizi ni dhana mbili tofauti.

**Mtoto:** Hunt (1994) anamwelezea mtoto kama binadamu ambaye akili na mwili wake havijakomaa. Fasili ya kisheria nchini Kenya inamtambua mtoto kama binadamu ambaye yuko chini ya umri wa miaka 18. Kwa mujibu wa utafiti huu, mtoto ni binadamu mwenye umri baina ya miaka 11 na 18 ambao katika maandishi mengi ndio umri unaohusishwa na visa vya ukatili miongoni mwa watoto.

# YALIYOMO

**UNGAMO** ........................................ **ii**

**TABARUKU** ........................................ **iii**

**SHUKRANI** ........................................ **iv**

**IKISIRI** ........................................ **v**

**ABSTRACT** ........................................ **vi**

**UFAFANUZI WA DHANA** ........................................ **vii**

**YALIYOMO** ........................................ **viii**

**SURA YA KWANZA** ........................................ **1**

**UTANGULIZI** ........................................ **1**

1.1 Usuli wa mada ........................................ 1

1.2 Suala la utafiti ........................................ 4

1.3 Malengo ya utafiti ........................................ 5

1.4 Maswali ya utafiti ........................................ 5

1.5 Sababu za kuchagua mada ........................................ 5

1.6 Upeo na mipaka ya utafiti ........................................ 6

1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada ........................................ 6

1.8 Misingi ya nadharia ........................................ 13

1.8.1 Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii ........................................ 13

1.8.2 Mihimili ya nadharia ya Ujifunzaji wa kijamii ........................................ 16

1.8.3 Nadharia ya uhalisia ........................................ 17

1.8.4 Mihimili ya nadharia ya uhalisia ........................................ 18

1.9 Mbinu za utafiti ........................................ 19

1.9.1 Muundo wa utafiti ........................................ 19

1.9.2 Eneo la Utafiti ........................................................................................20
1.9.3 Uteuzi wa sampuli.........................................................................................20
1.9.4 Mbinu za ukusanyaji data ................................................................................20
1.9.5 Mbinu za uchanganuzi wa data.........................................................................21
1.9.6 Mbinu za kuwasilisha matokeo........................................................................21
1.9.7 Maadili ...........................................................................................................21
**SURA YA PILI.............................................................................................22**
**AINA ZA UKATILI WA WATOTO KATIKA VITABU TEULE VYA FASIHI YA WATOTO.........................................................................................22**
2.0 Utangulizi.........................................................................................................22
2.1.1 Siku Njema (1996)..........................................................................................23
2.1.2 Tumaini (2006) ...............................................................................................27
2.1.3 Lulu ya Maisha (2013).....................................................................................32
2.1.4 Aina za ukatili wa watoto zinazobainika katika riwaya teule.......................35
2.1.5 Ukatili wa kimatendo........................................................................................35
2.1.5.1 Uharibifu wa mali ..........................................................................................42
2.1.5.2 Unyanyasaji wa kimapenzi ...........................................................................42
2.1.6 Ukatili wa kimatamshi......................................................................................44
2.1.7 Ukatili wa kuwaziwa.........................................................................................50
2.1.6 Hitimisho..........................................................................................................51
**SURA YA TATU.............................................................................................53**
**SABABU ZINAZOCHANGIA UKATILI MIONGONI MWA WATOTO KATIKA VITABU TEULE VYA FASIHI YA WATOTO NA ATHARI ZAKE KWA WAHUSIKA WENGINE..........................................................53**

3.0 Utangulizi...........................................................................................53

3.1. Sababu zinazochangia tabia ya ukatili katika vitabu teule vya fasihi ya watoto.......................................................................................................54

3.1.1 Sababu za kifamilia.............................................................................54

3.1.2 Sababu za kijamii................................................................................64

3.1.2.1 Matumizi ya dawa za kulevya.........................................................65

3.1.2.2 Ushawishi wa marika.......................................................................67

3.1.2.3 Imani na itikadi katika jamii ............................................................69

3.1.2.4 Utabaka katika jamii ........................................................................70

3.1.3 Sababu zinazohusiana na shule..........................................................72

3.2 Athari Za Ukatili wa Watoto kwa Wahusika Wengine Katika Vitabu Teule vya Fasihi ya Watoto ...................................................................................78

3.2.1 Athari zinazoonekana bayana ............................................................78

3.2.2 Athari za kisaikolojia..........................................................................80

3.2.3 Mwathiriwa kujitenga na wanajamii wengine ......................................84

3.2.4 Hitimisho............................................................................................85

**SURA YA NNE ..........................................................................................87**

**MIKAKATI YA KUUKABILI UKATILI MIONGONI MWA WATOTO KATILI KATIKA VITABU TEULE..............................................................87**

4.0 Utangulizi...........................................................................................87

4.1 Mikakati ya kuukabili ukatili miongoni mwa watoto. ...................................88

4.1.1 Kuyapunguza mambo yanayoweza kusababisha ukatili katika familia........89

4.1.1.1 Kudhibiti matendo ya ukatili katika familia ...........................................89

4.1.1.2 Kuepuka adhabu kali wakati wa kuwarekebisha watoto ...........................94

4.1.1.3. Familia kuwa na watu vielelezo wanaokidhi mahitaji ya mtoto...............96

4.1.2 Kuyapunguza mambo yanayoweza kusababisha ukatili shuleni ................103

4.1.2.1 Kuepuka adhabu kali na kutumia njia mbadala kushughulikia nidhamu 104

4.1.2.2 Kubuni njia mwafaka za kushughulikia utovu wa nidhamu....................109

4.1.2.3 Kuandaa shughuli za masomo ambazo zinakidhi mahitaji ya wanafunzi wote..........................................................................................................113

4.1.2.4. Kudhibiti Ushawishi wa Marika ...........................................................115

4.1.3 Kuyapunguza mambo yanayoweza kusababisha ukatili katika jamii.........117

4.1.3.1 Kuwakanya watu wanaowapotosha watoto .............................................118

4.1.3.2. Kudhibiti ushawishi wa marika katika kiwango cha jamii .....................120

4.1.4 Hitimisho...................................................................................................122

**SURA YA TANO .........................................................................................123**

**HITIMISHO, MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI ..............123**

5.0 Utangulizi.....................................................................................................123

5.1 Muhtasari wa utafiti .....................................................................................123

5.2 Matokeo ya utafiti ........................................................................................125

5.3 Mchango wa utafiti ......................................................................................127

5.4 Changamoto za utafiti ..................................................................................128

5.5 Mapendekezo ...............................................................................................129

**MAREJELEO ...............................................................................................130**

Kiambatisho I: Barua ya NACOSTI ..................................................................141

# SURA YA KWANZA

# UTANGULIZI

## 1.1 Usuli wa mada

Visa vya ukatili miongoni mwa watoto vimeongezeka katika siku za hivi punde na kulifanya kuwa suala mtanzuka katika jamii (Connor, 2002; Khan, 2014, AACAP, 2015). Kulingana na AACAP (2015), watoto ambao hawajafikisha umri wa kuenda shuleni wanaweza kuonyesha tabia za ukatili kwa sababu ya kuwa waathiriwa wa kuchapwa, kudhulumiwa kimapenzi, kushuhudia ukatili nyumbani na katika jamii, kutazama ukatili kwenye vyombo vya habari, na kuwa wahanga wa udhalilishaji miongoni mwa sababu nyingine. Kulingana na AACAP (keshatajwa) , tabia ya ukatili inayotokea katika umri wowote wa mtoto inapaswa kushughulikiwa bali isipuuzwe na kuchukuliwa kuwa ni hatua mojawapo ya ukuaji wa mtoto.

Khan (2014) anaeleza kuwa ukatili ni tatizo lililo dhahiri katika takribani asilimia 23-40 ya watoto ulimwenguni. Naye Connor (2002) anafafanua kuwa watoto wenye kasoro ya kitabia mara nyingi husababisha migogoro katika familia zao na kuleta balaa shuleni ambapo walimu wao hujaribu kuzishughulikia kasoro hizo na kulinda usalama wa wanafunzi wenzao na wahusika wengine. Aidha, watoto ambao wamekua katika mazingira yaliyo na ukatili wako katika hatari kubwa ya kutenda uhalifu katika maisha yao ya baadaye na hivyo kuwa sehemu ya mzunguko wa ukatili (Finkelhor, Turner, Ormrod, Hamby na Kracke, 2009).

Nchini Kenya, ukatili miongoni mwa watoto unajidhihirisha kupitia ngono na udhalilishaji miongoni mwa matendo mengine (Ministry of Gender Children and Social Development, 2010). Kulingana na ripoti ambayo imerejelewa, asilimia 25 ya wale waliotekeleza ukatili wa kingono dhidi ya watoto wenye umri wa miaka 13 -17 walikuwa wanafunzi wenza.

Ukatili unadhihirika katika fasihi simulizi. Baadhi ya masimulizi, kwa mfano, hadithi,visasili, mighani miongoni mwa mengine yalijumuisha ukatili mwingi na dhuluma dhidi ya watoto (Morellato,2017). Katika vitabu vya fasihi ya watoto,ukatili si suala geni ila lina mizizi yake katika hadithi za kwanza zilizoandikiwa watoto (Nimon, 1993; Todorova, 2020). Todorova (keshatajwa) anatumia mikusanyiko ya hadithi za kifantasia za Charles Perrault (1697) na Brothers Grimm (1812) kuonyesha kuwa ukatili, jinsi unavyoeleweka sasa, ulikuwa jambo la kawaida katika maisha ya utoto na katika hadithi zilizosimuliwa watoto tangu kale katika sehemu mbalimbali za dunia. Nimon (keshatajwa) na Todorova (keshatajwa) wanaeleza kuwa picha za matendo ya kikatili yanayosababisha uchungu kwa mwili zilitumika kama kielelezo cha nidhamu katika vitabu vya kufunzia watoto uadilifu. Nimon (keshatajwa) anahitimisha kwamba vitabu vya fasihi ya watoto vinaweza kushughulikia ukatili na migogoro ila vifanye hivyo kwa njia ambayo inaonyesha majuto ya wahusika katili na suluhu ya ukatili wenyewe badala ya ulipizaji kisasi.

Pitcher (1969) anaeleza kwamba wakati mwingine vitabu vya fasihi ya watoto huwasilisha maudhui sawa na yale yanayojitokeza mara kwa mara katika fasihi ya watu wazima. Anafafanua kwamba ingawa baadhi ya maudhui hayo, kama vile vita na vifo, yanaweza kufasiliwa na watu wazima kama ukatili kwa watoto, watoto wenyewe huvutiwa nayo na hata kunufaika kisaikolojia kwa kudadisi wenyewe na kupambanua kile ambacho ni kizuri na kibaya. Pitcher (keshatajwa) anahitimisha kwamba haiwezekani watoto kuwa katili kwa kuyasoma masuala hayo katika vitabu vyao. Mtazamo huu unaelekea kukinzana na maoni ya Esma & Can (2019) kwamba ukatili katika vitabu vya fasihi ya watoto unaweza kuwa na athari kubwa ya kuwafanya watoto kuwa katili na kuudhihirisha ukatili huo waziwazi. Esma na Can (wametajwa) wanashauri kuwa katika kuandaa matini ambayo yanakusudiwa kuwakuza na kuwaimarisha watoto kwa njia mbalimbali, ni muhimu kuwa waandishi waliwasilishe suala la ukatili kiwastani bila kulitilia chuku.

Uandishi kuhusu ukatili katika fasihi ya watoto unaibua woga kuwa watoto wanaweza kuiga vitendo vya ukatili walivyovisoma na kuvitekeleza shuleni hasa ongezeko la ufyatuaji risasi shuleni unaotekelezwa na wanafunzi katika mataifa ya magharibi linapolitiwa manani (Megan, 2010). Msimamo wa Megan (keshatajwa) ni kwamba wanaoteua vitabu vya watoto vyenye vipengele vya ukatili wanapaswa kuchunguza kwa makini ili kuthibitisha kwamba ukatili unaojidhihirisha unatekeleza dhima kama vile kuonyesha madhara ya ukatili kwa wahusika.

Vitabu vya fasihi ya watoto vinavyojumuisha kiasi kidogo cha ukatili huwavutia watoto na kuwapa funzo chanya kuhusu kuadhibiwa kwa vitendo viovu (Ruthiiri, 2012; Ngugi, 2014). Ruthiiri na Ngugi wanaeleza kuwa watoto hupenda kusoma hadithi ambamo wavulana, wasichana na wanyama wanaadhibiwa kwa vitendo vyao viovu ila adhabu yenyewe isiwe kali sana au yenye nia mbaya lakini itoshe ili mtoto apate hisia za kutosheka kwamba haki imetendeka.

Watafiti wengi wamelishughulikia suala la ukatili katika fasihi ya watoto ijapokuwa kipengele cha mtoto kama mhusika katili hakijahakikiwa kwa kina. Aidha, wachanganuzi wengi ambao wameuangazia ukatili katika fasihi ya watoto wamefanya hivyo katika mazingira ya kimagharibi ambayo huenda yasiuakisi ukatili unavyotendeka katika mazingira ya Kiafrika. Ni katika misingi hii ambapo utafiti huu ulikusudia kuliziba pengo hili kwa kumwangazia mtoto kama mhusika katili katika fasihi ya watoto kwa lugha ya Kiswahili.

## 1.2 Suala la utafiti

Katika siku za hivi karibuni, visa vingi vya ukatili unaotekelezwa na watoto dhidi ya wanajamii wengine vimekuwa vikiangaziwa katika vyombo vya habari na mitandao ya kijamii na kulifanya jambo hilo kuwa suala mtanzuka. Visa hivyo ni pamoja na uharibifu wa mali, matumizi ya silaha hatari kujeruhi, udhalilishaji na mauaji miongoni mwa vingine . Wachanganuzi wengi wa fasihi ya watoto wameshughulikia kipengele cha mtoto kama mhanga wa matendo ya ukatili. Suala la mtoto kama mhusika katili halijahakikiwa kwa kina. Ni katika misingi hii

ambapo utafiti huu ulichanganua watoto katili katika vitabu teule vya fasihi ya watoto kwa lugha ya Kiswahili.

## 1.3 Malengo ya utafiti

Utafiti uliongozwa na malengo yafuatayo:

1) Kubaini aina za ukatili wa watoto katika vitabu teule vya fasihi ya watoto.
2) Kutathmini sababu zinazochangia matendo hayo miongoni mwa wahusika na athari kwa wahusika wengine.
3) Kutathmini mikakati mbalimbali ya kuukabili ukatili huo.

## 1.4 Maswali ya utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo:

1) Je, ni aina gani za ukatili wa watoto zinazojidhihirisha katika vitabu vilivyoteuliwa vya fasihi ya watoto?
2) Ni sababu gani zinazochangia matendo ya ukatili ya watoto na yana athari gani kwa wahusika wengine katika vitabu vilivyoteuliwa vya fasihi ya watoto?
3) Ni mikakakati gani inayoweza kutumiwa kuukabili ukatili huo?

## 1.5 Sababu za kuchagua mada

Mada ya ukatili unaohusu watoto nchini Kenya na sehemu nyingine za ulimwengu ni suala mtanzuka linaloendelea kuibua mijadala katika jamii kupitia vyombo mbalimbali vya mawasiliano. Ingawa wasomi wamelishughulikia suala la ukatili unaohusu watoto kwa mitazamo tofauti, changanuzi nyingi zinalenga

kipengele cha mtoto kama mhanga wa ukatili wala si kama mhusika katili. Aidha, mada hii imeshughulikiwa katika mazingira ya kimagharibi ambayo si yakinifu katika kuuelewa ukatili unaohusu watoto nchini Kenya. Uhaba wa maandishi yanayomwangazia mtoto kama mhusika katili katika fasihi ya watoto kwa lugha ya Kiswahili ni pengo muhimu la utafiti. Kwa kulishughulikia pengo hili, kazi hii imeongeza maarifa katika fasihi ya Kiswahili kuhusu mada hii. Licha ya hayo, imechangia katika kulielewa suala la watoto katili katika jamii, chanzo chake na jinsi ukatili huo unavyoweza kudhibitiwa. Vilevile, utafiti huu umeweka msingi wa kiutafiti kwa wasomi wengine ili waitafitie mada hii kwa kina zaidi.

### 1.6 Upeo na mipaka ya utafiti

Vitabu vinne; *Siku Njema* (Walibora, 1996)*; Tumaini* (Momanyi, 2006) *na Lulu ya Maisha* (Habwe, 2013) vilishughulikiwa. Sababu ya kuteua vitabu hivi ni kuwa vina wahusika watoto ambao ni katili. Katika vitabu hivi, tulichunguza na kuhakiki aina za ukatili wa watoto, sababu zinazochangia matendo ya ukatili, athari ya matendo yenyewe kwa wahusika wengine  na jinsi ya kuukabili ukatili huo.

### 1.7 Yaliyoandikwa kuhusu mada

Suala la ukatili katika fasihi ya watoto limehakikiwa na watafiti mbali mbali (Koehnecke, 2001, Mugubi, 2003; Karanja, 2008, Kavuria, 2008, Ruthiiri, 2012; Dunlap, 2012; Odhiambo, 2017; Muguro, 2018, Esma &Can, 2019 na Mwenda, 20202) kwa viwango mbalimbali.

Koehnecke (2001) amechanganua vitabu viwili vya picha vya watoto; *“Smoky Night”* cha Eve Bunting *(*1994) na “*The House that Crack Built* cha Clark Taylor (1992). ‘‘*Smoky Night’’* kinaangazia maandamano, uporaji na uchomaji wa mali unaotekelezwa na watoto katika jiji la Los Angeles ilhali ‘‘*The House that Crack Built’’* kinamwangazia mwanamume tajiri mlanguzi wa dawa ya kulevya ya kokeini anayeyatumia magenge ya vijana kuisambaza dawa hiyo katika jiji hilo hilo la Los Angeles. Koehnecke (keshatajwa), anaibua mitazamo mbalimbali ya wadau wa fasihi ya watoto kuhusu utumiaji wa vitabu hivi kuwafunzia wanafunzi wa gredi ya pili katika shule za jimbo la Los Angeles. Wanaopinga matumizi ya vitabu hivyo kufunzia watoto wanalalamika kuwa vinayaangazia kwa uwazi mno masuala yanayoonyesha hofu na yanayoweza kumwathiri mtoto kwa njia hasi. Wanaounga mkono wanaviona kama nyenzo muhimu ya kupitishia maadili shuleni na kwenye jamii kwa sababu vinashughulikia masuala ambayo aghalabu wazazi hawayajadili na watoto wao. Msomi huyu anahitimisha kuwa mada nyeti kama vile ulanguzi na matumizi ya dawa za kulevya, maandamano, uhalifu miongoni mwa nyingine zinaweza kujumuishwa katika hadithi za watoto kwa njia faafu, hakikifu na zingativu licha ya kuwa zinaweza kuzua utata. Utafiti wa Koehnecke (keshatajwa) unaangazia mitazamo tofauti ya wadau wa fasihi ya watoto kuhusu matumizi ya vitabu vyenye mada ya ukatili kufunzia watoto Hata hivyo, utafiti wa Koehnecke ulichangia utafiti huu katika kuelewa matendo yanayodhihirisha ukatili.

Mugubi (2003) ametafiti kuhusu mhusika mtoto katika fasihi ya watu wazima kwa kutumia nadharia za kisaikolojia na kisoshiolojia. Mugubi (keshatajwa) ambaye anazichanganua riwaya sita teule za waandishi wa Hindi-Magharibi anadhamiria kubaini nafasi ya mtoto katika jamii ya waandishi hao na dhima yake katika fasihi. Anafafanua kuwa waandishi wa Hindi-Magharibi wanamdhihirisha mtoto kama mhanga wa ubaguzi wa kikabila, kitabaka na kijinsia. Anahitimisha kwamba mtoto anaweza kutumika kama chombo ambacho kwacho maudhui kama vile umaskini, udhalimu wa polisi, ubaguzi wa rangi, dini na siasa yanaweza kuchunguzwa. Ingawa utafiti wa Mugubi unaangazia usawiri wa mtoto kwa njia tofauti tofauti katika fasihi ya watu wazima, ulisaidia kuyaelewa matendo yanoyodhihirisha ukatili na athari zake. Hata hivyo, utafiti huu ulitilia maanani ukweli kwamba utafiti wa Mugubi umejikita kwenye mazingira ya kigeni ambayo huenda yasisawiri picha halisi ya ukatili jinsi unavyotokea katika mazingira ya Kenya.

Mada kuhusu masuala ibuka katika hadithi za watoto imetafitiwa na Karanja (2008) kwa kutumia nadharia ya uhalisia na ya kimtindo. Ameonyesha jinsi waandishi wa vitabu teule vya fasihi ya watoto walivyoangazia dhuluma dhidi ya watoto ili kupitisha funzo chanya. Masuala aliyoyahakiki mtafiti ni ubaguzi wa kijinsia, ukiukaji wa haki za watoto, unyanyapaa dhidi ya walemavu miongoni mwa mengine. Utafiti wa Karanja (keshatajwa) unafaa kwa sababu umegusia kipengele cha ukatili unaotekelezwa na wahusika watoto. Suala hili ndilo lililohakikiwa kwa kina katika utafiti huu. Aidha, nadharia ya uhalisia aliyoitumia

ni sawa na iliyotumiwa katika utafiti huu. Vile vile, utafiti huo ulisaidia katika kubainisha matendo ya ukatili na athari zake. Hata hivyo, mtafiti amemshughulikia mtoto kama mhanga wa matukio ya dhuluma ilhali utafiti huu ulimwangazia mtoto kama mhusika katika matendo ya ukatili. Naye Kavuria (2008) ameshughulikia suala la dhuluma dhidi ya watoto kwa kutumia nadharia ya ukata tamaa na ushari. Miongoni mwa dhuluma alizoziangazia ni kujeruhi kimwili, dhuluma za kihisia, unyanyasaji kimapenzi na kutowatunza watoto. Utafiti huu utafaa zaidi kwa sababu vitabu viwili teule miongoni mwa vingine alivyovihakiki pia vilichanganuliwa katika utafiti huu ili kuonyesha jinsi ukatili unavyojitokeza kupitia wahusika watoto. Aidha, utafiti huo uliusaidia huu katika kubaini baadhi ya matendo ya ukatili jinsi alivyoyafafanua na athari zake. Utafiti wa Kavuria (keshatajwa) ni tofauti na huu kwa kuwa yeye amemhakiki mtoto kama mwathiriwa wa vitendo vya dhuluma.

Dunlap (2012) ametafiti kuhusu haki katika hadithi za kifantasia za watoto ili kubaini iwapo adhabu katika hadithi hizo inatekeleza dhima ya kuonyesha kuwa haki imetendeka. Anawasimulia watoto wa shule ya chekechea hadithi zenye miisho ya adhabu na msamaha na kuwaruhusu kuichagua miisho wanayoipendelea. Kisha, anawahoji watoto hao ili kufahamu kwa nini wanazipendelea hadithi zenye miisho fulani. Dunlap (keshatajwa), anahitimisha kuwa watoto hutaka haki na usawa utendeke na wanaweza kutathmini ufaafu wa adhabu. Watoto huziepuka hadithi zenye miisho ya adhabu ya kupindukia au iliyotumia ukatili. Ingawa utafiti wa Dunlap unalenga suala la ukatili katika

adhabu ulisaidia katika kutambua matendo ya ukatili, chanzo na athari zake katika utafiti huu.

Hill (2015) ametafiti kuhusu tanzu za awali zilizobuniwa kwa ajili ya watoto na athari yazo katika riwaya ya uhalisia ya kipindi cha Victorian akitumia nadharia ya uhalisia. Anazichunguza tanzu nne chini ya mada *"School Story", "It-narrative", "The Harm Narrative" na "Family Narrative*". Katika *"Harm Narrative",* mtalaamu huyu anaeleza jinsi ukatili na majeraha katika vitabu vya kwanza vya fasihi ya watoto ulivyopata utambuzi mpana ijapokuwa haukudadisiwa. Msomi huyu anaonyesha jinsi wahakiki kama vile Mc George wanavyokubali kuwepo kwa ukatili katika maandishi, kwa mfano, *"The History of the Fairchild Family"* bunilizi ya Mary Martha Sherwood *(1822)*. Kazi hii inafahamika sana kwa kusawiri picha ya maiti inayoning'inia kwenye kitanzi cha chakari na baba anayeitumia maiti hiyo kama kifaa cha kufunzia. Utafiti wa Hill ulisaidia katika kubaini baadhi ya matendo ya kikatili na athari zake. Hata hivyo, tofauti na ule wa Hill ambaye amemwangazia mtoto kama  mwathiriwa wa vitendo vya ukatili, , utafiti huu ulimwangazia mtoto kama mhusika wa vitendo vya ukatili katika fasihi ya watoto kwa lugha ya Kiswahili.

Mada kuhusu upambanuzi wa hadithi za kifantansia zilizoandikiwa watoto wa shule za msingi imetafitiwa kwa kutumia nadharia ya uhalisiaajabu (Odhiambo, 2017). Mtafiti anaelezea umuhimu wa kuyaangazia maudhui ya kuogofya katika kazi za watoto kama njia mojawapo ya kumtayarisha mtoto kukumbana na

matukio magumu maishani. Baadhi ya maudhui ya kuogofya anayoyaangazia ni mauaji, majeraha ya kimwili na uonevu dhidi ya viumbe wanyonge. Utafiti wa Odhiambo, ulisaidia kubaini baadhi ya matendo ya ukatili katika ngano za kifantasia na athari zake.

Muguro (2018) ameangazia maudhui ya uadilifu katika fasihi ya watoto kwa kutumia nadharia za kisoshiolojia. Ameeleza jinsi waandishi wa msururu wa vitabu vya "*Integrity Series"* wanavyowasilisha maudhui ya uadilifu kwa kuonyesha jinsi wahusika watoto kwa watu wazima wanavyoadhibiwa kwa kujihusisha na sifa mbaya na kupongezwa kwa kushiriki katika matendo mazuri. Aidha, mtafiti amefafanua jinsi mazingira hususan ya shuleni ni muhimu katika kukosoa vitendo viovu kama vile vitisho na dhuluma za watoto dhidi ya wenzao. Ingawa utafiti wa Muguro ni tofauti na huu kwa sababu unaegemea zaidi ufunzaji wa uadilifu, ulifaa katika kubaini baadhi ya matendo ya ukatili yanayojidhihirisha kupitia wahusika watoto katika mazingira ya shule na athari zake kwa wahusika wengine.

Esma na Can (2019) wamefanya utafiti kuhusu ukatili na hofu katika msururu wa vitabu vya Francesca Simon unaoitwa "*Horrid Henry"* kwa kutumia nadharia ya ujifunzaji wa kijamii ya Bandura (1977). Wamechunguza vipengele vinavyoonyesha ukatili na hofu katika msururu huu na athari yavyo katika kukomaa kwa mtoto. Matokeo ya uchunguzi wao yanaonyesha kwamba kuna jumla ya vipengele 185 vinavyoonyesha ukatili. Vipengele 38 kati ya hivi

vinaonyesha ukatili unaokusudiwa kusababisha majeraha ya mwili ilhali 147 vinaonyesha ukatili wa kisaikolojia. Vipengele vinavyoweza kusababisha hofu ni 10 ambapo 6 vinaonyesha hofu inayoweza kusababishwa na binadamu na 4 hofu inayosababishwa na wanyama. Wataalamu hawa wanahitimisha kuwa ingawa msururu wa "*Horrid Henry*" unaweza kuwaathiri watoto kwa njia hasi una mchango wa kuongezea maarifa jinsi ya kutatua migogoro mbalimbali. Wanaolengwa ni watoto wa shule ya msingi ambao wanaweza kuibuka na njia mbadala za kutatua matatizo yao. Utafiti wa Esma na Can (wametajwa) ni tofauti na huu kwa sababu wameungazia ukatili kwa ujumla mno huku wakimdhihirisha mtoto kama mhanga wa matukio ya ukatili katika fasihi ya watoto ilhali utafiti huu ulimwangazia mtoto kama mhusika wa vitendo vya ukatili katika fasihi ya watoto kwa lugha ya Kiswahili. Aidha, watafiti wameufanyia utafiti wao nchini Uturuki; mazingira ambayo huenda yasiakisi tabia ya ukatili jinsi inavyojitokeza kupitia watoto barani Afrika hasa nchini Kenya ambapo utafiti huu umefanyiwa. Hata hivyo, nadharia ya ujifunzaji wa kijamii ya Bandura (1977) waliyoitumia wasomi hawa kuchunguza jinsi mazingira yanavyoweza kuchangia tabia ya ukatili iliufaa utafiti huu pia katika kuchunguza chanzo cha baadhi ya matendo ya ukatili ya watoto. Aidha, ulisaidia utafiti huu katika kubaini baadhi ya matendo ya ukatili na athari yake.

Mwenda (2020) ametafiti kuhusu malezi katika fasihi ya watoto ambapo amefafanua jinsi baadhi ya mbinu za malezi huchangia tabia ya ukatili miongoni

mwa watoto. Utafiti wa mwenda ulichangia katika kuelewa sababu zinazochangia ukatili wa watoto katika fasihi ya watoto.

Watafiti mbalimbali wa fasihi ya watoto wameliangazia suala la ukatili katika vitabu vya fasihi ya watoto kwa upana hivyo basi kutoa mchango muhimu kuhusu mada hii. Hata hivyo, suala la mtoto kama mhusika ambaye anaweza kutekeleza ukatili dhidi ya wahusika wengine katika fasihi ya watoto kwa lugha ya Kiswahili halijahakikiwa kwa kina katika tafiti hizi hivyo basi kuacha pengo muhimu ambalo utafiti huu ulilenga kuziba.

## 1.8 Misingi ya nadharia

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii na ya uhalisia zilitumiwa. Nadharia ya kwanza ililenga kuelezea jinsi ambavyo watoto huiga tabia za watu wazima ilhali ya pili ilisaidia kuelezea jinsi ukatili katika jamii unavyoakisiwa na waandishi wa fasihi.

### 1.8.1 Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii iliasisiwa na Albert Bandura (1977). Waendelezaji wa nadharia hii ni Baltes na Reese (1984). Rosenstock, Strecher na Becker (1988), wanaeleza kuwa nadharia ya ujifunzaji wa kijamii ya Bandura ambayo baadaye aliita ufahamu wa kijamii inashikilia kuwa tabia husababishwa na matarajio na tuzo. Wanafafanua kuwa matarajio yanaweza kuwa ya aina tatu. Kwanza, ni yale yanayohusu mazingira na jinsi matukio yanavyochangiana katika kusababisha tabia. Pili, matarajio kuhusu matokeo yanayoletwa na matendo au tabia ya mtu binafsi. Tatu, ni matarajio kuhusu umilisi au ujuzi wa mtu binafsi wa

kutenda tabia inayotakiwa ili kuchochea matokeo. Rosenstock na wengine (1988) wanaeleza kuwa tuzo ni thamani ya kitu fulani au matokeo. Matokeo yanaweza kuwa hali ya afya, mwonekano wa mtu, wanayosema wengine kuhusu mwingine, mapato miongoni mwa mambo mengine.

McLeod (2016) naye anaeleza kuwa Bandura alikubaliana na nadharia za *Classic conditioning* na *Operent Conditioning za* B.F. Skinner, (*1948)* ila akaongezea dhana mbili muhimu ambazo ni ujifunzaji kwa njia ya kutazama na mchakato wa upatanisho.

**Ujifunzaji kwa njia ya kutazama**

Watoto huwatazama watu wanaowazunguka kwa njia nyingi. Jambo hili linafafanuliwa kupitia jaribio la Bobo Doll (katika Bandura, 1961). Watu ambao wanatazamwa wanaitwa vielelezo. Katika jamii, watoto wanazungukwa na vielelezo vingi kama vile wazazi katika familia, wahusika katika vipindi vya watoto kwenye runinga, marafiki katika makundi yao na walimu shuleni. Vielelezo hivi huwa mfano wa tabia ya kutazamwa na kuigwa. Watoto humakinikia sana watu hawa (vielelezo) na kuhifadhi au kusimba tabia zao. Baadaye huiga tabia waliyoitazama. Wanaweza kufanya hivyo bila kujali iwapo tabia hiyo ni faafu kwa jinsia husika au la ila kuna michakato ambayo hutoa uwezekano kwamba mtoto anaweza kuirudufisha tabia ambayo jamii yake inaiona bora kulingana na jinsia yake.

Mtoto ana uwezo mkubwa wa kuwamakinikia na kuwaiga watu wale ambao kwa mtazamo wake wananasibiana naye. Watu wanaoishi karibu na mtoto wanaweza kuitikia tabia ambayo mtoto ameiga kwa kumwimarisha au kumpasha adhabu. Iwapo mtoto anaiga tabia ya kielelezo na matokeo yake yakawa ya kutuzwa, kuna uwezekano kuiendeleza tabia hiyo. Aidha, mtoto atazingatia kile kinachowatendekea watu wengine wakati wanafanya uamuzi iwapo wataiga vitendo vya mtu mwingine au la. Kwa mfano, msichana ambaye anamtazama dada yake akipewa tuzo kutokana na tabia fulani inawezekana airudie tabia ile yeye mwenyewe.

**Mchakato wa upatanisho**

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii inaelezwa kuwa ni daraja baina ya utabia na mtazamo wa kiakili. Hii ni kwa sababu inaangazia jinsi akili inavyohusika katika ujifunzaji. Ujifunzaji kwa njia ya kutazama hauwezi kutendeka isipokuwa michakato ya kiakili inatenda kazi. Kwa hivyo, mtu hutazama tabia ya kielelezo kwa njia ya "otomatiki" na kuiiga. Kuna mawazo yanayotangulia uigaji na uzingatifu huu ndio unaojulikana kama mchakato wa upatanisho. Kuna michakato minne ya upatanisho ambayo ni pamoja na makini, uhifadhi, urudufishaji na motisha.

Ili tabia iigwe lazima inase makini. Watu hutazama tabia nyingi ila kuna nyingi ya hizo si za kuvuta makini. Kwa hivyo, makini ni muhimu sana katika kuamua iwapo tabia itashawishi uigaji. Aidha, tabia inaweza kutambulika lakini

isikumbukike wakati wote; jambo ambalo linazuia uigaji. Ni muhimu basi tabia kuhifadhiwa ili utendaji utokee kwa mtazamaji. Urudufishaji nao ni uwezo wa kuitekeleza tabia ambayo kielelezo ameionyesha. Watu hutazama tabia nyingi kila siku ambayo wangependa kuiga ila hili haliwezekani. Watu hao huzuiliwa na uwezo wao wa kimaumbile na kwa jinsi hiyo hata ingawa wangependa kuirudufisha tabia hawawezi. Vilevile, motisha kama msukumo wa kuitekeleza tabia ni muhimu katika uigaji wa tabia. Tuzo na adhabu ambayo huandama tabia itazingatiwa na mtazamaji. Iwapo tuzo inayotazamiwa inazidi gharama inayotazamiwa, basi upo uwezekano wa tabia kuigwa na mtazamaji.

### 1.8.2 Mihimili ya nadharia ya Ujifunzaji wa kijamii

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii ina mihimili ifuatayo:

1. Ujifunzaji unaweza kutokea kwa kutazama tabia na matokeo ya tabia yenyewe. Mhimili huu utasaidia katika kuelezea jinsi watoto hujifunza tabia ya ukatili kwa njia ya kuwatazama watu wazima ambao ni vielelezo kwenye jamii.
2. Mwanafunzi hawi mpokezi tu wa ujumbe. Ufahamu, mazingira na tabia vyote huchangiana. Mhimili huu utasaidia kafafanua jinsi kutazama, mazingira na ufahamu huchangiana katika kufunza tabia ya ukatili.
3. Ujifunzaji huhusisha kutazama, kudondoa ujumbe kutokana na mitazamo hiyo na kufanya uamuzi kuhusu matokeo ya tabia. Mhimili huu utasaidia kufafanua sababu zinazochangia tabia za ukatili miongoni mwa watoto na athari za tabia hizo kwa wahusika wengine katika fasihi ya watoto.

4. Uimarishaji tabia huchochea ujifunzaji wa tabia ambapo tabia chanya hutuzwa ilhali tabia hasi huadhibiwa. Mhimili huu utasaidia kuelezea jinsi ukatili miongoni mwa watoto unaweza kudhibitiwa.
5. Watu ambao ni vielelezo katika mazingira ya mtoto ni muhimu katika ujifunzaji wa tabia. Mhimili huu pia utasaidia katika kueleza jinsi ya kuudhibiti ukatili kwa njia ya kutumia vielelezo

Ingawa nadharia ya ujifunzaji wa kijamii inaeleza kwa upana jinsi tabia zinavyoibuka katika jamii na mambo ambayo huchangia uigaji wa tabia, nadharia hii haielezei jinsi tabia hizo zinavyoakisiwa katika mazingira ya sasa. Ni katika msingi huu ambapo nadharia ya uhalisia ilitusaidia kuyaelewa mambo haya kwa kina.

### 1.8.3 Nadharia ya uhalisia

Nadharia ya uhalisia ilipata umaarufu mwanzomwanzo wa miaka ya 1850 ambapo dhana uhalisia na matumizi yake katika fasihi ilianza kujitokeza katika majarida ya Kiingereza kama vile *Fraser's magazine* na *The Westminster Review* (Villanueva, 1997). Nadharia ya uhalisia inahusishwa na wananadharia mbalimbali kama vile Rene Wellek (1961), Niebuhr, Reinhold (1944), Lazaro Catter (1970) miongoni mwa wengine (Villanueva, 1997; Donnelly, 2000). Villanueva (1997) anaelezea uhalisia kama dhana muhimu iliyoelekeza historia ya fasihi na ambayo hujitokeza katika fasihi zote. Anafafanua kwamba uhalisia ulijitokeza kwanza kama nadharia ya fasihi katika ushairi wa Aristotle uliojikita

katika kanuni ya mwigo wa maisha. Msomi huyu anaelezea mipaka ya nadharia hii na kuitofautisha na maswala mengine ya kifilosofia ili kuondoa utata ambao aghalabu huandamana na matumizi yake.

Nadharia ya uhalisia husisisitiza kwamba maisha ya jamii sharti yaangaziwe jinsi yalivyo (Wamitila, 2002). Wamitila (keshatajwa) anafafanua kwamba mwandishi anayeandika kwa kutumia uhalisia husawiri picha ya wahusika, matukio na mandhari kwa njia inayoakisi jamii anamoishi. Mawazo haya yanakubaliana na ya Wafula na Njogu (2007) wanaoshauri kuhusu umuhimu wa mwandishi kuchora picha halisi ya jamii bila kuidunisha wala kuipiga chuku.

### 1.8.4 Mihimili ya nadharia ya uhalisia

Uhalisia una mihimili ifuatayo:

1. Kazi za fasihi zilizoandikwa kwa msingi wa nadharia ya uhalisia huimulika jamii katika ngazi zake zote za maisha. Utafiti utabainisha jinsi ukatili miongoni mwa watoto ulivyo suala halisi katika jamii na kwa nini unapaswa kuangaziwa na waandishi wa fasihi ili kuonyesha athari zake mbalimbali.
2. Waaandishi wa kazi za fasihi ya watoto wanaoongozwa na nadharia hii wanapaswa kuyaangazia matukio, wahusika, mandhari na mazingira katika uyakinifu na uaminifu mkubwa. Katika kuvihakiki vitabu teule, utafiti utaangazia wahusika ambao ni watoto katili katika jamii na mambo mbalimbali ambayo huchangia ukatili huo yakiwamo mazingira na athari za watoto wenyewe katika jamii husika.

Nadharia ya ujifunzaji wa kijamii na nadharia ya uhalisia zimechangiana katika kueleza chanzo cha tabia ya ukatili miongoni mwa watoto, mazingira ya sasa ambamo tabia yenyewe inatokea, athari za tabia yenyewe inavyojidhihirisha katika jamii na kusawiriwa na waandishi wa fasihi ya watoto.

## 1.9 Mbinu za utafiti

Orodho (2003) anaelezea mbinu za utafiti kama utaratibu maalumu unaotumiwa ili kuibuka na majibu ya maswali ya utafiti. Mambo yaliyoangaziwa katika sehemu hii ni pamoja na muundo wa utafiti, eneo la utafiti, uteuzi wa sampuli, mbinu za ukusanyaji data, mbinu za uchanganuzi wa data na mbinu za kuwasilisha matokeo.

### 1.9.1 Muundo wa utafiti

Muundo wa utafiti ni mwongozo wa kutimiza malengo na kupata majibu ya maswali ya utafiti kwa kufuata utaratibu maalumu(Kothari,2007). Ili kuafikia malengo yaliyoratibiwa, utafiti huu ulitumia muundo wa kimaelezo. Muundo wa kimaelezo ulifaa kwa sababu maelezo yalihitajika katika kutoa ufafanuzi na ulinganishi jinsi ukatili unavyojitokeza miongoni mwa watoto na jinsi ukatili wenyewe ulivyoangaziwa na waandishi wa vitabu teule vya fasihi ya watoto. Mugenda na Mugenda (1999),wanafafanua kwamba utafiti wa kimaelezo hutoa ripoti ya jinsi mambo yalivyo katika mazingira fulani na hueleza tabia, mielekeo, itikadi na hali mbalimbali za watu.

### 1.9.2 Eneo la Utafiti

Utafiti ulijikita maktabani. Data ya msingi ilipatikana kwa kuvisoma vitabu teule. Aidha, utafiti ulinufaika kutokana na makala muhimu yaliyoandikwa kuhusu mada, nadharia husika, tafiti nyingine na matini mengine muhimu.

### 1.9.3 Uteuzi wa sampuli

Kothari (2007) anaeleza sampuli kama sehemu ya kitu au watu fulani ambao huteuliwa na kutumiwa kwa minajili ya kufanya maamuzi yanayohusu kundi zima. Utafiti ulitumia sampuli kusudio ambapo uchanganuzi ulifanywa kuhusu watoto katili katika vitabu teule vya fasihi ya watoto. Riwaya tatu za waandishi tofauti ambazo zinalenga hadhira ya watoto na vijana zilitumiwa kuchunguza jinsi waandishi walivyoshughulikia watoto katili katika kazi hizo. Riwaya hizo ni:

1) *Siku Njema* (Walibora, 1996)
2) *Tumaini (*Momanyi, 2006)
3) *Lulu ya Maisha* (Habwe,2013)

### 1.9.4 Mbinu za ukusanyaji data

Kothari (2004) anaeleza kwamba katika kutafiti kuhusu tukio halisi la maisha, data aliyo nayo mtafiti mkononi haitoshi hivyo basi itambidi kukusanya data faafu kwa kutumia mbinu mbalimbali zinazopatikana. Data ya msingi katika utafiti huu ilipatikana kwa kuvisoma kwa makini vitabu teule na kuyanukuu yale yanayohitajika kwenye mwongozo wa ukusanyaji data. Aidha, utafiti ulihusisha

usomaji wa vitabu kuhusu nadharia na makala, majarida, magazeti na tasnifu kuhusu mada ya utafiti.

### 1.9.5 Mbinu za uchanganuzi wa data

Data iliyopatikana kwa kuvisoma vitabu teule vilivyotajwa iligawanywa kwenye makundi na kuchanganuliwa kwa kutumia mwongozo wa uchanganuzi. Mwongozo huo ulizingatia malengo ya utafiti, nadharia husika, na makala mengine muhimu.

### 1.9.6 Mbinu za kuwasilisha matokeo

Maelezo ya kina yametolewa kuhusu aina za ukatili wa watoto katika vitabu teule, sababu zinazochangia matendo ya ukatili na athari zake kwa wahusika wengine. Maelezo yalizingatia nadharia na makala mengine husika. Matokeo yamejumuisha hitimisho na mapekendekezo ya utafiti.

### 1.9.7 Maadili

Utafiti huu umezingatia taratibu maalumu za maadili. Mtafiti alipata kibali cha kufanya utafiti kutoka kwa NACOSTI na ruhusa ya Chuo Kikuu cha Kenyatta ya kufanya utafiti.

# SURA YA PILI

# AINA ZA UKATILI WA WATOTO KATIKA VITABU TEULE VYA FASIHI YA WATOTO

## 2.0 Utangulizi

Wataalamu mbalimbali wameeleza kuhusu yale yanayolifanya tendo kuitwa katili (kwa mfano, Stepanek, 2013; Leach, 2014; Chamandar & Jabbari, 2017). Kulingana na Stepanek , kitendo kinaelezewa kuwa cha ukatili iwapo pana matumizi ya nguvu kwa nia ya kusababisha majeraha, maumivu ya kisaikolojia au kifo. Leach (2014) naye anaeleza kuwa ili kitendo kiweze kufasiliwa kama cha ukatili ni sharti kiwe na nia ya kuumiza kimwili na kisaikolojia. Chamandar & Jabbari (wametajwa) wanafafanua kwamba kitendo cha ukatili hubainika kwa kuitazama dhamira ya mtendaji. Mitazamo ya wataalamu hawa ni kwamba kitendo ni katili iwapo dhamira ya mtendaji ni kujinufaisha mwenyewe kwa kupuuza haki za wengine. Kutokana na mitazamo hii, inabainika kwamba ukatili unaweza hujidhihirisha kwa matendo ya aina mbalimbali baadhi yao yakiwa bayana kuliko mengine.

Sura hii imechanganua aina za ukatili zinazodhihirika katika vitabu vilivyoteuliwa vya fasihi ya watoto. Mhimili wa nadharia ya uhalisia unaoeleza kwamba waandishi wa kazi za fasihi huyaangazia matukio, wahusika, mazingira na mandhari kwa uyakinifu na uaminifu umetumikizwa ili kuelewa jinsi watoto katili walivyosawiriwa na waandishi wa vitabu teule. Muhtasari wa vitabu hivi

umetolewa ili kuyaelewa matukio muhimu kabla ya kuzichanganua aina za ukatili.

### 2.1.1 Siku Njema (1996)

Riwaya ya *Siku Njema* imeandikwa na Ken Walibora na kuchapishwa na *Longhorn Publishers* mwaka wa 1996. Inasimulia safari ya Kongowea Mswahili ya kumsaka baba yake. Mwandishi anautanguliza ukoo wa kuukeni wa mamaye Kongowea Mswahili, Zainabu Makame. Mzee Mwinyi Makame, ambaye anamzaa Zainabu katika umri wa uzee ana wake kumi na wawili. Zainabu Makame ni kitindamimba wa mke wa mwisho wa mzee huyo.

Mwinyi Makame anapoaga dunia, mji wake unakumbwa na masaibu mbalimbali yakiwemo mizozo ya ukewenza. Matatizo hayo yanapofikia kiwango cha kutostahimilika, mamaye Zainabu Makame anahamia nyumbani kwao katika kijiji cha Chongoleani, Mkoa wa Tanga. Ni hapa Tanga ambapo Kongowea Mswahili anazaliwa. Anazaliwa wakati ambapo sifa za mama yake za utunzi na uimbaji wa nyimbo za taarab zilikuwa zimezagaa ndani na nje ya taifa la Tanzania. Kongowea anapotimu umri wa kuenda shule, mama yake anampeleka katika shule ya Tanga ambapo anasajiliwa.

Katika shule ya Tanga, baadhi ya wanafunzi wanadhihirisha ukatili kwake kwa kumdhihaki na kumwita ‘mwanaharamu’ na ‘kikojozi’ kila wakati alipowashinda masomoni. Anaitwa mwanaharamu kwa sababu mama yake anamzaa nje ya ndoa. Kitendo cha kuitwa mwanaharamu kinamkera Kongowea Mswahili na

kumkosesha furaha daima. Heshima aliyo nayo kwa mama yake inamzuia kumkabili na kumwuliza amweleze kuhusu yule aliyekuwa baba yake.

Mhusika mwingine ambaye matendo yake ya ukatili yanamwathiri Kongowea Mswahili ni Selemani Mapunda. Mapunda ambaye alisoma darasa moja na Kongowea Mswahili anamuumbua waziwazi kwa kumwita 'mwanaharamu msi baba'. Inasemekana kwamba Mapunda alikwenda kwa mganga mmoja katika mji wa Tanga kuganguliwa akaambiwa kwamba kushindwa kwake masomoni kulisababishwa na Kongowea Mswahili.

Mapunda ambaye hakupenda kuoga anaamrishwa na mwalimu mkuu kuvua nguo na kuoga mbele ya wanafunzi waliokusanyika kwenye gwaride. Jambo hilo linamfanya kutoroka na kufanya uamuzi wa kutorudi shuleni tena. Kuanzia wakati huo, vitendo vyake vya ukatili vinakithiri. Akiwa kwenye genge la majambazi wanamshambulia hedimasta, wanampiga kipopo na kumjeruhi vibaya. Kongowea Mswahili anaporipoti tukio hili kwa polisi, Selemani Mapunda anaamua kulipiza kisasi kwa kumwinda ili kumwangamiza.

Mama yake Kongowea Mswahili anaugua maradhi yasiyokuwa na tiba yanayomtaabisha kwa siku nyingi. Anapoaga dunia, anamwachia ndugu yake, Kitwana, wajibu wa kumlea Kongowea Mswahili. Hata hivyo, mkewe Kitwana, Mwanasaumu, anamchukia Kongowea Mswahili kwa sababu ya wivu. Mwandishi anaeleza kuwa Kongowea Mswahili alikuwa mwerevu kuliko watoto wa Mwana

Saumu. Wivu huo unamfanya kumtumia Kongowea Mswahili kufanya kazi zote za nyumbani huku watoto wake wamepakata mikono.

Kilele cha chuki ya Mwana Saumu ni jaribio la kutaka kumwua Kongowea Mswahili kwa kumtilia sumu kwenye chai ya mkandaa. Kitendo hiki cha wivu kinatokana na kufaulu kwa Kongowea katika mtihani wake wa kitaifa. Mjomba Kitwana ambaye alikuwa radhi kuyafadhili masomo ya kijana huyu, anashambuliwa na maradhi katika mkono wake. Maradhi hayo yanamnyima fursa ya kuendelea na kazi yake ya useremala.

Kongowea Mswahili anapokea barua ya mwaliko kujiunga na shule ya upili ya kitaifa ila anakosa msaada wa ufadhili. Anaamua kuhamia mji wa Mombasa kuanza safari ya kumsaka baba yake ambaye kulingana na maelezo ya Bi. Rahma, msiri wa mama yake, alikuwa anaishi katika eneo moja la bara nchini Kenya.

Jambo jingine linalomfanya Kongowea Mswahili kuhama Tanga ni barua anayoipokea kutoka kwa Selemani Mapunda ambaye alikuwa ametoka jela alikofungwa kwa kumjeruhi mwalimu mkuu. Selemani anatishia kumwua Kongowea Mswahili kwa kudai kuwa ndiye aliyemchongea akafungwa jela. Siku ya kuhama kwa Kongowea Mswahili kutoka Tanga, Mapunda anapatikana na bastola ambayo inasemekana angeitumia kumwua Kongowea Mswahili.

Kongowea Mswahili anapowasili katika mji wa Mombasa, anatarajia kukutana na mjomba wake mwingine aliyeitwa Salim ili awe mwenyeji wake. Hata hivyo,

mjomba huyo ambaye alikuwa anajulikana kama Mpendaraha alikuwa ametoweka kwa njia ya kutatanisha. Baadhi ya wakazi wa Mombasa walisema kwamba yamkini matendo ya wizi na unyanganyi ya Bakari, mwanawe Salim, ndiyo yaliyokuwa yamemwaibisha akaamua kujitosa baharini. Mkewe Salim, Wamboi, naye ni majununi anayeokota vitu katika mji wa Mombasa. Vitendo vya mwana wao, Bakari vinashtadi. Anageuka na kuwa jizi hodari katika mji wa Mombasa.

Selemani Mapunda anatoroka jela na kutorokea mji wa Mombasa ambapo sadfa inamkutanisha na Bakari anayeshirikiana naye katika vitendo vya uvunjaji sheria. Selemani Mapunda anauendeleza ukatili wake dhidi ya Kongowea katika mji wa Mombasa. Ni katika mji huu ambapo Mapunda na Bakari wanashirikiana kuwahangaisha wakazi wa Mombasa kupitia vitendo mbalimbali vya ukatili.

Malezi ya kudekeza yanaelezewa kuwa sababu ya kuathirika kwa Bakari kihulka. Salim aliselelea katika vilabu vya pombe na kupuuza malezi ya kijana mwenyewe. Kwa upande mwingine, Wamboi alimdekeza sana Bakari kwa kumpa kila alichotaka. Rashid, mwenyeji wa Kongowea Mswahili, anamweleza kwamba Bakari ni jizi hodari na sugu wa jela. Tukio mojawapo linaloonyesha wizi wa Bakari ni wakati anaponyakua kipochi cha mwanamke mmoja mtalii; jambo linalomfanya kuvamiwa na umati wenye hasira na kupigwa kitutu.

Selemani Mapunda anaandika ujumbe wa kutisha katika choo cha wapangaji akimwarifu Kongowea Mswahili kuwa alikuwa amewasili Mombasa na kwamba

angemwua. Ujumbe huu pamoja na tukio mojawapo ambapo Kongowea anamwona Selemani Mapunda akiandamana na Bakari vinamfanya Kongowea Mswahili kuharakisha safari yake ya kuelekea bara kumtafuta baba yake.

Katika mji wa Kitale, Bi Mercy Macdonald, mkewe mlowezi anayeitwa Macdonald, anamwauni Kongowea Mswahili anapokumbwa na homa ya mkunguru katika mkahawa mmojawapo. Anampeleka nyumbani kwake na kukaa naye kama mwanawe mpaka sadfa inapomkutanisha baba yake, Bwana Juma Mukosi. Juma Mukosi alikuwa amesuluhia kuishi maisha ya upweke. Kutokana na hali hiyo, watu walimwambaa. Hadithi inakamilika pale ambapo Kongowea Mswahili anamzika baba yake kulingana na maagizo anayomwachia kabla ya kufa. Hatimaye anarithi mali ya baba yake.

**2.1.2 Tumaini (2006)**

Riwaya ya *Tumaini* imeandikwa na Clara Momanyi na kuchapishwa na *Vide - Muwa publishers Limited* mwaka wa 2006. Riwaya hii inahusu msichana anayeitwa Tumaini ambaye anajitahidi kujitanzua kutoka kwenye mila hasi zinazomnyanyasa mtoto wa kike. Tumaini ni kifunguamimba katika familia ya watoto wanne – watatu wa kike na mmoja wa kiume. Baba yake, Mzee Masumbuko, anasifika sana katika mtaa wa Mbuyuni kutokana na tabia yake ya kuwalea wanawe kwa ukatili uliopindukia.

Tabia yake ya ukatili inamwathiri kitindamimba wake, Idi, ambaye anaonesha ukatili kwa Tumaini na dada zake wengine kupitia kauli zake zinazowadhihirisha

kama bidhaa zilizohifadhiwa nyumbani zikingoja wakati mwafaka wa kuuzwa. Aidha, kila wakati Idi anapoombwa na Tumaini kumsaidia katika kazi za nyumbani, anakaidi kwa kusema kuwa kazi za aina hiyo ni za wanawake. Juhudi za Tumaini za kurekebisha tabia ya Idi hazifaulu kwa sababu Mzee Masumbuko anamwambia kinaganaga aachane na Idi kwa sababu ni mtoto wa kiume si wa kike.

Katika shule ya Kivulini anakosomea Tumaini kunao wanafunzi wengine wanaodhihirisha ukatili kupitia matendo yao. Majuto na Kijungwe ni miongoni mwa wanafunzi hao ambao wanaelezewa kwamba wana ubwete na ubwege unaotishia usalama wa wanafunzi wenza na walimu. Majuto ni mtoto wa Chifu Andrea ambaye amelelewa kwa kutendekezwa mno akaishia kupotoka kitabia. Wakati mmoja, akishirikiana na Kijungwe wanavunja ofisi ya mwalimu mkuu, Bwana Mwadime, na kuiba madaftari ya shule kisha wanamwuzia mmiliki wa duka la jumla anayeitwa Karim.

Aidha, Majuto anamrushia mwalimu wake mawe kupitia dirishani na kutishia si tu usalama wa mwalimu huyo bali pia wanafunzi. Mwalimu anawaamrisha wanafunzi kumkimbiza Majuto lakini Majuto anawapiku mbio na kutorokea mbali asirudi tena shuleni. Baada ya kuwaasi walimu, anageuka lofa anayezurura ovyo mitaani ambapo anawaibia watu mali yao na kuwabaka mabinti zao. Katika tukio jingine, Majuto anakimbizwa na vijana kwa kuiba baiskeli yao ambayo anaiendesha kwa kasi na kutokomea katika mtaa wa mabanda wa Mkwajuni.

Chifu Andrea, baba yake Majuto, anatumia cheo chake kuvihonga vyombo vya dola ili viyafunike makosa ya Majuto. Mwandishi anaeleza kwamba kila wakati wazazi wa wasichana waliodhulumiwa na Majuto walipoleta mashtaka kwa Bwana Andrea, aliwapuuza. Wazazi hao walipoamua kupeleka mashataka yao kortini, Andrea aliwahonga mawakili na hata mahakimu wakatupilia mbali mashtaka. Jambo hili linamfanya Majuto kukithiri katika matendo ya ukatili. Yeye na vijana wa hirimu yake wanamkaba koo mke wa mfanyabiashara anayeitwa Karim na kumwibia kisanduku chenye vitu vya thamani. Kilele cha matendo ya ukatili kinakuwa jaribio la wizi katika ofisi ya D.O ambapo Majuto na Kijungwe wanapigwa risasi za miguuni na kutiwa mbaroni.

Licha ya Kijungwe kuwa mshirika wa Majuto katika matendo mbalimbali ya ukatili, ni kijana mwenye kinywa kilichojaa matusi. Wakati mmoja, anamdhihaki Tumaini kwa kumwambia kuwa aliasi tohara ya wasichana kwa sababu ya kuogopa kisu cha ngariba.

Tumaini anapokamilisha masomo yake ya darasa la saba katika shule ya Kivulini, baba yake anaanza kutayarisha tohara yake. Kuwasili kwa mwanamke ambaye angemfunza mambo ya unyagoni nyumbani kwao kunamdokezea kwamba mipango ya tohara ilikuwa imekaribia. Anaamua kutorokea nyumbani kwa shangaziye, Bi. Halima. Maadamu, Bi. Halima ni mmoja wa wanaharakati wa kikundi kilichopinga tohara ya wasichana, anamnusuru Tumaini kutoka kwenye mipango miovu ya Mzee Masumbuko, baba yake Tumaini.

Mzee Masumbuko ambaye anapandwa na hasira anamwamrisha mkewe kumtafuta Tumaini na kumrejesha nyumbani ili akatahiriwe ima fa ima. Hata hivyo, Bi. Halima na mumewe, Shabani, wanamweleza Mzee Masumbuko kwamba hawatamshurutisha Tumaini kutahiriwa kinyume na matakwa yake. Isitoshe, wanamwambia kuwa kumtahiri msichana kulikuwa kinyume cha sheria. Kauli hizi zinamwudhi sana Mzee Masumbuko ambaye anasuka mpango mwingine wa kumwoza Tumaini kwa Mabruk, mwana wa Mzee Sulemani. Mzee Masumbuko anasingizia kwamba kumwoza Tumaini kwa Mabruk kungemwondolea aibu ya kusemwa kwamba alikuwa anaishi na msungo au msichana ambaye hajatahiriwa.

Siku ya Mzee Selamani ya kwenda kumposa bintiye Masumbuko inapangwa. Masumbuko anawaalika tu jamaa na marafiki waliounga mkono mipango ya kumwoza bintiye. Siku ya sherehe inapowadia, mzee huyo anapigwa na butwaa Bi. Halima na mumewe Shabani pamoja na Yusufu, kakake Bi. Amina, wanapohudhuria bila mwaliko.

Baada ya wageni kukaribishwa vizuri na kuandaliwa meza, Mzee Sulemani anaiweka wazi sababu ya kuwasili kwao nyumbani kwa Masumbuko. Hata hivyo, yeye na ujumbe wake wanatamaushwa wanapoelezwa kwamba jamaa hawakuwa na habari kuhusu mpango wa kumwoza Tumaini. Isitoshe, Yufusu anaeleza wazi kuwa Tumaini alikuwa angali mwanafunzi. Mabishano kati ya Masumbuko na

jamaa yake yanavuruga sherehe ambapo wageni wanaondoka bila kutimiza kusudi lao.

Tumaini ambaye sasa anaishi kwa shangaziye, Bi. Halima, anarudi shuleni kuendelea na masomo yake ya darasa la nane. Baada ya kuufanya mtihani wa darasa la nane anakwenda kwa Chifu Andrea kumsaidia mkewe kazi za nyumbani huku akiendelea kungoja matokeo. Majuto anaonyesha ukatili wake kwa Tumaini kwa kutaka kumbaka. Fauka ya hayo, Chifu Andrea naye anajaribu kumdhulumu kimapenzi. Vitendo vya ukatili vya watu hawa wawili vinamfanya Tumaini kuacha kazi na kurudi kwa shangaziye.

Baada ya matokeo ya mtihani wa darasa la nane kutangazwa na Tumaini kufaulu vyema, Masumbuko anapeleka hongo kwa Chifu Andrea na wawili hao wanakula njama ya kuliondoa jina lake kwenye orodha ya wanafunzi ambao wangepokea ufadhili wa serikali. Tumaini anaishinda njama hii anapojitambulisha kwa D.O siku ya kukaguliwa kwa majina ya wanafunzi watatu ambao wangenufaika na ufadhili wa serikali. D.O anamkemea Chifu kwa kula njama na Mzee Masumbuko kumnyima Tumaini nafasi ya ufadhili wa masomo. Mzee Masumbuko pia anaamrishwa kufika mbele ya D.O ambapo anapewa onyo kali dhidi ya njama zake za kumzuia bintiye kuendelea na masomo yake.

Tumaini anajiunga na shule ya upili ya *Milimani Mission School* ambapo anafanya bidii masomoni akiwa na matumaini ya kufuzu vyema na kujiunga na chuo kikuu ili kusomea taaluma ya udaktari. Riwaya inakamilika kwa mseto wa

hisia za furaha na huzuni. Furaha kwa sababu Tumaini anafaulu vyema katika mtihani wa kidato cha nne na kuitwa katika chuo kikuu kwenda kuisomea taaluma ya udaktari. Huzuni inadhihiri Majuto na Kijungwe wanapohukumiwa kufungwa jela miaka minne na kazi ngumu kutokana na matendo yao ya uvunjaji sheria. Bi Selina, mkewe Chifu Andrea anazoroteka kiafya kutokana na habari za kufungwa kwa mwanawe.

### 2.1.3 Lulu ya Maisha (2013)

Riwaya ya *Lulu ya Maisha* imeandikwa na John Habwe na kuchapishwa na shirika la *The Jomo Kenyatta Foundation* mwaka wa 2013. Riwaya hii inasimulia kuhusu masaibu yanayowakumba Omido na Sue, wana wa Bwana na Bi.Tiito. Wazazi hawa wanaaga dunia kutokana na janga la ukimwi. Omido anapotoka kitabia na kuwa katili kutokana na ushawishi wa vijana wa hirimu yake anaokutana nao katika mtaa wa mabanda wa Kisera.

Hadithi inaanza kusimulia kuhusu kujumuishwa kwa Tiito kwenye kikosi cha Umoja wa Mataifa kinachotumwa nchini Sierra Leone kuhifadhi amani. Familia yake inafurahi kwa sababu angepata marupurupu zaidi ambayo yangeifanya kuishi maisha mazuri. Katika uwanja wa ndege mkewe Tiito anamuaga na kumshauri kujihadhari akiwa huko Sierra Leone.

Muda wa Tiito wa kuhudumu nchini Sierra Leone unapokamilika, anarejea nchini na kulakiwa vyema na aila yake. Anayatumia marupurupu anayoyapata ughaibuni kununua gari zuri, samani mpya, vyombo vipya vya elektroniki na kuboresha

maisha ya aila yake. Haupiti muda mrefu kabla ya Tiito kuanza kuugua. Vipimo anavyofanyiwa hospitalini vinaonyesha kwamba anaugua ukimwi. Habari hizo zinabadili maisha ya aila yake. Mkewe anamlaumu kwa kuchuma janga la ukimwi akaishia kumwambukiza.

Tiito anatoka hospitalini anakolazwa kwa muda mrefu na kurejea kazini. Hata hivyo, hali yake ya afya haimruhusu kuendelea kutekeleza majukumu yake hivyo basi anashurutika kustaafu mapema. Pesa zote anazozipata baada ya kustaafu zinaishia katika matibabu. Maisha yanaibadilikia aila kwani haina tena pesa za kukidhi mahitaji ya msingi. Tiito anapoaga dunia, mkewe na watoto wake wanakumbwa na majonzi. Nduguze Tiito wanatwalia kila kitu alichomiliki likiwamo shamba la nyumbani.

Mkewe Tiito anashindwa kumudu kodi ya nyumba katika mtaa wa kifahari wa Onyonka na kushurutika kuihamisha aila yake hadi mtaa wa mabanda wa Kisera. Ni hapa Kisera ambapo Omido anashawishiwa na kundi la vijana wa hirimu yake linalojiita RIZIKI na anajiunga nalo. Kijana huyu anashawishiwa na genge hili na kujitosa katika matukio ya uvunjaji sheria. Anavunja nyumba za watu na kuwaibia mali yao, analeta magenge ya wezi ambayo yanawaibia majirani zake. Licha ya hayo, anaanza kutumia dawa za kulevya waziwazi bila kuwachelea polisi. Isitoshe, akiwa na wenzake, wanatekeleza wizi wa kimabavu katika duka la Bwana Sultani.

Fazul na Fatila ni vijana wengine wanaotekeleza ukatili kwa sababu ya mazingira yanayowazunguka. Mwandishi anaeleza kwamba vijana hawa wawili ambao walioana wakiwa watoto wanaishi maisha ya uchochole. Fazul alipolea vibaruani katika mabohari ya viwandani ilhali Fatila alikuwa mke wa nyumbani. Fazul alipowasili nyumbani bila kubeba chochote, Fatila alimrushia cheche za matusi na kumfedhehesha kwa majirani waliowasikiliza. Baada ya matusi vijana hawa walipigana na kuumizana vibaya.

Mama yake Omido anapoaga dunia anazikwa kwenye maziara ya Lang'ata. Sue anaingilia kazi ya kuokota chupa anazoziuza ili kujipatia riziki. Siku moja akiwa katika shughuli ya kuokota chupa anawaona wezi walioiba pesa kwenye benki ya *Africa Accounts* wakizificha kwenye pipa mojawapo la kuhifadhia takataka. Anazipeleka pesa hizo kwenye kituo cha polisi ambapo meneja wa benki hiyo, Bwana Onokoye, anaitwa ili kuzitwalia.

Riwaya inapokamilika, Bwana Onokoye anampa Sue kiangazamacho cha shilingi milioni moja na kuahidi kuyafadhili masomo yake hadi kiwango chochote ambacho alitaka kufika. Onokoye anamtafutia shule ya St. Mary's Girls Primary Boarding ambayo anajiunga nayo ili kukinai kiu yake ya masomo. Katika shule hii, baadhi ya wanafunzi washari wanamkaribisha kwa kumwamrisha kuimba kidogo, kulia na kuwaita viranja wao kwa jina 'your honour'.

Omido anauawa na polisi kutokana na vitendo vyake vya uvunjaji wa sheria. Jambo hili ndilo linalomhuzunisha sana Sue kwa sababu huyo ndugu yake hakupata fursa ya kuyaendelea masomo yake kama ile aliyoipata yeye.

### 2.1.4 Aina za ukatili wa watoto zinazobainika katika riwaya teule

Wataalamu wameugawa ukatili katika makundi matatu: ukatili wa kimatendo, wa kimatamshi na wa kuwaziwa (Young, Boye & Nelson, 2006 ;.Chamandar & Jabbari, 2017; Leach, 2014.; Coyne, Archer & Eslea, 2006; Murray, Eisner & Ribeaud, 2018). Sehemu itakayofuata itachanganua aina hizi za ukatili jinsi zinavyojitokeza katika vitabu vilivyoteuliwa vya fasihi ya watoto. Matendo ya ukatili yanatambulika kupitia yale wanayoyafanya wahusika, kuyatamka, au wasifu wa wahusika kuhusu wahusika wenza (Wamitila, 2002).

### 2.1.5 Ukatili wa kimatendo

Kulingana na Young, Boye & Nelson (2006), ukatili wa kimatendo unahusu kusababisha majeraha au kutishia kusababisha majeraha hayo. Katika riwaya ya *Siku Njema*, Walibora (1996) amesimulia kuhusu Selemani, mwana wa Mapunda anayemvua nguo hedimasta wa shule ya Tanga, kumpiga na kumjeruhi vibaya kwa kushirikiana na vijana wenzake . Mapunda anatekeleza kitendo hiki cha ukatili ili kulipiza kisasi dhidi ya mwalimu huyo ambaye awali alimwamrisha kuvua nguo na kuoga mbele ya wanafunzi na walimu waliokusanyika kwenye gwaride.

Hivi ndivyo tukio la kupigwa kwa mwalimu linavyosimuliwa na Kongowea Mswahil:

> “Yule mwanaume aliyepigwa na kugaragara chini uchi alikuwa hedimasta wetu. Alikuwa kajeruhiwa vibaya kichwani. Damu ilimtoka kwa wingi. Kisha nikamuona Selemani. Macho alikuwa kayatoa pima na mkononi kashika kigongo huku majasho yanamtoka. Alihema kwa uchovu....”(uk. 21).

Mwandishi amesawiri picha ya Selemani Mapunda akiwa ametokwa na macho pima huku mkononi amebeba kigongo ambacho anakitumia kumjeruhi mwalimu wake kichwani. Pokhrel, Sussman, Black & Sun (2010) wanafafanua kuwa kumpiga mtu kwa kutumia silaha kama vile gongo, kisu, bunduki na kadhalika na kumsababishia majeraha ya kimwili ni ukatili. Mwandishi amekiakisi kitendo hiki kwa usahihi kwa kuzingatia mhimili wa uhalisia unaoeleza kuwa waandishi wa fasihi ya watoto huyaakisi matendo kwa uyakinifu na uaminifu. Matendo haya hutokea mara kwa mara katika shule mbalimbali nchini Kenya. Kwa mfano, katika gazeti la *The Standard* Abuga (2021) anasimulia tukio ambapo mwanafunzi wa kidato cha tatu katika Shule ya Upili ya Kisii anasemekana kuwadunga walimu wawili kisu na kuwajeruhi vibaya alipoulizwa kuelezea sababu iliyomfanya kuchelewa kuwasili shuleni.

Katika riwaya ya *Tumaini* (2006), kinasimuliwa kisa cha Majuto, mwana wa Bwana Andrea, mwenye tabia inayotishia usalama wa wanafunzi na walimu katika shule ya Kivulini (uk. 20). Wakati mmoja, Majuto anamvurumizia mwalimu wake, Bwana Mwadime, mawe kupitia kwenye madirisha ya darasa lao.

Bwana Mwadime anashurutika kujificha chini ya meza ili kuyakwepa mawe hayo yanayotupwa kwa kasi (uk.27). Majuto anakitekeleza kitendo hiki kwa sababu ya kuamrishwa na Bwana Mwadime kupiga magoti kisha anamfukuza nje ya darasa. Ijapokuwa Majuto hadiriki kumjeruhi mwalimu wake, kitendo hiki kinafasiliwa kuwa cha kikatili kwa sababu nia yake ilikuwa kujeruhi anavyoeleza Onukwufor (2013:62):

> "Mwuguzi ambaye anamdunga mgonjwa wake sindano chungu hawezi kusemekana kuwa katili kwa sababu hakuwa na nia ya kuumiza. Hata hivyo, mwanafunzi aliyemtupia mwenzake jiwe lakini likamkosa ni katili kwa sababu alikuwa na nia ya kujeruhi.''(tafsiri ya mtafiti).

Mwandishi wa riwaya ya *Tumaini* vile vile amekiakisi kitendo cha Majuto kwa uyakinifu na uaminifu ikizingatiwa kwamba matukio ya wanafunzi kuwatupia walimu wao mawe au kuwatishia kwa silaha hatari yamekuwa yakiangaziwa katika jamii na vyombo mbalimbali vya mawasiliano. Katika *The Daily Nation,* Ochunge (2021) anasimulia jinsi mwanafunzi wa darasa la sita katika shule ya msingi ya Shihumbi anavyosemekana kumwua mwalimu wake, Bw. Khataka, kwa kumpiga jiwe kwenye paji la uso kwa sababu marehemu alimzuia kuteka maji kwenye kisima chake.

Katika riwaya ya *Tumaini*, Tumaini anadhihirisha ukatili kwa kumrushia Kijungwe jiwe ambalo linaishia kumjeruhi mwalimu wao (uk. 73). Tumaini anakitekeleza kitendo hiki kutokana na hasira ya kudhihakiwa na Kijungwe kwamba alitoroka tohara kwa sababu ya kuogopa kisu cha ngariba. Ijapokuwa kitendo cha Tumaini kilikuwa cha kujihami dhidi ya ushari wa Kijungwe, ni cha

kikatili kwa kuwa ukatili si njia mujarabu ya kusuluhisha migogoro (Nimon, 1993). Nao Chamandar & Jabbari (2017) wanaeleza kuwa vitisho vya kujitetea dhidi ya ukatili unaoelekezwa kwako na mtu mwingine vinafasiliwa kuwa ukatili. Kitendo cha Tumaini kimeakisiwa kwa uyakinifu na uaminifu kwa sababu picha ya wanafunzi kugeukia ukatili kama njia ya kujitetea dhidi ya ukatili wa wenzao au kusuluhisha migogoro baina yao hujitokeza aghalabu katika jamii. Ongwae (2021) anasimulia tukio ambapo mwanafunzi wa shule ya msingi ya Bogwendo katika kaunti ya Nyamira anasemekana kumdunga mwenzake kisu na kumwua baada ya kugombania umiliki wa kalamu ya wino.

Kisa kingine cha ukatili kinachosimuliwa katika riwaya ya *Tumaini* kinahusu Waridi, mwanafunzi wa kike wa shule ya Kivulini anayemshambulia msichana anayeitwa Masika kwa sababu ya wivu wa kimapenzi. Waridi alimtaka kimapenzi mvulana aliyeitwa Paulo, mpenziwe Masika, ila Paulo akamwambia Waridi waziwazi mbele ya Masika kwamba hampendi. Jambo hilo lilimchoma Waridi moyoni akaamua kulipiza kisasi kwa kumdhihaki, kumtusi na kuanzisha vita baina yake na Masika. Hii ndiyo taswira ambayo mwandishi anaichora kuhusu tukio hilo:

> “Papo hapo, hasira zilimpanda Waridi, macho yakaiva kwa wingi wa hamaki. Alitupa ndoo aliyokuwa ameishika mkononi na kumrukia Masika jinsi kozi anavyomrukia kifaranga. Alianza kumbigija koo, huku Masika akijitahidi kuimamanua mikono ya Waridi iliyokazana shingoni mwake”.(uk. 111-112).

Kitendo cha watu wawili au kundi la watu kupigana inavyotokea baina ya Waridi na Masika kinaelezewa kuwa ukatili ( Onukwufor, 2013). Aidha, utafiti uliofanywa umeonyesha kwamba katika umri wa kuvunja ungo, watoto wa kike hujihusisha katika ukatili kwa sababu ya kutaka kutambuliwa na kupendwa (Owens, Shute, & Slee, , 2000). Mwandishi wa riwaya ya *Tumaini* ameuakisi ukatili huu kwa uyakinifu na uaminifu.

Tukio jingine la ukatili kwa njia ya kupigana linaangaziwa katika riwaya ya *Lulu ya Maisha* (2013) kupitia wahusika Fazul na Fatila. Mwandishi anaeleza kuwa vijana hao wawili ambao walioana wakiwa watoto walipigana na kuumizana (uk. 63-64). Vijana hawa wanapigana kwa sababu ya mambo madogo madogo. Kwa mfano, Fazul aliyetarajiwa kukidhi mahitaji ya chakula, wakati mwingine alifika nyumbani mikono mitupu hivyo basi ikambidi Fatila amzomee na ugomvi wenyewe ukaibua vita. Kitendo hiki cha Fatila na Fazul kupigana ni cha kikatili kwa mujibu wa Onukwufor (2013)

Aidha, katika riwaya hiyo, kuna msichana anayeitwa Semo ambaye anapigwa na watoto wa halati yake na kutumiwa kama msichana wa nyumbani (uk. 17). Msichana huyu ambaye wazazi wake waliaga dunia kutokana na janga la ukimwi akahamishiwa kwa halati yake anashurutika kutoroka na kujiunga na mkururo wa watoto wa mitaani ili kuuepuka ukatili wa binamu zake. Sorre & Oino (2013) wanaeleza kuwa ukiukwaji wa haki za msingi na dhuluma dhidi ya watoto katika familia wanamoishi ni mojawapo ya sababu zinazowafanya watoto hao

kukimbilia mitaani. Mwandishi wa riwaya ya *Lulu ya Maisha* ameangazia suala la ukatili unaotekelezwa na watoto dhidi ya wenzao kwa uyakinifu na uaminifu.

Kunao ukatili wa kimatendo unaojitokeza kupitia vitendo vya wizi na unyang'anyi. Katika riwaya ya *Siku Njema,* Bakari, mwanawe Salim Makame, ananyakua kipochi cha mwanamke mmoja mtalii (uk. 60). Kitendo hicho kinaukasirisha umati wa watu ambao unampiga kitutu na kumwumiza. Maelezo mengine yanayotolewa na mhusika anayeitwa Rashid yanamsawiri Bakari kama mhusika sugu wa wizi. Hivi ndivyo Rashid anavyosema:

> "Basi Bakari ni mwanawe....Ni jizi hodari kweli. Mara unasikia kaiba hiki mara kile. Yuateza na uhai wake huyo. Mara ngapi ameponea tundu la sindano."(uk. 64).

Katika riwaya hiyo ya *Siku Njema*, Selemani Mapunda na Bakari wanashirikiana katika kutekeleza vitendo vingi vya unyang'anyi na wizi wa kimabavu katika mji wa Mombasa na viunga vyake. Maelezo yanayotolewa kwenye gazeti la *Taifa Leo* punde tu polisi wanapowapiga risasi na kuwaua yanadhihirisha matendo hayo:

> "Polisi waliwapiga risasi na kuwaua majambazi waliokuwa wakijaribu kuiba gari mjini Mombasa... Majina ya majambazi hao waliopigwa risasi mpaka kufa yalitolewa kama Bakari Salim na Selemani Mapunda. Selemani ni raia wa Tanzania. Wote wawili wanasemekana ni sugu wa jela ambao wamehusika katika visa vingi vya uhalifu" (uk. 130-131).

Katika riwaya ya *Tumaini*, Majuto Kijungwe na kijana mwingine (hajatajwa jina) wanamwingilia mkewe mfanyabiashara anayeitwa Karim na kumkaba koo kisha wanamwibia kisanduku chenye vito (uk. 109) .

Licha ya hayo, katika riwaya ya *Lulu ya Maisha*, Omido, mwana wa Tiito, anawaibia watu mali yao (uk. 47). Majirani wa mtaa wa mabanda wa Kisera wanamwelekezea kidole cha lawama kwa kuleta magenge ya wezi yanayowaibia. Aidha, polisi wanaanzisha msako dhidi ya Omido na genge linalojiita RIZIKI kutokana na kisa cha wizi katika duka la Bwana Sultani (uk 48). Maelezo mengine yanayoonyesha matendo ya wizi wa unaotekelezwa na Omido yanatolewa na Sue:

> "Omido aliathiriwa na hirimu zake kuamini si vibaya kula cha haramu kisicho chako cha halali. Aligeuka hayawani, pakashume wa kudukiza na kuingia nyumba za watu kuwachukulia chao cha jasho lao."(uk. 60).

Matendo ya wizi na unyanganyi yanavyodhihirika kupitia wahusika Mapunda, Bakari na Omido ambao wana umri wa takriban miaka kumi na minne jinsi yanavyodhihirika katika vitabu vitatu teule vya fasihi ya watoto ni ukatili. Coyne, Archer & Eslea (2006) wanayafasili matendo kama vile kumnyang'anya au kumwibia mtu mali, uharibifu na kadhalika kuwa ukatili. Naye Felson (2009) anaeleza kuwa wizi na unyanganyi ni ukatili kwa sababu wanyang'anyi na wezi huwatisha na wakati mwingine kuwajeruhi kimwili wahanga wao kama njia ya kupata wanachohitaji kwao. Jambo hili linabainika kiuyakinifu na kiuaminifu wakati Majuto, Kijungwe na wenzake wanapomkaba koo mke wa Karim ili kumwibia kisanduku chenye vito (Momanyi, 2006:109) Waandishi wameyaakisi matendo ya ukatili wa wahusika hawa kwa uyakinifu na uaminifu.

### 2.1.5.1 Uharibifu wa mali

Kitendo kingine kinachodhihirisha ukatili ni uharibifu wa mali ya mtu, kampuni, shirika na kadhalika. Katika riwaya ya *Tumaini*, Majuto na Kijungwe wanavunja ofisi ya mwalimu mkuu, Bwana Mwadime, na kuiba madaftari wanayomwuzia Karim, mmiliki wa duka la jumla (uk. 20). Katika kisa hiki, Bwana Karim anachochea ukatili wa Majuto na Kijungwe kwa kununua bidhaa za wizi. Hoja hii itaangaziwa kwa kina katika mada inayohusu sababu zinachochangia matendo ya ukatili miongoni mwa watoto. Kitendo hiki cha wizi kinaufanya usimamizi wa shule kuwalazimisha wazazi wa vijana hao kugharimia mali iliyoibwa. Katika tukio jingine, Majuto na wenzake wanavunja ofisi ya D.O ili kuiba pesa (uk. 142). Wizi huu unatibuliwa na polisi ambao wanawafyatulia Majuto na Kijungwe risasi za miguuni na kuwatia mbaroni. Matukio haya mawili yanahusisha matendo mawili ambayo yanatendeka sambamba. Matendo haya ni uharibifu wa mali kupitia uvunjaji wa ofisi ya mwalimu mkuu na ile ya D.O pamoja na wizi. Kwa mujibu wa Coyne, Archer & Eslea ( 2006) kumwibia mtu au kuharibu mali ni matendo ya ukatili. Naye, Bourguignon (2000) anafafanua kuwa wizi, unyang'anyi na au uharibifu wa mali hudidimiza uchumi, kusababisha umaskini na kutokuwepo kwa usawa hivyo basi kutoa mwanya kwa mzunguko wa visa vya ukatili miongoni mwa watoto.

### 2.1.5.2 Unyanyasaji wa kimapenzi

Unyanyasaji wa kimapenzi pia ni kitendo kingine cha ukatili wa kimatendo. Katika riwaya ya *Siku Njema*, Selemani Mapunda alipotoroka shule anaelezewa

kuwa alishiriki matendo mengi ya ukatili yakiwamo ubakaji wa mabinti wa watu (uk. 20). Maelezo sawa na hayo yanatolewa kuhusu mhusika Majuto wa riwaya ya *Tumaini* ambaye anaelezewa kuwa alipowaasi walimu aligeuka lofa wa kuzunguka mitaani ambapo alitekeleza matendo mbalimbali ya ukatili yakiwamo kuwabaka mabinti wa watu (uk. 53). Tukio moja ambalo linaonyesha bayana kitendo cha ubakaji cha Majuto ni wakati anapojaribu kumbaka Tumaini:

> "Majuto alikuwa akihema kama anayekimbia. Kwa ghafla alimshika Tumaini kiuno na kujaribu kumbwaga chini. Tumaini alijua sasa yumo hatarini. Alimpiga Majuto kwa kiko cha mkono katika sehemu ya kinena kwa nguvu zake zote. Majuto alipiga kelele kwa maumivu huku akifyonya na kumwachilia (uk. 89).

Kavuria (2008) anahoji kwamba unyanyasaji wa kimapenzi hutokea mtu anapomshurutisha mwenzake kushiriki naye mapenzi au kumgusagusa kwa lengo hilo na kwamba hutokea sambamba na aina nyingine za ukatili. Naye Felson (2009) anaeleza kuwa wabakaji huwalazimisha wahanga wao kujisalimisha; hiyo ikiwa njia ya pekee ya kupata wanachohitaji. Matendo ya wahusika hawa yameakisiwa kwa uyakinifu na uaminifu na waandishi wa riwaya mbili teule.

Sehemu hii imeangazia ukatili wa kimatendo unaojidhihirisha kupitia matendo ya kusababisha majeraha ya kimwili, kutishia kusababisha majeraha hayo, wizi na unyang'anyi, ubakaji pamoja na udhalilishaji. Ukatili huu umeakisiwa kwa uyakinifu na uaminifu na waandishi wa vitabu teule vya fasihi ya watoto kwa sababu matukio ya watoto ambao hutekeleza ukatili huu dhidi ya wahusika wengine huangaziwa katika vyombo mbalimbali vya habari nchini na kimataifa.

### 2.1.6 Ukatili wa kimatamshi

Ukatili wa kimatamshi hujitokeza kwa njia ya matusi, kejeli, dhihaka, vitisho miongoni mwa nyingine (Leach, 2014). Leach anafafanua kwamba wanaotekeleza ukatili huu hudhamiria kusababisha maumivu ya kisaikolojia kwa wenzao.

Reyes (2007) anaeleza kwamba si rahisi kufasili dhana ‘maumivu ya kisaikolojia’ kwa sababu matendo ambayo hukusudiwa kuumiza mwili pia yanaweza kuumiza hisia. Mtaalamu huyu anafasili dhana maumivu ya kisaikolojia kuwa ni maumivu makali ya akili au mateso ambayo husababishwa na vitisho au matendo yanayodhamiriwa kuathiri utendakazi wa hisia au silika (personality). Reyes anaendelea kueleza kuwa maumivu ya kisaikolojia yanaweza pia kusababishwa kwa njia zisizosababisha majeraha ya kimwili au hata kugusa mwili lakini zinazogusa akili au hisia za mwathiriwa. Katika riwaya ya *Siku Njema*, Selamani Mapunda anaonesha ukatili kupitia maneno anayoyatumia kumrejelea hedimasta wao. Hivi ndivyo anavyosema:

> “Hili bwege leo litajua kilichomfanya sangara kuchomwa moto. Ati alitaka nioge mbele ya hadhara ile. Wallahi! Tutaliua hili. Na liwe liwalo.”(uk. 21).

Maneno ya Mapunda yanajumuisha vitisho na matusi yanayokusudiwa kumfanya mwalimu mkuu kuhisi duni na kukijutia kitendo chake cha awali cha kumwamrisha Mapunda aoge mbele ya wanafunzi. Licha ya hayo, Mapunda anamwambia Kongowea Mswahili kwamba angemwua iwapo angeripoti kitendo cha kudhulumiwa kwa mwalimu mkuu kwa polisi.

Hivi ndivyo anavyosema:

> "Wewe sikia bwana...yote uliyoyasikia na kuona hapa usimwambie mtu yeyote. Ushasikia? Ukimwambia mtu basi hakika utakufa."(uk. 21)

Matamshi ya Mapunda katika usemi ulionukuliwa hapa juu yanadhihirisha vitisho. Vitisho vingine vinajitokeza katika riwaya ya *Tumaini* kupitia mhusika Majuto. Baada ya jaribio la kumbaka Tumaini kutibuka, Majuto anamtishia kwa maneno yafuatayo:

> "Nitakuonyesha mimi ni nani siku moja." (uk. 89)

Kauli hii inaonyesha kwamba Majuto alikuwa na nia ya kuuendeleza ukatili wake dhidi ya mwathiriwa katika siku za baadaye. Katika riwaya hiyo, Waridi anaonyesha ukatili kwa Masika anapotishia kwa maneno yafuatayo:

> "Bado hayajaisha – nitakushika siku nyingine – utanijua mie n'nani.''(uk. 112).

Maneno haya ambayo Waridi anayatamka baada ya vita baina yake na Masika kuamuliwa na wanawake waliofika kisimani, yanadhihirisha nia ya Waridi kumpiga tena Masika katika siku za baadaye. Matamshi mengine yenye vitisho yanajitokeza katika riwaya ya *Lulu ya Maisha* kupitia mhusika Maanzo ambaye anamtishia Sue kwa sababu Sue anakataa ombi lake la kumtaka wawe wapenzi.

> "Utaniona" (uk. 51)

Matendo ya wahusika waliojadiliwa hapa yanaonyesha ukatili wa kimatamshi nayo yameakisiwa kwa uyakinifu na uaminifu. Osterman, Bjorkqvist& Lagerspetz (1998) wanaeleza kuwa ukatili wa kimatamshi huhusisha, vitisho, kiapo na

matusi, usawiri hasi ambao hudhamiriwa kumfanya mwathiriwa kujiona duni na kadhalika.

Vitisho anavyovitoa mwathiriwa ili kujitetea dhidi ya ukatili unaoelekezwa kwake pia huchukuliwa kuwa ukatili (Chamandar & Jabbari , 2017). Vitisho hivi wakati mwingine huambatanishwa na ishara na miondoko fulani ya mwili kama vile kuchukua silaha ili kujihami au kujitetea. Jambo hili linajitokeza kiuhalisia katika riwaya ya *Tumaini* ambapo Tumaini anatwalia kisu cha mboga na kumtishia Majuto kwa maneno yafuatayo:

> “Nikaribie uone ikiwa wewe kweli ni mwanamume. Unadhani kuwa mimi ni kama wale unaowavizia mitaroni!’’(uk. 89).

Ingawa vitisho vya Tumaini vinakusudiwa kumzuia Majuto kuendeleza dhuluma zake, bado vinafasiliwa kuwa ukatili kwa mujibu wa Chamandar & Jabbari (2017).

Katika riwaya hiyo, Idi, mwana wa Mzee Masumbuko, anasawiriwa kama mtoto katili kutokana na matamshi yake ya kuwadunisha dada zake na jinsia ya kike kwa jumla. Idi anamwona Tumaini kama bidhaa ambayo punde si punde ingeuzwa ili baba yake apate pesa za matumizi. Anamwambia Tumaini waziwazi kwamba hata akikataa kupashwa tohara hatimaye angeolewa tu (uk. 29). Anapomwambia Tumaini kwamba angeolewa tu, Idi aliamini kuwa hilo ndilo lililokuwa jukumu muhimu la kila mtoto wa kike. Maneno mengine yanayoonyesha ukatili wa Idi ni wakati anapomwambia dada yake kwamba kazi

ya kuchochea moto mekoni na kuteka maji ni ya wanawake hivyo basi hakuwa radhi kumsaidia kutekeleza kazi za aina hiyo (uk. 29). Tumaini mwenyewe anaonyesha hofu yake kuhusu athari ya baadaye ya kauli za Idi ambazo anaeleza zilisheheni ukatili na ujeuri (uk. 71). Maneno ya Idi ambayo yanaidhalilisha jinsia ya kike kwa jumla yanatokana na taasubi za kiume zilizotawala mazingira anamokulia Idi (Mwenda, 2020).

Mhusika Kijungwe katika riwaya hiyo ni mwanafunzi mwingine aliyejawa na ujeuri na ukatili. Anadhihirisha tabia hiyo anapomdhihaki Tumaini kwa maneno yafuatayo:

> “Tuma hivi uliikimbia tohara kwa sababu ya woga au mchumba uliyechaguliwa hukumpenda... nilidhani wewe ni msichana jasiri sana wala hungeogopa kisu. Au ni wembe?”(uk. 72).

Fasili ya Osterman, Bjorkqvist & Lagerspetz (1998) inatusaidia kuuelewa ukatili wa Kijungwe unaojidhihirisha kwa njia ya dhihaka.

Aidha, katika riwaya hiyo baadhi ya wanafunzi wa kike wa shule ya Kivulini ambao hawafaulu katika masomo fulani au katika takriban masomo yote wanaonyesha ukatili wao kwa walimu wa masomo hayo kupitia kauli zao zilizojaa chuki. Almasi ni mmoja wa wanafunzi hao ambao wanamchukia mwalimu wa somo la Hisabati bila sababu. Kauli ifuatayo inaonyesha matamshi yake ya ukatili:

> “Wacha hilo somo lenyewe, hata mwalimu anayefunza, mimi namchukia pia....Namchukia tu basi.” (uk. 73).

Matamshi ya wanafunzi kama vile Almasi huenda yasiwe na athari ya moja kwa moja kwa mwalimu wao lakini yanaweza kuwaathiri wanafunzi wengine kwa njia hasi kwa kuwafanya kutolipenda somo lenyewe. Kulingana na Chamandar & Jabbari (2017) ishara za mwili kama vile kuonyesha uso wa hamaki au kutamka maneno ya hasira kuhusu mtu fulani ni ukatili. Katika riwaya ya *Lulu ya Maisha*, Omido anadhihirisha ukatili anapomwambia dada yake, Sue, kwamba angefanya alivyotaka kwani sasa hakuwa na baba wala mama wa kumwangalia (uk. 47). Anayatamka maneno hayo kwa hasira ili kumkomesha Sue kumchunguzachunguza. Maneno ya Omido pia ni ukatili kwa mujibu wa Chamandar & Jabbari (wametajwa).

Katika riwaya ya *Lulu ya Maisha*, mwandishi anasimulia kuhusu maisha ya kuzozana ya vijana wawili; Fazul na Fatila ambao walioana wakiwa watoto. Kila wakati Fatila aliwasha zogo kwa kumzomea mumewe kutokana na mambo madogo madogo ambayo yasingeibua ugomvi. Kwa mfano, kila wakati Fazul alipowasili nyumbani mikono ikiwa imejaa, Fatila alifurahi. Hata hivyo, aliporudi mikono mitupu alimtupia cheche za matusi ya kila aina akimfedhehesha kwa jirani wanaosikiliza (uk 63 ). Huu nao ni ukatili wa kimatamshi unaojibainisha kwa njia ya matusi jinsi ulivyofasiliwa na Osterman, Bjorkqvist & Lagerspetz (1998).

Matamshi ya wanafunzi ya kuwadhalilisha wenzao katika mazingira ya shule pia yanajumuisha ukatili wa kimatamshi. Visa kadha wa kadha vya ukatili huu

vimesimuliwa katika vitabu teule vya fasihi ya watoto. Kwa mfano, katika *Siku Njema*, baadhi ya wanafunzi wa darasa la Kongowea Mswahili wanamdhihaki na kumuumbua kwa sababu ya kimo chake. Kila wakati alipowashinda masomoni walimdhalilisha kwa kauli:

> "Hiki kitoto kichekechea kinatushindaje masomoni, kwani kina akili nyingi vipi?"(uk. 8).

Maneno mengine ya udhalilishaji wanayoyatumia wanafunzi hao kwa Kongowea Mswahili ni kumwita, "kikojozi" na "mwanaharamu''. Ukatili huu ambao unatokea katika mazingira ya shule unamfanya Kongowea kuathirika kisaikolojia anavyoeleza kwa maneno yafuatayo:

> ''...Hili la kuitwa ''mwanaharamu'' lilinikeketa maini kama msumeno na kunikosesha furaha daima...''( uk. 8).

Katika riwaya ya *Lulu ya Maisha*, Sue anakuwa mwathiriwa wa vitendo vya ukatili vya wanafunzi wa shule ya *St. Mary's Girls Primary Boarding* . Wanafunzi hao wanamwamrisha kuimba kidogo, kulia na kuwasifu wale ambao walikuwa viranja wao kwa kuwarejelea kwa jina '*your honour'* au'mheshimiwa'(uk. 70). Ukatili wa njia ya udhalilishaji wa wanafunzi dhidi ya wenzao nao umeakisiwa kwa uyakinifu na uaminifu na waandishi wa vitabu husika vya fasihi ya watoto kwani ni suala ambalo limetafitiwa na athari zake kuelezewa wazi (Osterman, Bjorkqvist, Lagerspetz, 1998; Itegi, 2017). Itegi (keshatajwa) anaeleza kuwa wanafunzi huwadhalilisha wenzao kwa kuwatusi na kutishia kusababisha majeraha miongoni mwa njia nyingine.

Sehemu hii imeangazia ukatili wa kimatamshi. Ukatili huu hudhihirika kwa njia ya matusi, kejeli, dhihaka na vitisho miongoni mwa njia nyingine ambazo huwaathiri wahusika kisaikolojia.

### 2.1.7 Ukatili wa kuwaziwa

Leach (2014) anafafanua kuwa ukatili wa kuwaziwa ni hali ya kufikiria, kupanga njama au kitendo cha ukatili bila kukitekeleza kitendo chenyewe. Ukatili huo pia unaelezewa kuwa ni mawazo au fikra za kifantasia za kumjeruhi mtu mwingine (Murray, Eisner & Ribeaud, 2018). Katika vitabu teule, ishara mbalimbali zinaonyesha kuwa wahusika fulani wanawazia kutekeleza ukatili dhidi ya wenzao. Ishara hizi zinajidhihirisha kwa njia ya matamshi, maandishi, kumiliki silaha hatari na kuwaandamaandama wahanga kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa nia ya kuwadhuru miongoni mwa nyingine. Katika riwaya ya *Siku Njema*, Mapunda anatishia maisha ya Kongowea Mswahili kupitia barua anayomwandikia katika mji wa Tanga punde tu anapotoka jela:

> *Kwa kongoweya Muswahili,*
> *Uliniponza nikafungwa jera. Sasa nimetoka jera.Utakiona cha mutema kuni. Taree 31 julai 1971 muaka uu nitakuua.*
> *Selemani."(uk.33)*

Baadaye, Mapunda anatiwa mbaroni na polisi akiwa na bastola anayopanga kuitumia kutekeleza vitisho alivyowasilisha kwenye barua. *(*uk. 92). Fauka ya hayo, Mapunda anapotoroka jela, anatorokea mji wa Mombasa kwa nia ya kumsaka na kumwangamiza Kongowea inavyodhihirika kupitia ujumbe anaoandika kwenye choo cha wapangaji katika mji huo yanayosomeka:

> "Kongoweya wewe ndiye uliniharipiya bahati yangu, ulipokimbilia Mwambasa ulifikili sitokupata. Nitakuua. Niko apa mjini. S.M."(Walibora: 100).

Katika *Lulu ya Maisha,* Sue anadhihirisha ukatili anapowazia kuchukua shoka ili akawakabili ami zake ambao wanawanyang'anya urithi walioachiwa na marehemu baba yao (uk. 21) . Hata hivyo, hakitekelezi kitendo chenyewe kutokana na maonyo ya mama yake ambaye anamuusia kwamba ilikuwa vibaya hata kuwatukana ami zake.

Ukatili wa kuwaziwa umeakisiwa kwa usahihi na waandishi wa riwaya tatu za fasihi ya watoto kwa kuwa matendo ya aina hiyo yamewahi kuangaziwa nchini Kenya. Kwa mfano, vimeripotiwa visa vya wanafunzi waliopanga kuharibu mali ya shule au waliopatikana na silaha au vifaa hatari walivyokusudia kuvitumia kutekeleza uhalifu. Kwa mfano, mwanafunzi wa Shule ya upili ya Kamama katika kaunti ya Meru alipatikana na risasi ambayo inaweza kutumiwa kwenye bunduki ya AK47. Tukio hili lilijiri baada ya usimamizi wa shule kufanya msako wa ghafla kutokana na jaribio jingine la awali la baadhi ya wanafunzi kuchoma shule ( Mugo, 2021)

### 2.1.6 Hitimisho

Mhimili wa nadharia ya uhalisia unaohusu usawiri wa matukio kwa uyakinifu na uaminifu na waandishi wa fasihi ya watoto ni faafu katika kuzielewa aina za ukatili katika riwaya teule za fasihi ya watoto. Waandishi wa kazi hizo wameyaangazia matendo ya ukatili wa watoto kwa uhalisia hivyo basi kubainisha

kuwa ni matendo ambayo yamo katika jamii na ambayo hujitokeza aghalabu katika vyombo vya mawasiliano. Aidha, ni wazi kwamba matendo haya yametokea katika mazingira walimokulia waandishi hao nayo yakawaathiri kwa njia moja au nyingine. Kuna haja ya kuyaangazia matendo hayo kwa sababu yatapitisha mafunzo chanya kwa watoto kuhusu madhara yanayotokana na matendo ya ukatili hivyo basi kujaribu kuyaepuka matendo hayo.

# SURA YA TATU

# SABABU ZINAZOCHANGIA UKATILI MIONGONI MWA WATOTO KATIKA VITABU TEULE VYA FASIHI YA WATOTO NA ATHARI ZAKE KWA WAHUSIKA WENGINE

## 3.0 Utangulizi

Sura iliyotangulia iliangazia aina za ukatili zinazojitokeza katika vitabu vilivyoteuliwa vya fasihi ya watoto. Aina tatu za ukatili zilijitokeza ambazo ni ukatili wa kimatendo, wa kimatamshi na wa kimawazo. Sura hii imejadili sababu zinazochangia tabia ya ukatili miongoni mwa watoto na athari zake kwa wahusika wengine katika kazi hizo za fasihi ya watoto. Mhimili mmoja wa nadharia ya ujifunzaji wa kijamii ya Bandura (1977) unaeleza kuwa tabia ya mwanafunzi haikuzwi tu na upokezi wa ujumbe bali ni mchango baina ya mambo tofauti muhimu, yaani mazingira. Mhimili huu ulisaidia utafiti huu kuonyesha jinsi sababu mbalimbali huchangiana katika kukuza tabia ya ukatili miongoni mwa watoto. Mhimili wa nadharia ya uhalisia unaeleza kwamba waandishi wa kazi za fasihi huyaangazia matukio, wahusika, mazingira na mandhari kwa uyakinifu na uaminifu. Mhimili huu ulitumikizwa katika kazi hii ili kuelewa jinsi athari za watoto katili kwa wahusika wengine zilivyoangaziwa kwa uhalisia na waandishi wa vitabu husika.

### 3.1. Sababu zinazochangia tabia ya ukatili katika vitabu teule vya fasihi ya watoto

Mayne (2011) anaeleza kuwa matukio mengi hayaelezeki kikamilifu kwa kutoa sababu moja pekee. Mtaalamu huyu anafafanua kuwa masuala mengi ni changamano na kwa hiyo kujaribu kuyanasibisha na sababu za moja kwa moja mara nyingi huzua utata kimantiki.

Ukatili miongoni mwa watoto una sababu nyingi (Kauffman, 1994; Watson, Fischer, Andreas & Smith, 2004 & Imtiaz, Yasim & Yaseen 2010). Kauffman (1994) anafafanua kwamba watafiti wamevumbua sababu nyingi za tabia ya ukatili ila wameibuka na suluhu chache. Watson, Fischer, Andreas & Smith (2004) nao wanaeleza kuwa ingawa sababu nyingi huchangia tabia ya ukatili watafiti hujaribu kuchunguza zile zenye mchango mkubwa katika kusababisha tabia yenyewe.

Utafiti huu utachanganua sababu zenye mchango muhimu katika tabia ya ukatili miongoni mwa watoto katika vitabu teule vya fasihi ya watoto chini ya mada tatu: sababu za kifamilia, sababu za kijamii na sababu zinazohusiana na shule (Mabitla, 2006).

#### 3.1.1 Sababu za kifamilia

Kihistoria, familia imekuwa na mchango muhimu katika kuwakuza watoto (Kitzmann, Gaylord, Holt & Kenny, 2003) .Wataalamu hawa wanaeleza kuwa ukatili miongoni mwa watoto aghalabu huhusishwa na sababu za kifamilia hasa

za kimalezi. Katika riwaya ya *Siku Njema*, Walibora (1996) amedhihirisha kuwa mojawapo ya sababu zinazoathiri tabia ya Bakari Salim na kumfanya kuwa jambazi sugu ni kudekezwa na mama yake. Bakari anaharibiwa na mapenzi ya kupindukia ya Wamboi ambaye alimpa chochote alichokitaka alipokuwa mdogo. Kutendekezwa huko kulitokana na sababu kuwa alikuwa mtoto wao wa pekee (uk. 65-66). Tabia ya ukatili ya Bakari inapokithiri anafungwa jela mara kwa mara kutokana na matendo ya wizi wa kimabavu.

Katika riwaya ya *Tumaini*, Momanyi (2006) anasimulia jinsi Majuto, mwana wa Bwana Andrea, anavyogeuka katili kwa sababu ya kudekezwa na baba yake. Kila wakati Majuto alipofukuzwa shuleni kutokana na utovu wa nidhamu, Bwana Andrea alimtetea na kutumia ushawishi na cheo chake cha uchifu kuhakikisha kuwa amerejeshwa shuleni (uk.20). Aidha, wakati wowote Chifu Andrea alipojuzwa kuhusu wizi wa Majuto alijitia hamnazo. Walalamishi wa matendo ya wizi walipotishia kuchukua hatua za kisheria, aliwahonga ili Majuto asitiwe mbaroni (uk. 71). Isitoshe, wazazi wa mabinti ambao walinyanyaswa kimapenzi na Majuto walipopeleka mashtaka kwa Bwana Andrea, aliwapuuza. Walipowasilisha mashtaka mahakamani, Andrea aliwahonga mawakili na hata mahakimu kutupilia mbali kesi (uk 53-54). Tabia ya ukatili ya Majuto inavuka mipaka kiasi cha kufukuzwa shuleni kwa kuasi kanuni. Anaanza kurandaranda mitaani huku akiwadhulumu mabinti wa watu kimapenzi na kuiba mali. Katika riwaya hiyo, Idi, mwana wa Masumbuko, anakuwa katili kwa sababu ya kudekezwa na baba yake. Ukatili wa kijana huyu unadhihirika kupitia matusi yake

dhidi ya dada zake (uk. 14). Kila wakati Tumaini, dada yake Idi, alipomlalamikia baba yao kuhusu matusi ya Idi, Mzee Masumbuko alimkanya Tumaini asiyaingilie malezi ya Idi kwa sababu yeye (Idi) alikuwa mtoto wa kiume wala si wa kike. Matamshi ya Masumbuko yanahalalisha ukatili wa Idi na kumfanya atendese. Mwendwa (2020) anaeleza kuwa wazazi huwatendekeza wana wao kwa sababu mbali mbali mojawapo ikiwa kutaka kuhepa mambo yoyote ambayo yanaweza kuleta kutoelewana kati yao na wana hao. Baadhi ya wazazi hao huwapa watoto wao vitu ambavyo hawavihitaji kwa wakati huo na kuwaruhusu kufanya mambo yoyote yanayowafurahisha bila kuwepo kwa sheria za kuwaongoza. Matokeo ya utendekezaji huo ni kukithiri kwa tabia ya ukatili.

Kukosekana kwa watu wanaoweza kukidhi mahitaji mbalimbali ya mtoto yakiwemo yale ya kisaikolojia katika familia ni sababu nyingine inayoashiriwa na waandishi wa vitabu teule vya fasihi ya watoto kwamba imechangia kutokea kwa tabia ya ukatili miongoni mwa watoto. Watu hawa wanajumuisha wazazi, walezi na jamaa wengine wenye uhusiano wa karibu na mtoto (Reese, Vera, Simon & Ikeda, 2000). Wazazi wana wajibu muhimu wa kuwashawishi na kuwaongoza watoto kuiga tabia inayokubalika na jamii (Vanassche, Sodermans, Matthijs & Swicegood 2014). Morell (2006) anatambua umuhimu wa baba mzazi katika kukidhi mahitaji mbalimbali ya mtoto yakiwamo yale ya kimsingi na kisaikolojia. Pia, mtaalamu huyu anafafanua kwamba baba huwa kielelezo cha wa kuigwa na mtoto. Bugental, Corpuz & Schwartz, (2012) wanasisitiza kuhusu umuhimu wa mama katika kumsaidia mtoto kuyakubali mazingira yanayomzunguka.

Wataalamu hawa wanaendelea kufafanua kwamba kutojihusisha kikamilifu kwa mama katika malezi wakati mwingine humfanya mtoto kukumbwa na msongo wa mawazo, kukosa kujithamini na kuyaitikia mazingira yake kwa ukatili. Katika riwaya ya *Siku Njema,* mwandishi anaeleza kuwa Bakari anageuka kuwa katili kwa sababu ya kutowajibika kwa wazazi wake katika malezi yake. Salim Makame hakujihusisha katika malezi ya Bakari bali aliuacha wajibu huo mikononi mwa mkewe, Wamboi. Jambo hilo linajitokeza kupitia usemi wa Rashid ufuatao:

> "Mzee Salim alionekana nyumbani kwa nadra sana. Alikuwa anapenda raha kweli. Ungempata vilabuni anasharabu vileo. Alijiita Mpendaraha tangu hapo hata jina hilo likawa lake haswa lililosibu." (uk. 65).

Mzee Salim hakuwa na wasaa wa kukaa na Bakari ili kumwadilisha kwa sababu alikuwa ameingilia sana ulevi. Wamboi, mkewe Salim naye alimuengaenga Bakari kwa kumpa chochote alichokitaka katika umri wake mdogo. Jambo hilo lilimwathiri kitabia jinsi lilivyoelezewa katika hoja inayohusu udekezaji. Aidha, Bakari anaporudi nyumbani kutoka jela alipokuwa amefungwa kwa hatia ya wizi, hamkuti baba wala mama yake nyumbani. Baba yake alikuwa ametoweka asijulikane alikokwenda ilhali mama yake alikuwa amegeuka majununi aliyeokota vitu katika mji wa Mombasa. Kukosekana kwa wazazi wa Bakari nyumbani kunamnyima kijana huyo msaada aliouhitaji ili kuendelea kuirekebisha tabia yake. Anafanya uamuzi wa kuenda kukaa na hirimu zake (uk. 65). Ushawishi wa vijana wa hirimu yake wakiwamo akina Selemani Mapunda unaifanya tabia ya ukatili ya Bakari kukithiri.

Katika riwaya ya *Tumaini,* Bwana Andrea hana muda wa kutosha wa kuketi na Majuto ili kumwelekeza na kumwadilisha. Jambo hili linatokana na safari zake za kutwa za kujilimbikizia mali kwa njia ya ufisadi (uk. 54). Vile vile, wazazi wa Majuto hawashirikiani na walimu kuchunguza kiini cha tabia ya Majuto ili kumrekebisha wakati ambapo tabia yake ya ukatili inaanza kujidhihirisha. Tabia ya Majuto inaendelea kukithiri shuleni na kufikia kiwango ambapo walimu hawawezi kuidhibiti. Majuto anapoandikiwa barua ya kumtimua shuleni, wazazi hawajishughulishi naye tena. Jambo hilo linamfanya kijana mwenyewe kuwa sugu wa vitendo vya uhalifu mitaani (uk. 21). Baldry & Farrington (2005) wanaeleza kuwa wazazi ambao hawathamini elimu ya watoto na maendeleo yao shuleni wanaweza kuchangia kutokea kwa tabia ya ukatili miongoni mwa watoto hao. Sababu ni kwamba wazazi hao hukosa fursa ya kufahamu wakati wa kutokea kwa tabia ya ukatili ya watoto wao na kushirikiana na usimamizi wa shule kuishughulikia mapema iwezekanavyo. Aidha, wazazi wenyewe hawana fursa ya kuwatia motisha watoto wao kuelekeza juhudi zao masomoni badala ya kushiriki katika tabia ya ukatili.

Katika riwaya ya *Lulu ya Maisha*, mwandishi Habwe (2016) anadhihirisha jinsi kuaga dunia kwa Tiito, baba yake Sue na Omido, kunavyochangia tabia ya ukatili ya Omido (uk. 60). Mwandishi anaeleza kuwa Omido anageuka jambazi sugu linaloingia katika nyumba za watu na kuwaibia kwa kutumia nguvu. Kifo cha Tiito kinakuwa sababu ya familia yake kushindwa kumudu maisha ghali ya mtaa wa kifahari wa Onyoka hivyo basi kumshurutisha mke wake kuwahamishia

watoto katika mtaa wa mabanda wa Kisera. Maisha magumu katika mtaa wa mabanda yanamfanya Omido kushawishiwa kwa haraka na genge la vijana wa rika lake ambalo lilitafuta riziki kwa kuwaibia watu kwa nguvu. Richter (2006) anaeleza kuwa wajibu wa baba katika familia ni kukidhi mahitaji ya msingi na yale ya kisaikolojia miongoni mwa mengine. Mtaalamu huyu anaendelea kufafanua kuwa watoto wanaoishi na baba huwa na ulinzi thabiti dhidi ya vishawishi mbalimbali. Hali kadhalika, wazazi huwa na mchango muhimu katika kumsaidia mtoto kujifunza maadili yanayokubalika katika jamii.

Mienendo na mitindo ya maisha ya baadhi ya wazazi inaashiriwa na waandishi wa vitabu teule vya fasihi ya watoto kuwa sababu nyingine inayochangia tabia ya ukatili miongoni mwa watoto. Mambo hayo yanawafanya wazazi wenyewe wasiwe mfano mwema wa kuigwa na watoto. Perry, Perry, & Boldizar (1991) wanaeleza kuwa watu fulani ambao ni vielelezo na ambao watoto huiga tabia zao, wanaweza kuwa chanzo cha tabia ya ukatili ya watoto hao. Katika riwaya ya *Tumaini,* Andrea anasawiriwa kama mhusika ambaye ni mwingi wa dhuluma za kimapenzi. Tabia yake ya kuwanyanyasa kimapenzi wasichana wadogo inadhihirika bayana kupitia mzozo baina ya Bi. Halima na mkewe Andrea. Bi. Halima anamwambia mkewe Andrea maneno yafuatayo:

> “Ni wasichana wangapi mumeo amewaharibu mitaani, wengine hata akiwasaidia kuavya?... Vigoli wangapi wameajiriwa kazi hapa kisha wakatoka na mayowe, mikono vichwani? Sababu yake ni’nini? Mumeo kesha watunga mimba na wakikujuvya unawatimua kwa vishindo!”(uk. 95).

Majuto, mwanawe Andrea, amesawiriwa kama mhusika ambaye amejaa dhuluma za kimapenzi. Mwandishi wa riwaya ya *Tumaini* anaeleza kuwa Majuto alikuwa tisho mitaani ambapo aliwaibia watu mali na kuwabaka mabinti wa watu kwa kuwavizia vichochoroni (uk. 71). Licha ya hayo, linasimuliwa tukio ambapo Majuto anajaribu kumbaka Tumaini katika nyumba ya akina Majuto (uk. 90). Majuto ameiga tabia ya unyanyasaji wa kimapenzi kutoka kwa baba yake inavyodhihirika kupitia mawazo ya Tumaini yafuatayo:

> "Mtoto umleavyo, ndivyo akuavyo."(71).

Katika riwaya ya *Siku Njema*, Mzee Salim anasawiriwa kama mtu anayependa sana kusharabu vileo na kushiriki anasa nyingine za vilabuni (uk. 65). Tabia ya Salim imemwathiri mwanawe Bakari ambaye anaelezewa na mwandishi kuwa alikuwa mtumizi wa dawa za kulevya (uk. 64).

Adhabu kali dhidi ya watoto ni sababu nyingine ambayo inaashiriwa na waandishi wa riwaya teule za watoto kwamba ina mchango katika tabia ya ukatili miongoni mwa watoto. Katika riwaya ya *Tumaini*, Mzee Masumbuko anasawiriwa kuwa baba katili anayewalea watoto wake kwa ukatili mwingi (uk. 12). Mwandishi anaeleza kuwa Masumbuko alikuwa akiwafungia watoto wake ndani ya gunia lenye upupu na kuwatandika kwa fimbo mpaka fimbo yenyewe inakatika vipandevipande (uk. 28). Fauka ya hayo, mzee huyo anaelezewa kuwa mwingi wa hamaki ambazo zilivuka mpaka alipolewa. Vile vile, amesawiriwa kama mwanamume ambaye ni mwingi wa matusi anayoyatumia kama mbinu ya

kuwakosoa mabinti wake (uk. 14). Tabia ya Masumbuko inamwathiri Idi ambaye mara kwa mara anawatusi dada zake kwa kuwaita bidhaa zilizohifadhiwa nyumbani zikingoja wakati mwafaka wa kuuzwa (uk. 14). Ukatili wa Masumbuko pia unamfanya Idi kuingiwa na kasumba inayomfanya kufikiri kuwa njia pekee ya kurekebisha tabia ni kutumia adhabu kali. Jambo hili linadhihirika kupitia kauli yake kwa Tumaini:

> "Baba amekasirika Tuma! Alimwambia Mashaka amtayarishie gunia tupu kisha akachukua panga na kuelekea shambani.''(uk. 28).

Tabia nyingine ya Masumbuko inayomwathiri Idi kwa njia hasi ni ile ya kumpasha Idi adhabu kali inayodhamiriwa kumtia usugu. Mzee huyo anadhani kuwa adhabu kama hiyo ni njia mujarabu ya kumwandaa mtoto wa kiume kuyakabili maisha magumu kiume. Jambo hili inadhihirika kupitia kauli ya Masumbuko kuwa Idi alikuwa mtoto wa kiume wala si wa kike na kwamba alihitaji kuwa na moyo wa shujaa kama yeye (uk. 14). Aidha, adhabu kali anayowapitishia watoto wake inadhamiriwa kutekeleza jukumu hilo. Matamshi ya Masumbuko na adhabu yake kali vinamtia Idi 'usugu' na kumfanya kuyaona mambo kwa mtazamo wa ubabedume. Kwa mfano, anamdhihaki Tumaini kwa kumwambia kuwa tohara si jambo ambalo lingemfanya (Tumaini) kuogopa na kutoroka nyumbani (uk. 29). Aidha, Idi anadhihirisha tabia ya ubabedume kwa Tumaini anapomwambia kupitia maneno yafuatayo:

> "…si utaolewa tu."(uk. 29).

Tabia ya Idi ya kuwadunisha dada zake kupitia matamshi haya na mengine, imechochewa na baba yake. Mabitla (2006) anaeleza kuwa baadhi ya wazazi hudhihirisha ukatili kwa watoto wao hasa wa kiume wakati wanapowapitishia adhabu kali kama njia moja ya kuwatia ukakamavu kupambana na maisha magumu ya baadaye. Watoto waliopitia ukatili wa aina hii hujifunza tabia ya kuyakabili mambo kiume na kulipiza kisasi badala ya kutafuta msaada kutoka kwa watu wengine. Nao Watson, Fischer, Andreas & Smith (2004) wanaeleza kuwa watoto ambao wamekuwa wahanga wa ukatili hugeuka kuwa katili wakidhani kuwa hiyo ni njia moja ya kuzuia ukatili wowote wanaoutazamia kujitokeza katika mazingira yao. Mawazo ya wataalamu hawa yanaafikiana na kauli ya Momanyi (2006) ambaye anasimulia kuwa mojawapo ya mambo yanayomfanya Masumbuko kuwa katili ni adhabu kali aliyokuwa akipashwa na baba yake alipokuwa mtoto (uk. 66). Kinasimuliwa kisa kimoja ambapo baba yake Masumbuko alimwadhibu vikali mpaka mwili ukatoja damu na viboko kuvunjikia mwilini. Adhabu yenyewe ilijiri Masumbuko aliposusia kula chakula kwa sababu ya wivu wa kumwona dada yake amevaa viatu vipya alivyozawidiwa na wazungu fulani waliotembea kijijini (uk. 65). Momanyi anahitimisha kisa chake kwa kauli ifuatayo:

> “Adhabu kali ambayo Masumbuko alikuwa akiwapasha watoto wake yamkini ilikuwa ni njia moja ya kulipiza kisasi kutokana na ukatili aliokutishwa na baba yake” (uk. 66).

Dhuluma za kinyumbani zinaashiriwa na waandishi wa vitabu teule vya fasihi ya watoto kuwa sababu nyingine iliyochangia ukatili wa watoto. Katika riwaya ya

*Tumaini* Masumbuko anadhihirisha udhalimu wa kinyumbani kupitia makeke na vishindo vya mara kwa mara anavyomfanyia mkewe mbele ya watoto. Mwandishi anaeleza kwamba mkewe Masumbuko, alikuwa mnyamavu yamkini kutokana na vishindo hivyo. Hali hii inasawiriwa na mwandishi kupitia kauli zifuatazo:

> "Bi. Amina hakutaka kuivunja nyumba yake kwa kumfanyia mumewe vitimbi. Alihiari shingo upande kuvumilia unyanyasaji huo…ilimradi awalee wanawe na kusitiri nyumba yake." (uk. 13).

Dhuluma za kinyumbani zinadhihirika bayana Masumbuko anapomshambulia mkewe kwa sababu ya binti yao kuhepa tohara. Picha hii ya kuogofya inajidhihirisha katika dondoo lifuatalo:

> "Kabla ya mkewe kumjibu, Masumbuko alimrushia ule ufito kwa nguvu zake zote. Ufito ulifyatuka kama mshale, ukayoyomea kwa Bi. Amina ambaye alichutama ghafla na kuupisha. Ufito uliupiga dhoruba kali mpapai uliokuwa umepandwa hapo uani ukakatika vipande viwili.''(uk. 36)

Matamshi ya kikatili ya Idi yamechangiwa pia na makeke na vishindo vya baba yake. Mabitla (2006) anafafanua kuwa wazazi ambao hujaribu kutatua matatizo yao kwa kulaumiana na kufanyiana kelele, kutusiana au kupigana mbele ya watoto huwaathiri kwa njia hasi. Watoto hawa hugeukia ukatili wakidhani kuwa ni njia moja ya kusuluhisha tofauti zao.

Kutokana na maoni ya watafiti wa fasihi ya watoto walioangaziwa pamoja na waandishi wa vitabu teule vya fasihi ya watoto, inabainika kwamba tabia ya ukatili miongoni mwa watoto husababishwa na mambo kadhaa yanayochangiana. Bandura (1977) anaeleza kwamba mambo kadha huchangiana katika kufunza

tabia ya ukatili yakiwamo ufahamu na mazingira. Kwa hivyo, ili kuielewa vyema tabia hiyo ni muhimu kuyaangalia mambo haya kwa pamoja.

### 3.1.2 Sababu za kijamii

Ukatili miongoni mwa watoto huendelezwa kwa njia ya kutazama tabia ya ukatili ya watu wengine ambao ni vielelezo katika jamii, kuinakili tabia hiyo kwenye mawazo na hatimaye kuitumikiza na kuiendeleza (Bandura, 1977). Perry, Perry, & Boldizar (1991) wanaeleza kuwa sababu za kimazingira zinazosababisha ukatili miongoni mwa watoto hujumuisha watu fulani ambao ni vielelezo na ambao watoto huiga tabia zao, mambo fulani yanayoimarisha na kuchochea ukatili pamoja na yale ambayo humkatisha tamaa mtoto.

Katika riwaya ya *Tumaini*, mfanyabiashara anayeitwa Karim ananunua madaftari ambayo Majuto na Kijungwe wanayaiba kutoka shuleni mwao (uk. 20). Kitendo hiki kinakuwa mojawapo ya mambo yanayochochea na kuimarisha tabia ya wizi ya vijana hao. Bwana Karim mwenyewe anakuwa mwathiriwa wa ukatili ambao anaupalilia wakati Majuto na wenzake watatu wanaiba kisanduku cha vito kwenye duka lake (uk. 109). Mwandishi anaeleza kwamba katika harakati za wizi, Majuto na wenzake walimwingilia mkewe. Kitendo cha Karim cha kupokea mali ya wizi kutoka kwa watoto kinachochea na kuimarisha tabia ya watoto hao. Suala hili linaeleweka vyema kupitia maelezo ya Perry, Perry, & Boldozar (1991) wanaoelezea jinsi watu fulani ambao ni vielelezo katika jamii huwa sababu mojawapo ya watoto kuiga tabia ya ukatili.

### 3.1.2.1 Matumizi ya dawa za kulevya

Matumizi ya dawa za kulevya yameelezewa na waandishi wa vitabu teule vya fasihi ya watoto kama sababu nyingine iliyochangia tabia ya ukatili miongoni mwa watoto. Katika riwaya ya *Siku Njema,* Selemani Mapunda anaelezewa kuwa mvutaji hodari wa bangi (uk. 20). Bangi yenyewe inamzuzua na kumfanya kutenda mambo ya kichakaramu yanayowafanya watu kumwita punguani (uk. 103). Baadhi ya mambo hayo ni pamoja na kuwadhulumu kimapenzi mabinti wa watu, kuiba mali na magari na kuwajeruhi baadhi ya watu wakati wa kujilipizia kisasi miongoni mwa mengine. Katika riwaya hiyo, Bakari Salim anasawiriwa kuwa mraibu wa bangi. Maneno ya Rashid yanaidhihirisha tabia hiyo.

> "Nimemuusia siku nyingi aate kuwa sinzia na masikio kayatia pamba. Pengine ni ile bangi anayovuta imchocheayo." (uk. 64)

Matumizi ya dawa za kulevya yanamchochea Bakari kujitosa katika wizi wa kimabavu ili kupata pesa za kununua bangi. Kinasimuliwa kisa ambapo ananyakua kibeti cha mwanamke mmoja mtalii na kujaribu kutoroka nacho. Mwanamke huyo anapiga kamsa na umati wenye hasira unamshika Bakari na kuanza kumpiga kitutu (uk. 60-61). Uvutaji wa bangi unakuwa sababu ya tamaa ya Bakari ya kutaka pesa na tamaa ya pesa inasababisha wizi wa kimabavu. Matendo haya yanathibitisha ukweli wa hoja ya Bandura (1977) kuwa tabia ya ukatili husababishwa na mambo mbalimbali yanayochangiana

Katika riwaya ya *Lulu ya Maisha,* Omido amesawiriwa kama mraibu wa dawa za kulevya kama vile bangi, pombe haramu, sigara na kokeini (uk. 47). Aghalabu,

Omido alivuta bangi na kutumia kokeini waziwazi bila kuwachelea polisi. Matumizi ya dawa za kulevya yanakuwa kichocheo cha kijana huyu kujiingiza katika matendo ya ukatili kama vile kuwavamia watu katika nyumba zao wakati wa usiku na kuwaibia (uk. 60). Kinasimuliwa kisa ambapo Omido akishirikiana na vijana wa rika lake wanamwibia mfanyakazi anayeitwa Sultani. Polisi wanaanza kumsaka kutokana na ukatili huo (uk. 47-48). Aidha, uraibu wa dawa za kulevya unamfanya Omido kudhihirisha ukatili kupitia kauli zake zinazoelekezwa na hasira anazozitamka kwa dada yake kila wakati alipomwuliza kuhusu alipokuwa akitoa pesa za kununua vitu ghali (uk. 46). Mabitla (2006) anaeleza kwamba wanaotumia dawa za kulevya hupandwa na hasira haraka hasa wanapokosolewa kitabia.

Katika riwaya hiyo, Maanzo amesawiriwa kama mlevi wa pombe na mvutaji wa bangi. Sue anaeleza tabia hiyo kwa maneno yafuatayo:

> "Maanzo alionekana akiwa amelewa tayari na alikuwa na msokoto wa bangi aliokuwa anavuta akiuficha nyumanyuma mgongoni." (uk. 51)

Uraibu wa pombe na bangi unamfanya Maanzo kuwa jambazi sugu linaloshirikiana na akina Omido katika genge la RIZIKI kuwaibia wakazi wa Kisera (uk. 51). Imtiaz, Yasin & Yaseen (2010) wanaeleza kwamba miongoni mwa sababu ambazo mara kwa mara huchangia ukatili wa vijana ni matumizi ya vileo na dawa za kulevya. Nao Johnson & Belfer (1995) wanaeleza kwamba dawa za kulevya husababisha ukatili kupitia ushawishi unaoletwa nazo na matendo

yanayohusiana na ulanguzi wa dawa zenyewe hasa miongoni mwa watu wenye kipato cha chini.

### 3.1.2.2 Ushawishi wa marika

Kichocheo kingine kinachoashiriwa na waandishi wa kazi teule za fasihi ya watoto kwamba kinasababisha ukatili miongoni mwa watoto ni ushawishi wa marika. Mabitla (2006) anaeleza kwamba wanaojiunga na magenge ya hirimu hushurutika kufuata kanuni zilizowekwa na magenge hayo ili kukubalika na kudumisha urafiki. Meter, Casper & Card (2015) nao wanaeleza kuwa tabia ya ukatili miongoni mwa watoto huchochewa kwa kuiga matendo ya hirimu katika magenge. Katika riwaya ya *Siku Njema,* Selemani Mapunda anatekeleza matendo ya ukatili akishirikiana na magenge ya vijana wa rika lake. Katika mji wa Tanga, anamshambulia hedimasta wa shule ya Tanga akishirikiana na vijana hao (uk. 20). Anapokimbilia jiji la Mombasa, anashirikiana na Bakari na magenge mengine katika kutekeleza visa vya wizi wa kimabavu (uk. 102). Katika riwaya hiyo, Bakari anapotoka jela na kukuta nyumba yao imetiwa kufuli, anahiari kwenda kuishi na 'rafikize' licha ya ushawishi wa Rashid wa kutaka akae naye (uk. 65). Kutokana na ushawishi wa marika, Bakari anapotoka zaidi kitabia. Yeye na Selemani Mapunda wanapopigwa risasi na kuuawa na polisi, vyombo vya habari vinaeleza kuwa walikuwa miongoni mwa genge lililowahangaisha wakazi wa Mombasa kwa muda mrefu (uk. 130-131).

Katika riwaya ya *Tumaini*, Majuto, Kijungwe na vijana wengine wanahamia kwenye madanguro ya mtaa wa Mkwajuni ambapo wanaungana na vigoli kutoka mtaa huo kufuja mali na ngawira nyingine (uk. 111). Majuto anamvamia mke wa mfanyabiashara anayeitwa Karim akiwa kwenye genge la vijana wengine akiwamo Kijungwe (uk. 109). Majuto na Kijungwe na genge lake wanajaribu kuiba kwenye ofisi za D.O ila mpango wao unatibuliwa na polisi ambao wanampiga Majuto risasi mguuni na Kijungwe begani (uk.143). Katika shule ya Kivulini, Majuto anashirikiana na Kijungwe kutekeleza matendo ya ukatili. Mwandishi anasema kwamba vijana hao wawili walikuwa na ukaidi uliowasumbua walimu na wanafunzi (uk. 20). Kisa kimojawapo cha usumbufu huo kinadhihirika wanapovunja ofisi ya mwalimu mkuu, Bwana Mwadime, kuiba madaftari na kuyauza kwa Bwana Karim (uk. 20). Majuto anapofukuzwa shuleni kwa sababu ya kuwaasi walimu, Kijungwe naye anakatisha masomo yake na kujiunga naye katika kutekeleza visa mbalimbali vya uhalifu.  Bi. Halima anamsimulia mumewe tukio ambapo Majuto na genge lake wanakimbizwa na polisi baada ya kuiba kisanduku cha vito cha Karim. Kauli ya Bi. Halima inatueleza kuwa Majuto alikuwa akishirikiana na genge kubwa.

> “Nasikia Majuto amejificha katika mtaa mwingine pamoja na washirika wake.”(uk. 110).

Matukio haya katika riwaya ya *Siku Njema* na *Tumaini* yanaonyesha jinsi ushawishi wa marika unaweza kuwa na mchango mkubwa katika tabia ya ukatili ya watoto. Katika riwaya ya *Lulu ya Maisha*, maisha ya Omido yanabadilika

kutokana na ushawishi wa hirimu zake. Maelezo ya Sue yanadhihirisha athari hiyo.

> “Omido ndiye aliyenitia uchungu zaidi. Angekuwepo angerudi shuleni hata yeye. Lakini aliaathiriwa na hirimu zake kuamini si vibaya kula cha haramu kisicho chako cha halali.’’(uk. 60).

Katika riwaya hiyo, kijana Maanzo anaelezewa kuwa mmoja wa ‘wanachama’ wa genge linalojiita RIZIKI ambalo linawahangaisha wakazi wa mtaa wa Kisera kutokana ma matendo yao ya wizi wa kimabavu. Matukio ya ushawishi wa marika katika riwaya hizi tatu yanaeleweka vyema kupitia maelezo ya Meter, Casper & Card (2015) kwamba tabia ya ukatili ya watoto inaweza kuchochewa na matendo ya hirimu zao katika magenge.

#### 3.1.2.3 Imani na itikadi katika jamii

Imani na itikadi zinazotawala katika jamii ya mtoto ni mambo mengine yanayochangia tabia ya ukatili. Katika riwaya ya *Siku Njema*, imani za wenyeji wa mji wa Tanga kuhusu ndoa inajitokeza kuwa sababu mojawapo inayochangia ukatili miongoni mwa watoto. Kitendo cha kumzaa mtoto nje ya ndoa katika jamii hiyo kinachukuliwa kuwa haramu. Jambo hili linaifanya jamii hiyo kudhihirisha ukatili kwa watoto waliozaliwa nje ya ndoa kwa kuwaita majina kama vile ‘wanaharamu’ na ‘wasi baba’. Taswira hiyo ndiyo inayojitokeza katika shule ya Tanga ambapo Selemani Mapunda na wanafunzi wenzake wanadhihirisha ukatili waliojifunza katika jamii yao dhidi ya Kongowea Mswahili. Kila wakati

Kongowea Mswahili alipowashinda akina Mapunda masomoni, walimwonea gere na kumuumbua kwa kauli ‘mwanaharamu msi baba’ (uk. 8).

Imani nyingine iliyotwala mji wa Tanga ni ile ya usihiri na mambo ya uganga. Imani hii imeenea hata miongoni mwa watoto. Katika riwaya ya *Siku Njema*, Selemani Mapunda anasemekana kwenda kwa mganga wa Tanga ili kupigiwa bao na kuelezewa chanzo cha kutofaulu kwake masomoni. Mganga huyo anamweleza kuwa Kongowea Mswahili ndiye aliyekuwa amemroga (uk. 8). Ulaghai wa mganga unamfanya Mapunda kumchukia Kongowea Mswahili na kumwandama ili kulipiza kisasi. Chuki hiyo inadhihirika kupitia ujumbe wa kutisha ambao anamwandikia Kongowea Mswahili kwenye choo cha wapangaji:

> *“Kongoweya wewe ndiye uliniharipiya bahati yangu, ulipokimbilia Mwambasa ulifikili sitokupata. Nitakuua…*” (uk. 100)

Aidha, Kongowea Mswahili mwenyewe anaeleza jinsi ulaghai wa mganga unavyokuwa sababu ya Selemani Mapunda kumchukia. Kauli ifuatayo inaeleza jambo hilo:

> “Maisha yangu yalikuwa hatarini. Ulaghai wa mpiga ramli, kisasi na bangi ndizo dira zilizomuandisi Selemani.”(uk. 103).

**3.1.2.4 Utabaka katika jamii**

Katika riwaya ya *Lulu ya Maisha,* mwandishi anaonyesha jinsi utabaka katika jamii wanamokulia watoto unaweza kuwa sababu mojawapo inayosababisha ukatili miongoni mwa watoto. Katika riwaya hiyo, watu waliojaliwa nafasi ya hali maishani wanaamini kuwa umaskini unatokana na kukosa kusoma. Kwa hivyo,

wanaoishi katika mitaa ya mabanda na kufanya kazi za shokoa ili kujikimu wanachukuliwa na wenzao wenye kipato kama wajalaana waliokataa kusoma. Jambo hili linajidhihirisha kupitia mazungumzo baina ya Sue na baba yake ambayo yanarejelea wakazi wa mtaa wa mabanda wa Kisera: Sue anapomwuliza baba yake kosa lilikuwa la nani watu wale wakaishia kuishi maisha ya kutamausha, anaeleza kuwa ni lao kwa sababu walikataa kusoma (uk. 8). Kwa upande mwingine, maskini wanawaona waliojaliwa mali kama watu wenye kiburi na ubinafsi. Jambo hili linajitokeza bayana familia ya Tiito inaposhuka ngazi. Mke wake anapoamua kuhamia mtaa wa Kisera kwa kushindwa kumudu kodi ya nyumba kwenye mtaa wa fahari wa Onyoka, anakumbana na mwanamke mmoja muuzaji wa kibanda anayemdhihaki kwa maneno yafuatayo:

“Walikuwa wakiringa. Dunia ni ya kuringia?’’(uk. 15)

Chuki na uhasama baina ya matabaka haya mawili unakuwa chanzo cha matendo ya uhalifu kama vile wizi unavyodhihirika kupitia kwa wahusika watoto. Watoto hawa ambao wazazi wao wanakaa katika mtaa wa Mabanda wa Kisera wanaingia katika nyumba za majirani zao kuwaibia kwa kutumia nguvu. Omido anajipata katika hali hiyo wazazi wake wanapohamia katika mtaa wa Kisera. Maisha yanapokuwa magumu katika mtaa huu kutokana na kudodora kwa afya ya mama yake na hatimaye kutoweka kwake, anaamua kujitosa katika wizi wa kimabavu ili ‘kujichumia’. Mwandishi anaeleza kwamba aliingia kwenye nyumba za watu na kuiba mali waliyoyapata kwa jasho lao bila dhamira yake kumhukumu (uk. 60). Athari nyingine ya imani potovu baina ya matajiri na maskini inavyojitokeza

katika riwaya hii inatokana na chuki inayopulizwa na wazazi wenye nafasi ya hali kwa watoto wao kuhusu 'ukosefu'. Sue anaamini kuwa maisha waliyoishi watu wa mabanda yalikuwa ya kishenzi na ya kujitakia kwa sababu ya kutotaka kusoma. Hivi ndivyo anavyosema:

> "…nilishangaa jinsi ambavyo ningeishi hayo maisha ya kishenzi… waliyokaa wale watu baba aliowaita walaaniwa wa ulimwengu."(uk. 8)

Watson, Fischer, Andreas & Smith (2004) wanaeleza kuwa watoto walioathiriwa na masuala fulani hasi katika jamii yao huwa katili kwa kuamini kuwa ukatili ni njia moja ya kuyazuia masuala hayo hasi. Mabitla (2006) naye anaeleza kuwa watoto hugeuka katili wanapotazama matendo fulani ya ukatili yakiruhusiwa au kutukuzwa katika jamii yao.

### 3.1.3 Sababu zinazohusiana na shule

Lengo la shule ni kutoa mafunzo kwa wanafunzi ili kukuza maarifa na ujuzi ambao utawasaidia kupata ajira, kuendeleza taaluma zao na kuchangia katika ustawi wa jamii (Smith, 2003). Smith anaendelea kufafanua kuwa shule ni mazingira mwafaka kwa watoto na vijana kutangamana na wenzao, walimu na wafanyakazi wengine wa shule. Ni katika mazingira hayo ambapo watu walimu na wafanyakazi wengine wa shule huwasisitizia watoto kuiga tabia na mienendo ambayo inakubalika shuleni. Hata hivyo, watoto hujikuta wakiiga tabia ngeni kutoka kwa wenzao kwenye Makundi. Baadhi ya tabia hizo huwa za kikatili na zinazokinzana na zile walizoelekezwa na watu wazima kuzifuata. Katika riwaya ya *Siku Njema* ukatili wa kimatamshi katika shule ya Tanga unaashiriwa

kusababishwa na ushawishi wa hirimu za wanafunzi. Kongowea Mswahili anaelezea ukatili huo kwa maneno yafuatayo:

> "Nilipowashinda masomoni, wenzangu walisikika wakikengemeka, "Hiki kitoto kichekechea kinatushindaje masomoni, kwani kina akili nyingi vipi?'' Wengine walianza kunionea kijicho na kuniramba kisogo. Wenye ushupavu na ushari walinibeua waziwazi, bila kificho, na kuniita ''kikojozi'' au ''mwanaharamu".'(uk. 8).

Tabia ya ukatili ya baadhi ya wanafunzi wa Tanga inachochewa na makundi ya wanafunzi. Selemani Mapunda ni mmoja wa wanafunzi wenye ushawishi mkubwa katika makundi hayo kutokana na maelezo ya Kongowea Mswahili. Anasema kwamba hakuna aliyemdunisha na kumuumbua kuliko kijana mmoja aliyeitwa Selemani Mapunda (uk. 8). Watoto wengine ambao wamesawiriwa kwamba wameathiriwa na ushawishi wa kimakundi ni binamu zake Kongowea Mswahili ambao ni Daniel, Butambo na Rehema. Hawa wanaelezewa na Kongowea Mswahili kwamba hawakutaka hata chembe kunasibishwa naye. Kongowea Mswahili anaeleza kwamba alipochekwa, binamu zake walicheka na waliomcheka (uk.8). Ukatili unaotokana na ushawishi wa hirimu vile vile unajitokeza katika riwaya ya *Tumaini.* Majuto na Kijungwe wanachocheana katika kutekeleza visa vya utovu wa nidhamu ambao unaelezewa kuwa ulimsumbua sana mwalimu mkuu wa shule ya Kivulini (uk. 20). Ijapokuwa Majuto na Kijungwe wanaelezewa kuwa na tabia inayorandana sana, yapo mambo mengi ambayo yanaonyesha kuwa Kijungwe ameathiriwa na tabia ya Majuto. Kwanza, Majuto anapofukuzwa shuleni baada ya matendo yake ya ukatili

kukithiri, Kijungwe pia anaacha shule na kujiunga naye katika kutekeleza uhalifu. Licha ya hayo, katika matukio mengi ya uhalifu, Majuto anakuwa katika mstari wa mbele huku Kijungwe akisawiriwa kuwa kikaragosi chake (uk. 20, 53, 71, 111 na 143). Katika riwaya ya *Lulu ya Maisha*, udhalimu wa wanafunzi dhidi ya wenzao unashawishiwa na hirimu. Sue anasimulia jinsi wanafunzi wa shule ya St. Mary's Girls Boarding wanavyodhihirisha ukatili wa kimatamshi dhidi yake anapojiunga na shule hiyo. Baadhi yao walimwamrisha kuwarejelea viranja kwa kutumia jina 'your honour' (uk. 70). Smith (2003) anaeleza kuwa katika mazingira ya shule, kila mwanafunzi huja na tabia tofauti ambayo amejifunza katika jamii yake. Wanafunzi hawa hukutana na hirimu zao ambazo huwafunza tabia zaidi; nyingine zinazokinzana na jamii.

Adhabu kali na kukosekana kwa mikakati mwafaka ya kurekebisha na kudhibiti visa vya utovu wa nidhamu katika baadhi ya shule kunaashiriwa na waandishi wa vitabu teule vya fasihi ya watoto kama sababu nyingine inayochangia ukatili miongoni mwa watoto. Grundy & Blandford (1999) wanaeleza kwamba wadau wa elimu wanapaswa kung'amua kuwa utovu wa nidhamu shuleni si tukio la muda mfupi hivyo basi wanapaswa kuibuka na mikakati kabambe ya kuikabili tabia hiyo badala ya kutumia suluhu za muda mfupi ambazo huenda zisiwe na matokeo ya kuridhisha. Katika riwaya ya *Siku Njema*, hedimasta wa shule ya Tanga anajaribu kuirekebisha tabia ya Selemani Mapunda ya kutozingatia usafi wa kibinafsi kwa kumwamrisha kuoga mbele ya wanafunzi wenzake.

Tukio hili linasimuliwa na Kongowea Mswahili kwa maneno yafuatayo:

> “Hedimasta aliwaamuru vigoli wawili wajaze maji kwenye karai….Basi kengele ya paredi ililia, shule nzima ikajumuika pamoja. Maji yale yakaletwa mbele ya hadhara…Hedimasta akamwita Selemani Mapunda na kumpa kipande cha sabuni ya *Sunlight*. Kisha akamwamuru aoge mbele ya kaumu ya wanafunzi.”(uk. 20)

Ijapokuwa adhabu ya mwalimu mkuu ilikuwa na nia nzuri ya kuirekebisha tabia ya Mapunda ambayo inaelezewa kwamba iliwasumbua wenzake, ni kali mno. Badala ya adhabu yenyewe kuleta matokeo chanya, inaishia kuwa chanzo cha Mapunda kutoroka shule. Kuambiwa kuoga kadamnasi ni jambo ambalo linamtia Selemani Mapunda woga na aibu na kufanya viwango vyake vya kujithamini kushuka. Hali hii inadhihirika kupitia maneno anayoyatamka wakati anapomshambulia mwalimu mkuu:

> “Ati alitaka nioge mbele ya hadhara ile. Wallahi! Tutaliua hili. Na liwe liwalo.’’(uk.21)

Aidha, adhabu ya mwalimu mkuu inakuwa chanzo cha Selemani Mapunda kulipiza kisasi dhidi yake wanapomvamia na vijana wengine nje ya shule (uk. 20). Adhabu inayokaribiana na ya Mapunda inadhihirika katika riwaya ya *Tumaini*. Mwalimu mkuu, Bwana Mwadime, anajaribu kuirekebisha tabia ya utovu wa nidhamu ya Majuto kwa kumwamuru kupiga magoti mbele ya wanafunzi wenzake kisha anamfukuzia nje ya darasa somo linapoendelea (uk. 21). Adhabu ya Bwana Mwadime inaelezewa kumkasirisha Majuto ambaye anachukua mawe na kumrushia mwalimu kupitia dirishani. Isitoshe, hatua ya mwalimu mkuu ya kumwandikia Majuto barua kali ya kumfukuza shuleni inadhihirika kama suluhu

ya muda mfupi ya kupunguza udhia shuleni. Hata hivyo, tabia ya ukatili ya kijana huyo inakithiri anapopata uhuru mwingi nje ya shule. Hivi ndivyo mtunzi wa riwaya ya *Tumaini* anavyolisimulia tukio hilo:

> "Baada ya kufukuzwa shule alikuwa (Majuto) tisho mitaani. Aliwaibia watu mali zao na kubaka mabinti za watu kwa kuwavizia vichochoroni (uk. 71).

Blandford (1998) anaeleza kwamba iwapo wanafunzi hawajiheshimu, basi hawawezi kuwaheshimu wengine. Mtaalamu huyu anaendelea kufafanua kuwa watoto ambao hawajithamini hudhihirisha tabia ya ukaidi na huwa wagumu kuelekeza. Hasira na udhia (*frustration*) wao huwafanya watende mambo bila kuwazia kwa kina na kuishia kusababisha usumbufu kwa wale wanaotagusana nao.

Katika riwaya ya *Tumaini*, Majuto anapoanza kudhihirisha tabia ya ukatili darasani ambapo anawaibia wanafunzi wenzake vitabu, kalamu na hata mabegi (uk. 71), udhaifu mmoja unaodhihirika kupitia mwalimu wa darasa la Majuto ni kutochunguza ili kufahamu mwanafunzi anayehusika katika wizi wa nyenzo za wanafunzi na kuirekebisha tabia hiyo mapema. Kutochukuliwa kwa tahadhari zifaazo kunachangia kuzorota kwa tabia ya Majuto inavyoelezewa na mtunzi kwa maneno yafuatayo:

> "Wizi ule wa darasani sasa ulikita mizizi na kumfanya Majuto kuwa mwizi mtajika."(uk. 71).

Katika riwaya ya *Siku Njema*, shule ya Tanga ina wanafunzi katili ambao wanamdhalilisha Kongowea Mswahili anapowashinda masomoni. Baadhi ya

matusi na dhihaka zinazoelekezwa kwa Kongowea Mswahili ni za waziwazi anavyosema mwenyewe: “wenye ushupavu na ushari walinibeua waziwazi bila kificho na kuniita ‘kikojozi’ au ‘mwanaharamu’ (uk. 8). Isitoshe, baadhi ya wanafunzi, kwa mfano Selemani Mapunda, wanachukua hatua ya kwenda kwa waganga kupigiwa bao na kuelezewa kwa nini hawakuwa wakifanya vyema masomoni. Msururu huu wa utovu wa nidhamu ungedhibitiwa iwapo shule husika zingeweka mikakati mwafaka ya kukabili visa hivyo wanavyoshauri Grundy & Blandford (1999).

Katika riwaya ya *Lulu ya Maisha*, dhuluma za wanafunzi dhidi ya wenzao zinajidhihirisha katika shule ya St. Mary’s Girls Primary Boarding ambapo Sue anadhalilishwa na wanafunzi wenza anapojiunga na shule hiyo (uk. 70). Kulegea kwa mwalimu katika kudhibiti tabia hasi za wanafunzi kunavuruga mchakato wa ujifunzaji (Blandford, 1998).

Sababu kadha za mazingira ya shuleni zinachangiana katika kukuza tabia ya ukatili miongoni mwa watoto inavyodhihirika katika riwaya teule za fasihi ya watoto. Baadhi ya sababu hizo zinaweza kuwa na hatari ya kiwango cha juu ya kusababisha ukatili ilhali nyingine zinajidunduliza moja juu ya nyingine na kufikia kiwango cha kusababisha ukatili (Watson, Fischer, Andreas & Smith, 2004). Hali hii inakubaliana na mhimili wa nadharia ya ujifunzaji wa kijamii ya Bandura (1977) unaeleza jinsi mambo mbalimbali yakiwamo ujifunzaji na mazingira huchangiana katika kusababisha tabia ya ukatili miongoni mwa watoto.

## 3.2 Athari Za Ukatili wa Watoto kwa Wahusika Wengine Katika Vitabu Teule vya Fasihi ya Watoto

Matendo ya watoto katili huwa na athari mbalimbali kwa watu wengine katika jamii (Ndibalema, 2003, Omoteso, 2010, Mabitla, 2013 na Tambawal, 2017). Kwa mujibu wa Ndibalema, watoto katili huwakosesha watu usalama, huwadhalilisha wenzao na kufanya viwango vyao vya kujithamini kushuka. Omoteso (2010) naye anaeleza kuwa ukatili wa watoto kwa watoto wengine huwatia woga unaowafanya kuchukia mazingira ya shule kwa kuyaona kama yasiyo salama Vilevile watoto hao hukumbwa na madhara ya muda mrefu ya kisaikolojia ambayo huwafanya kujitenga na wenzao kwa kuhisi kutokuwa na thamani. Utafiti huu utashughulikia athari za aina tatu ambazo ni pamoja na athari zinazoonekana bayana, za kisaikolojia na zile zinazowafanya waathiriwa kujitenga na wanajami wengine.

### 3.2.1 Athari zinazoonekana bayana

Athari zinazojidhihirisha bayana hutokana na majeraha ya kimwili yanayosababishwa kwa matumizi ya mikono au fimbo miongoni mwa silaha nyingine (Kavuria, 2008). Katika riwaya ya *Siku Njema,* Selemani Mapunda na wenzake wanampiga na kumjeruhi mwalimu mkuu wa Tanga. Mwandishi anaeleza kuwa mwalimu huyo ambaye alikuwa akigaragara chini kutokana na kipigo cha Mapunda na wenzake alikuwa amejeruhiwa vibaya kichwani. Jeraha hilo ambalo linasababishwa na kigongo cha Selemani Mapunda linamfanya hedimasta kuvuja damu kwa wingi. (uk. 21). Katika riwaya ya *Tumaini*, Majuto

na vijana wengine watatu wanamvamia mke wa mfanyabiashara anayeitwa Karim na kumkaba koo kiasi cha kumfanya azirai kisha wanatoweka na kisanduku chake chenye vito (uk. 109). Tambawal (2017) anafafanua kuwa mikwaruzo, michubuko na makovu yanayoachwa kwenye ngozi ya waathiriwa wa ukatili wa watoto ni miongoni mwa athari zinazoonekana bayana. Waandishi wa riwaya hizi wameziakisi athari zinazotokana na usababishaji wa majeraha kiuhalisia. Visa vya watoto wanaowavamia wanajamii wengine na kuwasababishia majeraha mwilini vimekuwa vikiripotiwa mara kwa mara na vyombo vya habari. Kwa mfano, katika gazeti la *The Standard* Abuga (2021) anasimulia tukio ambapo mwanafunzi wa kidato cha tatu katika Shule ya Upili ya Kisii anasemekana kuwadunga walimu wawili kisu na kuwajeruhi vibaya. Tukio hilo lilijiri mwanafunzi mwenyewe alipoulizwa sababu iliyomfanya kuchelewa kuripoti shuleni.

Athari nyingine zinazoonekana bayana zinajidhihirisha kupitia wizi, unyang'anyi na uharibifu wa mali (Lawson, 2005). Katika riwaya ya T*umaini*, Majuto na Kijungwe wanavunja ofisi ya Bwana Mwadime na kuiba madaftari (uk. 20). Wazazi wa vijana hao wanaathirika kiuchumi kwa sababu wanashurutishwa na usimamizi wa shule kulipa gharama ya mali iliyoibwa. Vilevile, wanafunzi wa shule ya Kivulini wanaathiriwa na kitendo cha Majuto cha kuwaibia vitabu, kalamu na mikoba (uk. 71). Licha ya hayo, kinaripotiwa kisa ambapo Majuto anaiba baiskeli na kuiendesha kwa kasi na kutokomea mtaa wa mabanda (uk. 70). Katika riwaya ya *Siku Njema*, Selemani Mapunda na Bakari wanasawiriwa kama

wezi wa mali na magari (uk. 130-131). Katika riwaya ya *Lulu ya Maisha*,Omido anasawiriwa kama mwizi ambaye anaingia katika nyumba za majirani zake na kuwaibia mali waliyoichuma kwa kuawa jasho (uk. 60). Mwandishi anasimulia kisa kimoja ambapo Omido na genge lake wanamwibia mfanyabiashara anayeitwa Sultani (uk. 48). Bourguignon (2000) anafafanua kuwa wizi na unyanganyi ni miongoni mwa athari zinazoonekana bayana. Matendo hayo hudidimiza uchumi, husababisha umaskini na kutokuwepo kwa usawa hivyo basi kutoa mwanya wa mzunguko wa visa vingine vya ukatili. Athari hizi pia zimeakisiwa kihalisia na waandishi wa vitabu teule vya fasihi ya watoto; jambo ambalo linathibitisha kuwa ni matukio ambayo hutokea katika jamii. Kindiki (2009) anaeleza kwamba uharibifu wa mali unaotekelezwa na wanafunzi shuleni umekuwa ukiangaziwa mara kwa mara na vyombo vya habari nchini Kenya. Mtaalamu huyu anaendelea kufafanua kwamba licha ya kuwa serikali ya Kenya imekuwa ikiweka mikakati ya kukabiliana na uharibifu huu, bado ungali tatizo shuleni. Ndambuki (2016) naye anaeleza kuwa wizi miongoni mwa wanafunzi hasa katika shule za umma za mabweni umekuwa tatizo linaloathiri maisha ya wanafunzi wanaosomea shule hizo.

### 3.2.2 Athari za kisaikolojia

Guerra, Huessmann & Spindler (2003) wanaeleza kwamba athari za kisaikolojia husababishwa kupitia vitisho vya kutamka au vinavyojitokeza kwa njia ya maandishi kama vile barua au ilani. Vitisho hivi huwatia watu wengine woga, kuwafanya kujihisi wanyonge na kufanya viwango vyao vya kujithamini kushuka

miongoni mwa madhara mengine ya kisaikolojia. Vilevile, matamshi na matendo ya wahusika katili huwaaibisha wanajamii wengine. Katika riwaya ya *Siku Njema*, Kongowea Mswahili anaathirika kwa njia mbalimbali kisaikolojia kutokana na ukatili anaofanyiwa na Selemani Mapunda na wanafunzi wengine. Wanafunzi hao wanapomtukana kwa kumwita, ‘mwanaharamu msi baba’ anakereka moyoni, anakosa furaha na kujihisi mnyonge anavyoeleza kwa maneno yafuatayo:

> “Hili la kuitwa ‘‘mwanaharamu’’ lilinikeketa maini kama msumeno na kunikosesha furaha daima. Hakuna aliyenidunisha na kuniumbua kuliko kijana mmoja aliyeitwa Selemani Mapunda….” (uk. 8).

Ujumbe na barua za vitisho ambazo Selemani Mapunda anamwandikia Kongowea Mswahili zinamtia woga na kumkosesha amani na utulivu. Kongowea Mswahili anahama mji wa Tanga kutokana na barua ya vitisho iliyoandikwa kwa wino mwekundu anayoipokea kutoka kwa Selemani Mapunda. Athari ya ujumbe wa barua hiyo inajitokeza katika usemi wa Kongowea Mswahili.

> “Ilikuwa barua ya kuogofya. Baada ya kuisoma nikaikunja na kuiweka mfukoni... Nilielewa fika kuwa haukuwa mzaha. Maisha yangu yalikuwa hatarini.’’(uk. 34).

Katika mji wa Mombasa, Selemani Mapunda ananakili maandishi ya kutisha kwenye ukuta wa choo cha wapangaji. Maandishi hayo yanaeleza kinaganaga kwamba Kongowea Mswahili ndiye aliyemharibia Mapunda nyota yake. Mapunda anavisisitiza vitisho vyake kwa kauli ‘nitakuua’ (uk. 100). Ujumbe huu pamoja na kukutana ana kwa ana na Selemani Mapunda vinamwathiri kisaikolojia na kumtia woga mwingi. Vitisho hivyo vinamfanya kuharakisha mpango wake wa

kuhama Mombasa kwenda bara (uk. 103). Watoto ambao ni waathiriwa wa ukatili wa wenzao aghalabu huyaogopa mazingira wanayokaa kama yasiyopendeza na yasiyokuwa salama. (Kavuria, 2008, Omoteso, 2010)

Katika riwaya ya *Tumaini*, mwandishi anaeleza kwamba Majuto na Kijungwe walikuwa na mapepe ambayo yaliikosesha shule nzima amani na utulivu (uk 20). Inaelezewa kuwa Majuto alikuwa amefukuzwa shuleni mara kwa mara kwa sababu ya utovu wake wa nidhamu uliowakosesha wengine usalama shuleni.

Tumaini anadhihirisha ukatili kwa Kijungwe kwa kumrushia jiwe kutokana na athari ya maneno ya mvulana huyo kwake.

> “Tuma, hivi ulikimbia tohara kwa sababu ya woga au mchumba uliyechaguliwa hukumpenda?’’ (uk.72)

Mwandishi anaeleza kuwa swali la Kijungwe la kumkejeli Tumaini lilimfanya Tumaini kukasirika na kumjibu Kijungwe kwa hasira (uk. 72). Majibizano yanapoendelea, Tumaini anamrushia Kijungwe jiwe ambalo linaishia kumjeruhi mwalimu. Lawrence, Yoon, Langer & Eunyoe (2009) wanaeleza kwamba kejeli, vitisho na kumfanya mtu mwingine kukasirika au kuhisi kudunishwa ni baadhi ya athari za kisaikolojia zinazosababishwa na ukatili.

Katika riwaya hiyo, Tumaini anajihisi kama mja asiye na thamani baada ya Majuto kumdhalilisha kwa kumwambia kwamba yeye alikuwa msichana bure tu na kwamba hapakuwa na tofauti kati yake na wasichana wengine aliowahi kukutana nao (uk. 89). Mwandishi anaeleza kwamba baada ya Majuto kuondoka,

Tumaini anatiririkwa na machozi kutokana na maneno ya Majuto yanayomfanya kuhisi kudunishwa wanavyofafanua Lawrence na wengine (2009)

Watoto katili huwaaibisha, kuwashushia heshima, kuwahuzunisha na kuwaletea balaa wazazi wao. Jambo hili linajitokeza katika riwaya ya *Siku Njema* ambapo sifa mbaya za Selemani Mapunda zinamshushia baba yake heshima katika mji wa Tanga. Jambo hili linajitokeza kupitia maneno anayoyatamka mjombawe Kongowea Mswahili anayeitwa Kitwana:

> "Lahaula! Mwanawe Mzee Mapunda! Lile jambazi! Alaa! Keshatoka jela kumbe…? (uk. 41-42).

Katika riwaya ya *Tumaini*, Majuto anawaabisha na kuwazulia wazazi wake balaa. Siku aambayo Majuto anaiba baiskeli na kukimbia mitaani huku akifuatwa na vijana wenye hasira, Bi. Halima anakiona kitendo hicho kama kinachowaaibisha wazazi na kuwazulia balaa.

> "Lahaula! Maajabu ya Firauni haya! Mwana yule amegeuka kuwa jizi sugu. Mnh! Anawaaibisha wazazi wake…Ama kweli mchuma janga hula na wa kwao.''(uk. 70).

Majuto anapopigwa risasi na polisi na kulazwa hospitalini akiwa hali mahututi, mama yake anaingiwa na kivumvu kinachomfanya kuomboleza bila kukoma na kugaragara kwenye sakafu ya nyumba yake. (uk. 147). Maneno anayoyatamka Bi. Selina yanamdhihirisha kama mzazi anayejutia kitendo cha kumzaa Majuto.

> "Ah! Usinitajie Majuto. Mimi sina mwana tena Tumaini mwanangu eee!"(uk. 147).

Katika riwaya ya *Lulu ya Maisha,* kifo cha Omido kinachosababishwa na polisi kinamtia dada yake, Sue, uchungu tele moyoni. Sue anaeleza kuwa lau Omido asingalijitosa katika uhalifu angalipata nafasi ya kuendeleza masomo yake (uk. 60). Athari za kisaikolojia zinazosababishwa na watoto katili zimeakisiwa kihalisia na waandishi wa vitabu teule vya fasihi ya watoto. Mambo hayo huangaziwa mara kwa mara na vyombo mbalimbali vya habari. Kwa mfano, katika gazeti la *The Standard* Mutura &Nzau (2022) wameandika kuhusu tukio ambapo mwanafunzi wa kidato cha kwanza katika shule ya upili ya Aquinas alijaribu kujiua baada ya kusemekana kulawitiwa na wanafunzi fulani wakiwa katika bweni.

### 3.2.3 Mwathiriwa kujitenga na wanajamii wengine

Ukatili huathiri uhusiano wa mwathiriwa na marafiki zake na wanajamii wengine (Tambawal, 2017). Mtaalamu huyu anaeleza kuwa mtoto ambaye ni mwathiriwa wa vitendo vya ukatili wa wenzake hujitenga na wenzake kwa sababu ya kukosa kujithamini. Vile vile, mtoto huyo hukosa imani kwa wanajamii wengine.

Katika Riwaya ya *Siku Njema,* Kongowea Mswahili anajikuta pweke shuleni kutokana na ukatili anaotendewa na wenzake. Anaeleza kwamba hata binamu zake ambao ni Daniel, Butambo na Rehema hawakutamani hata chembe kunasibishwa naye. Walimbeza na kumwambaa shuleni walivyofanya wanafunzi wengine watundu (uk. 18). Aidha, Kongowea Mswahili alipochekwa, binamu

zake walicheka na wale waliomcheka (uk. 8). Upweke wa Kongowea Mswahili shuleni unadhihirika kupitia usemi wake:

> "Niliona fundo chungu moyoni. Msichana mmoja tu aliyeitwa Vumilia, binti yake Diwani Abdala, wa Baraza la mji wa Tanga, ndiye peke yake aliyenitetea mbele ya bughudha za Selemani na wenzake."(uk. 8)

Katika riwaya ya *Tumaini,* Tumaini anajipata pweke shuleni mwake kwa sababu ya mizaha na kejeli za baadhi ya wanafunzi wenzake wakiwamo Juma na Kijungwe (uk. 44). Wanafunzi hao walimdhihaki kutokana na masaibu yanayomkumba wakati baba yake alitaka kumpasha tohara kwa lazima. Wengine walimkebehi kwa lengo la kutaka kumvunja moyo masomoni hasa wale aliokuwa akiwashinda darasani mwake.

Katika riwaya ya *Lulu ya Maisha*, Semo anajihisi pweke kutokana na ukatili anaotendewa na binamu zake ambao wanampiga na kumtumia kama msichana wa kazi (uk. 17-18). Kuvurugika kwa uhusiano baina ya Semo na binamu zake kunamfanya kutoroka nyumbani na kwenda kuishi na watoto wanaozurura mitaani.

### 3.2.4 Hitimisho

Sura hii imeangazia sababu mbalimbali zinazochangia tabia ya ukatili miongoni mwa watoto na athari za tabia ya ukatili kwa wahusika wengine. Sababu za kifamilia, za kijamii na zinazohusiana na shule zilijitokeza kuwa miongoni mwa zile zinazochangia matendo hayo ya ukatili. Aidha, ilibainika kuwa matendo ya watoto katili husababisha athari zinazoonekana bayana na za kisaikolojia. Mhimili

wa nadharia ya ujifunzaji wa kijamii unaoonyesha jinsi sababu mbalimbali huchangiana katika kusababisha ukatili wa watoto na ule wa uhalisia unaoeleza jinsi athari za ukatili zilivyoakisiwa kihalisia ilitumiwa kwa ufaafu.

# SURA YA NNE

# MIKAKATI YA KUUKABILI UKATILI MIONGONI MWA WATOTO KATILI KATIKA VITABU TEULE

## 4.0 Utangulizi

Sura ya tatu ilifafanua sababu zinazochangia ukatili miongoni mwa watoto na athari za ukatili huo kwa wahusika wengine, jinsi zinavyojitokeza katika vitabu teule vya fasihi ya watoto. Sababu za kifamilia, za kijamii na za shuleni zilielezewa kama miongoni mwa zile zenye mchango muhimu katika kuchochea tabia hiyo. Athari zilizo bayana na zile za kisaikolojia ziliangaziwa. Sura hii imeangazia baadhi ya mikakati ya kuukabili ukatili miongoni mwa watoto jinsi ilivyoashiriwa na waandishi wa vitabu teule vya fasihi ya watoto. Mihimili miwili ya nadharia ya ujifunzaji wa kijamii ya Bandura (1977) imetumikizwa. Mhimili wa kwanza ni ule wa uimarishaji tabia ambao unaelezea kwamba tabia chanya hutuzwa ili kuiendeleza ilhali tabia hasi huzuiwa kwa njia ya adhabu. Mhimili huu uliusaidia utafiti katika kueleza jinsi uimarishaji tabia unaweza kuwa njia mwafaka ya kuukabili ukatili miongoni mwa watoto hasa pale unapoanza kujidhihirisha. Mhimili wa pili ni ule unaohusu mchango wa vielelezo vilivyoko katika mazingira anayoishi mtoto katika kukuza tabia yake. Mhimili huu ulisaidia utafiti kufafanua jinsi tabia ya ukatili miongoni mwa watoto inaweza kuzuiwa kwa kuwapa watoto vielelezo bora katika mazingira wanamokulia.

## 4.1 Mikakati ya kuukabili ukatili miongoni mwa watoto.

Watafiti mbalimbali wanaafikiana kwamba tabia ya ukatili miongoni mwa watoto inapaswa kushughulikiwa mapema utotoni (Webster-Stratton & Taylor, 2001; Hotton, 2003; Burnett, 2007 na Espelage, 2014,). Webster-Stratton & Taylor, Hotton na Espelage (wametajwa) wanashikilia kwamba umri wa takriban miaka minane mtoto anaposajiliwa kuanza masomo katika shule ya chekechea ni umri bora katika kuitambua tabia ya ukatili kwa urahisi na kuishugh ulikia. Wanaelezea kwamba tabia hii huanza kujitokeza hasa pale mtoto anapokuwa katika harakati za kutagusana na wenzake. Aidha, watafiki hawa wanaelezea umuhimu wa waalimu wa shule za chekechea kushirikiana na wazazi katika kuiwahi tabia hiyo punde tu inapochipuka. Webster-Stratton & Taylor (2001) wanasema kwamba, kuukabili ukatili baada ya mtoto kukomaa huibua changamoto nyingi. Burnett (2007) ana mtazamo kwamba tabia ya ukatili inapaswa kushughulikiwa mapema zaidi hata kabla mtoto kujiunga na shule ya chekechea kwa kutambua na kudhibiti chanzo cha tabia hiyo katika mazingira ya nyumbani. Maoni mengine yanayoibuliwa na watafiti waliotajwa yanahusu kuyapunguza mambo mbalimbali yenye uwezo wa kuchangia kutokea kwa tabia ya ukatili miongoni mwa watoto na kupalilia mazingira ya kuigwa ili kukuza tabia bora. Utafiti huu utafafanua jinsi mambo mbalimbali yenye uwezo wa kuchangia ukatili katika kiwango cha familia, jamii na shuleni yanaweza kupunguzwa na kupalilia mazingira yatakayopatia watoto vielelezo vya tabia inayokubalika.

### 4.1.1 Kuyapunguza mambo yanayoweza kusababisha ukatili katika familia

Wazazi na walezi wa watoto wana wajibu muhimu katika kuwakuza watoto kwa kukidhi mahitaji yao ya msingi, kuwashawishi na kuwaongoza kuiga tabia inayokubalika katika jamii miongoni mwa mwingine (Kitzmann, Gaylord, Holt & Kenny, 2003; Vanassche, Sodermans, Matthijs & Swicegood 2014). Sehemu hii iliangazia baadhi ya mambo yanayoweza kuchangia tabia ya ukatili miongoni mwa watoto katika kiwango cha familia na ambayo yanahitaji kupunguzwa ili kukabiliana na tabia hiyo.

#### 4.1.1.1 Kudhibiti matendo ya ukatili katika familia

Hotton (2003) anaeleza kuwa mazingira ya kifamilia yaliyosheheni matendo ya ukatili kwa mfano, dhuluma za kinyumbani yanaweza kumfanya mtoto kuwa katili kwa kuiga matendo hayo au kutumia ukatili kutatua mizozo itakayomkumba baadaye maishani. Katika riwaya ya *Tumaini* (2006), mwandishi anamsawiri Mzee Masumbuko kama mzazi katili ambaye amejawa dhuluma za kinyumbani na anayewalea watoto wake kwa ukatili mwingi (uk. 12). Mwandishi anaeleza kwamba kila wakati mzee huyu alipolewa pombe, hamaki zake zilivuka mpaka na kumfanya kila mmoja nyumbani kwake akiwamo mkewe na watoto wake kumwogopa. Licha ya hayo, ulevi ulimfanya kubwabwaja matusi mengi. Baadhi ya matusi hayo aliyaelekeza kwa mabinti wake ambao aliwaona kama bidhaa alizohifadhi nyumbani ili zimsaidie kupata mali. Isitoshe, Masumbuko alipowasili nyumbani akiwa mlevi alizua fujo kwa kuulizia chakula kwa hasira (uk.13). Mkewe anaelezewa kuwa mnyamavu na mwenye wasiwasi kutokana na vishindo

alivyofanyiwa na mumewe (uk. 13). Tabia ya udhalimu ya Masumbuko inawaathiri sana watoto wake hasa yule wa kiume anayeitwa Idi. Mwandishi anaeleza kwamba Idi alifanana sana na baba yake si kwa sura tu bali hata kwa tabia. Maneno yafuatayo yanachora taswira ya Idi:

> "Alikuwa mwingi wa hamaki na ukaidi. Kutokana na vitimbivyababake, kijana huyo mdogoaliwaona dada zake kama watumishi pale nyumbani. Alithibitisha haya kutokana na kauli alizoelekeza kwa dada zake, kama vile kuwaambia wao ni kama bidhaa za uwekezaji tu pale nyumbani."(uk. 14)

Si Idi tu ambaye ameathiriwa na tabia ya baba yake bali pia Tumaini. Tumaini amesawiriwa kama mwingi wa hamaki zinazomfanya kutumia ukatili kusuluhisha mizozo inayoibuka baina yake na wanafunzi wenzake. Kwa mfano, Kijungwe anapomtania kwamba alikataa kutahiriwa kwa sababu ya kuogopa kisu cha ngariba, anapandwa na hasira na kumrushia jiwe ambalo linaishia kumjeruhi mwalimu wao (uk. 73). Aidha, Idi anapomtania Tumaini kwamba ataolewa tu hata akikataa kutahiriwa, anasimama kwa hasira ili kumpiga Idi lakini Riziki, binamu yao, anamzuia (uk. 29).

Matendo ya ukatili wanayoyadhihirisha Idi na Tumaini yanatokana na dhuluma za kinyumbani zinazoendelezwa na baba yao ambapo watoto hao pia wanageuka wahanga. Hotton (2003) anaeleza kwamba mazingira ya kifamilia yaliyosheheni dhuluma za nyumbani huathiri watoto kwa njia hasi. Watoto hao huiga matendo ya ukatili ya wazazi wao au hutumia ukatili kama mbinu ya kutatua mizozo inayowakumba maishani. Maelezo ya mwandishi wa riwaya ya *Tumaini*

yanapitisha ushauri kwa wazazi kwamba njia mojawapo ambayo ukatili wa watoto unaweza kudhibitiwa ni kwa kulikabili tatizo la dhuluma za kinyumbani. Tofauti zinazoibuka baina ya wazazi zinapaswa kutatuliwa kwa amani na zifichwe kutoka kwa watoto. Mwandishi Momanyi analithibitisha jambo hili kupitia mhusika Bi. Halima. Wakati mmoja bintiye Bi. Halima anapomweleza mama yake kwamba pengine lengo la Mzee Masumbuko la kutaka Tumaini atahiriwe lilikuwa kumwoza ili apate mahari, Bi. Halima anauficha ukweli huo kutoka kwa Riziki na Tumaini kwa sababu hataki wawe na mtazamo hasi kuhusu Mzee Masumbuko. Nukuu ifuatayo inalithibitisha jambo hilo:

> Bi. Halima aliyafahamu vyema makusudio ya Mzee Masumbuko kwani alikuwa mroho sana wa pesa. Tayari alijua kiasi cha mahari ambacho angepata baada ya kumwoza Tumaini. Alifahamu pia jinsi mzee huyo alivyofisidi mapato yake ulevini. Lakini hakutaka kuyatamka hadharani mambo haya mbele ya watoto wale. Aidha, alijua yangemchoma sana Tumaini. Kwa hivyo, akamjibu Riziki, "Aa! Kama hilo lilikuwa lengo lake, Amina angekuwa ashanieleza kitambo."(uk. 24).

Maneno ya Bi. Halima yanapitisha ushauri kwa wazazi kwamba hawapaswi kuonesha tofauti zao waziwazi mbele ya watoto kwa sababu watoto hao wanaweza kuiga tabia ya ukatili. Aidha, mwandishi anathibitisha kuwa inawezekana wazazi kuwalea watoto wao katika mazingira yenye vielelezo vyema vya kuigwa; hiyo ikiwa njia bora ya kuikabili tabia ya ukatili. Analithibitisha jambo hili kupitia usawiri wa familia ya Shabani na mkewe anayeitwa Bi. Halima. Familia hii inatofautiana kimalezi na ile ya Mzee

Masumbuko. Shabani anasawiriwa kama mwanamume mwenye sifa nzuri za kuigwa kupitia maneno haya:

> "…alikuwa mtu adibu, mcheshi na mkarimu sana.''(uk. 10)

Sifa hizi za Shabani na ushauri anaompa bintiye, Riziki, vinamfanya Riziki awe mwadilifu. Mwandishi anaeleza kuwa Riziki alijifunza mengi kutokana na hulka ya baba yake na akasuluhia. Kauli ifuatayo inalielezea jambo hilo:

> "Riziki alijifunza mengi, akawa mweledi sana katika masomo."(uk. 11).

Licha ya hayo, Bi. Halima mwenyewe ni kielelezo cha kuigwa kutokana na tabia yake ya kuwa katika mstari wa mbele kupinga dhuluma zote dhidi ya wanawake na watoto wa kike. Maelezo ya mwandishi yanathibitisha hilo:

> "Bi. Halima alikuwa katibu katika kundi la akina mama ambalo lilishughulikia maslahi ya wanawake na watoto wa kike. Baadhi ya shughuli hizo ni pamoja na kukabiliana na ukeketaji wa wasichana.''(uk. 15).

Tumaini anapotoroka tohara ya lazima ya baba yake, Bi. Halima na Shabani wanamkaribisha kwa mikono miwili nyumbani kwao na kumhakikishia kuwa alikuwa katika mazingira salama na asingeshurutishwa kuolewa kinyume na mapenzi yake (uk. 25). Usawiri wa familia ya Shabani na mkewe, Bi. Halima, unathibitisha umuhimu wa kupalilia mazingira yenye vielelezo bora vinavyochangia kuigwa kwa tabia chanya.

Katika riwaya ya *Lulu ya Maisha* (2013) mwandishi anaonyesha jinsi watoto wa Tiito wanavyoathirika kutokana na tabia ya wazazi wao ya kulaumiana kwa kelele

kuhusu kukosekana kwa uaminifu katika ndoa yao. Sue anauelezea ugomvi huo kwa maneno yafuatayo:

> "Usiku tungemsikia baba na mama wakigombana, wote wakilaumiana. "Ni wewe,'' mama alimwambia kwa ukali…Hata kama baba alipona kiasi na kurudi kazini, mahusiano yake na mama yalikuwa ya tabu. Kuna wakati mama alimtisha kwamba angemwacha" (uk. 11).

Mzozo baina ya Tiito na mkewe unaathiri tabia ya watoto wake. Watoto wanamchukia baba yao kwa kumwona kama aliyechangia katika matatizo ya kiuchumi yanayoikumba familia yao. Hali hiyo inajitokeza kupitia usemi unaotolewa na Sue baada ya kifo cha baba yao:

> "…tulikuwa na hasira na baba na maisha kwa jumla."(uk. 14).

Aidha, chuki ya Sue dhidi ya baba yake pia inadhihirika kupitia maneno yafuatayo:

> "Nilihisi kumchukia baba sasa kwani niliona angesababisha kifo chake na hata cha mama mzazi."(uk. 13).

Mwandishi wa riwaya ya hii anadhihirisha kwamba kupigiana kelele hadharani na kufichua kunga za ndoa kwa watoto kunaweza kuwafanya watoto kumchukia mmoja wa wazazi na kudhihirisha hasira zao waziwazi kwa mzazi huyo. Maelezo ya mwandishi yanaoana na yale ya Hotton (2003) anayeeleza kuwa watoto wanaposhuhudia wazazi wakizozana hadharani huathiriwa kwa njia hasi na kwamba wanaweza kuiga tabia ya ukatili.

#### 4.1.1.2 Kuepuka adhabu kali wakati wa kuwarekebisha watoto

Maelezo ya mwandishi wa riwaya ya *Tumaini*, yanaashiria kwamba adhabu kali ya wazazi dhidi ya watoto huwa na madhara mbalimbali. Kwanza, husababisha usugu kwa baadhi ya watoto na kuwafanya kuwa katili maishani. Watoto hao huamua kutumia ukatili kama njia mojawapo ya kutatua mizozo yoyote inayowakumba. Hali kadhalika, baadhi ya watoto ambao ni wahanga wa adhabu kali wanapokuwa watu wazima, huonyesha ukatili dhidi ya aila na jamaa zao kama njia ya kulipiza kisasi kutokana na ukatili waliotendewa. Adhabu kali ambayo Mzee Masumbuko anaitumia katika kuwarudi watoto wake inakuwa chanzo cha ukatili anaoudhihirisha mwanawe, Idi. Masumbuko alikuwa na mazoea ya kuwatia watoto wake ndani ya gunia lenye jani la upupu na kuwachapa mpaka fimbo inakatika vipandevipande (uk. 28). Licha ya hayo, wakati mwingine mzee huyo aliwaadhibu watoto wake bila sababu au hata bila kuwaelezea sababu ya adhabu aliyowapasha. Tabia hiyo inaelezewa kupitia maneno ya Tumaini:

> "Siku moja Idi aliamshwa kwa mateke na magumi. Kisa na maana ni kuwa baba alitegwa na gunzi pale uani na kuanguka kifudifudi. Gunzi tu Ma Mdogo! Idi kapigwa wala hakujua kipigo hicho kilikuwa cha nini."(uk. 68).

Kitendo cha kuwaadhibu watoto bila sababu au bila kuwaelezea makosa yao kinakinzana na kanuni zinazohusu upashaji adhabu jinsi zinavyofafanuliwa na baadhi ya wataalamu (Webster-Stratton, 2001, Kenani, 2003, Mwenda, 2020). Wataalamu hawa wanafafanua kwamba mtoto anapaswa kuelezwa kwa ufupi na kwa njia wazi sababu ya adhabu ili aelewe na arekebishe tabia. Mtoto asipoelewa

vizuri sababu ya kuadhibiwa anaweza kuhalalisha matendo yake, kukuza tabia ya usugu na kuwa na hisia za chuki dhidi ya anayempasha adhabu. Mwandishi Momanyi (2006) anadhihirisha bayana kuwa ukatili ambao Masumbuko anauelekeza kwa watoto wake unatokana na adhabu kali ambayo yeye mwenyewe mara kwa mara alipashwa na baba yake alipokuwa mdogo. Maelezo yafuatayo yanaonyesha adhabu kali ambayo baba yake Masumbuko anampasha Masumbuko kwa sababu ya kususia chakula:

> “Baba yao hangeweza kustahimili hasira hizo za mwanawe. Alimsubiri hadi alipoenda kulala, kisha alimwamsha kwa kumchapa viboko mfululizo. Aliamrishwa kula chakula huku babake akifululiza kumchapa mpaka mamake akamwonea huruma. Masumbuko alitoja damu mwili mzima, viboko vikavunjikia mwilini mwake kimoja baada ya kingine.”(uk. 65).

Adhabu anayopaswa Masumbuko na mzazi wake ni kali mno na inayoumiza kisaikolojia kutokana na kitendo cha kumchapwa huku akishurutishwa kula chakula. Kitendo chenyewe kinakiuka kanuni mbalimbali zinazohusu upashaji adhabu (Mbaka, Gatumu & Tumuti, 2011). Wataalamu hawa wanaeleza kwamba adhabu inapaswa kulingana na kosa lililofanywa na kwamba adhabu zote zinazosababisha maumivu ya kisaikolojia zinapaswa kuepukwa. Momanyi (2006) anahitimisha kwamba ukatili alioudhihirisha Masumbuko dhidi ya watoto wake ulikuwa njia moja ya kulipiza kisasi kutokana na ukatili alioupitia mikononi mwa baba yake (uk. 65). Mwandishi huyu anaashiria kuwa matumizi ya adhabu kali dhidi ya watoto husababisha usugu na ukatili badala ya kurekebisha tabia jinsi inavyodhihirika kwa Masumbuko (uk. 66). Momanyi anaonyesha jinsi uimarishaji

chanya unaweza kuendeleza tabia njema kwa watoto waliokuziwa katika mazingira sawa. Analithibitisha jambo hili kupitia kwa kijana anayeitwa Sifa ambaye tabia yake inakinzana na ile ya Idi, mwanawe Mzee Masumbuko. Majaliwa, baba yake Sifa, anamtuza mwanawe baiskeli kwa kujitahidi masomoni (uk. 21). Kitendo hicho kinamfanya Sifa kutia bidii masomoni na kudumisha tabia njema (uk. 20). Isitoshe, himizo za baadhi ya wazazi kwa wanao zinachangia katika kuwaadilisha. Mwandishi anasimulia kuhusu Sifa na Yohana ambao walikuwa na tabia njema iliyotofautiana na ile ya ukatili ya Majuto na Kijungwe. Himizo za kila mara za wazazi wa Sifa na Yohana zilichangia katika kuendeleza tabia yao njema (uk. 21). Kupitia maelezo haya, mwandishi anaashiria kuwa inawezekana tabia ya ukatili miongoni mwa watoto ikakabiliwa kupitia upaliliaji wa mazingira mwafaka ambapo tabia njema inaweza kuendelezwa. Maelezo hayo yanaafikiana na mhimili wa nadharia ya ujifunzaji wa kijamii ya Bandura (1977) unaoeleza kwamba uimarishaji chanya unasaidia katika kuendeleza tabia inayokubalika katika jamii.

#### 4.1.1.3. Familia kuwa na watu vielelezo wanaokidhi mahitaji ya mtoto

Watu vielelezo katika familia na wanaokidhi mahitaji mbalimbali ya mtoto yakiwamo yale kisaikolojia watamsaidia mtoto kuiga tabia njema na kuepuka vitendo vya ukatili. Watu hawa wanajumuisha wazazi, walezi na jamaa wengine wenye uhusiano wa karibu na mtoto (Reese, Vera, Simon & Ikeda, 2000). Vanassche, Sodermans, Matthijs & Swicegood (2014) wanaeleza kuwa wazazi hutekeleza wajibu muhimu wa kuwashawishi na kuwaelekeza watoto kuiga tabia

inayokubalika katika jamii. Naye Morell (2006) anatambua umuhimu wa baba mzazi katika kukidhi mahitaji wa kisaikolojia ya mtoto na kuwa mfano wa kuigwa. Bugental, Corpuz & Schwartz, (2012) wanafafanua kuhusu wajibu wa mama katika kukidhi mahitaji mbalimbali ya mtoto na kumsaidia kuyaitikia mazingira yake kwa njia chanya. Wataalamu hawa wanaendelea kufafanua kuwa kukosekana au kutojihusisha kikamilifu kwa mama katika malezi ya mtoto kunaweza kuchangia msongo wa mawazo wa mtoto na kumfanya kuyaitikia mazingira kwa ukatili.

Waandishi wa vitabu teule vya fasihi ya watoto wanaonyesha jinsi baadhi ya watu wa familia walivyochangia katika kukuza tabia ya ukatili miongoni mwa watoto kwa kutokuwa vielelezo vyema vya kuigwa na kwa kutokidhi baadhi ya mahitaji muhimu ya watoto. Katika riwaya ya *Siku Njema*, mwandishi anaashiria kwamba tabia za wazazi wa Bakari yamkini ni sababu mojawapo inayomfanya kijana huyo kuanza kuwa katili katika umri mdogo. Baba yake Bakari, Mzee Salim, aliingilia sana unywaji wa pombe hivyo basi kuonekana nyumbani kwake kwa nadra; jambo ambalo linamnyima Bakari upendo wa baba mzazi (uk. 65). Naye Wamboi, mama yake Bakari, anaelezewa na mwandishi kwamba aliizorotesha tabia ya mtoto wao kwa kumpa chochote alichokitaka hata kama hakukihitaji katika umri huo mdogo (uk. 65). Mwenda (2020) anaelezea kuwa tabia ya wazazi kuwapa watoto vitu hata vile ambavyo hawavihitaji katika umri wao ili kuwafurahisha na kuepuka migogoro huiathiri tabia yao kwa njia hasi. Isitoshe, Bakari anapoachiliwa kutoka jela alipokuwa amefungwa kwa sababu ya wizi, hawapati

wazazi wake nyumbani. Mzee Salim alikuwa ametoweka asijulikane alikokwenda ilhali Wamboi alikuwa amerukwa na akili akawa anazururuka katika mji wa Mombasa akiokota vyakula jalalani. Kukosekana kwa wazazi wa Bakari wakati ambapo alikuwa ametoka jela na alihitaji kusaidiwa kihisia na kisaikolojia ili kuirekebisha tabia, kunaizorotesha zaidi tabia hiyo. Kijana huyo anaamua kwenda kuishi na marika zake anavyoeleza Rashid katika maneno yafuatayo:

> “Nikamwambia aje kuishi nami akadinda. Akanieleza yuaenda kustakimu na rafikize…’’ (uk. 65).

Kitendo cha Bakari cha kuamua kuishi na ‘rafikize’ kinatoa nafasi kwa rafikize kumwathiri zaidi kitabia. Hoja hii itafafanuliwa zaidi chini ya mkakati unaohusu kumkinga mtoto kutokana na ushawishi wa marika. Ujumbe muhimu anaoupitisha Walibora (1996) ni kwamba wazazi au watu wengine wenye uhusiano wa karibu na mtoto ni muhimu sana katika kumwadilisha mtoto kitabia. Mwandishi analithibitisha jambo hili kwa kutuonyesha mazingira mengine ambapo mzazi kielelezo anamsaidia mtoto kuiga tabia na mienendo inayokubalika katika jamii. Taswira hii inajitokeza kupitia kwa Zainabu Makame, mama yake Kongowea Mswahili. Zainabu anakuwa kielelezo chema cha kuigwa na mwanawe, Kongowea Mswahili, akiwa katika umri mdogo. Mzazi huyu anakaa karibu sana na mtoto wake na kumwonyesha upendo tangu siku ile alipozaliwa.

Mwandishi anauelezea wajibu wa Zainabu Makame katika kumlea mwanawe kupitia maneno ya Kongowea Mswahili:

> "Baada ya kunikopoa, mama akapunguza safari za mbali. Akawa yuaimba tu maadamu *Mbelewele* hawakwenda nje ya Tanzania au miji iliyo mbali na Tanga. Alitaka awe karibu na kitoto chake, akae nacho akichuchie, akipakate, akikoshe, akiase, akilishe – mradi alipania kukitunza kama afanyavyo ndege mzazi kwa kinda lake.''(uk. 3)

Kupitia kwenye dondoo hili, inabainika wazi kwamba Zainabu Makame anapunguza safari zake za kuendelea kukivumisha kipawa chake cha utunzi na uimbaji wa taarab ili kuwajibikia malezi ya Kongowea Mswahili. Kitendo cha Zainabu kuwajibikia malezi ya Kongowea Mswahili katika umri mdogo kinachangia tabia ya uadilifu anayoidhihirisha kijana huyo. Wajibu wa mzazi huyu katika malezi ya mwanawe unaeleweka zaidi kupitia ufafanuzi wa Bugental, Corpuz & Schwartz, (2012). Wataalamu hawa wanafafanua kuwa mama ni mhimili muhimu katika kukidhi mahitaji ya kihisia, kisaikolojia na ya kimwili ya mtoto na humfanya mtoto huyo kuyaitikia mazingira yake kwa njia inayofaa.

Hali kadhalika, katika riwaya hiyo ya *Siku Njema* Zainabu Makame anapokuwa mgonjwa, anaupitisha wajibu wa malezi ya Kongowea Mswahili kwa ndugu yake, Kitwana Makame. Jambo hilo linabainika kupitia maneno ya Kitwana kwa Kongowea Mswahili:

> "Alipokuwa akiugua dadangu…aliniachia dhima ya kukulea mpaka nikuoze mke. Huo ni wajibu nisioweza kuupuuza alaa kulihali, mpwa wangu.''(uk. 39).

Kitwana Makame anatoa mchango muhimu katika kuiendeleza tabia ya uadilifu ya Kongowea Mswahili ambayo tayari mama yake alikuwa ameiwekea msingi. Ujumbe anaoupitisha Walibora (1996) kupitia usawiri wa Bakari na Kongowea Mswahili ni kuwa watu wanaomzunguka mtoto katika familia hasa wazazi huelekeza aina ya tabia ambayo mtoto ataiga baadaye maishani. Wazazi wakiwa waadilifu na wanaowajibika ipasavyo kama vile Zainabu Makame, mtoto atakuwa na tabia njema. Kwa upande mwingine, wazazi wakiwa vielelezo vibaya kwa mtoto kama vile Mzee Salim na mkewe Wamboi, mtoto atajifunza tabia ya ukatili. Maelezo haya yanaafikiana na mhimili wa nadharia ya ujifunzaji wa kijamii unaosisitiza kuhusu umuhimu wa kuwapa watoto vielelezo bora vya kuigwa kama njia ya kuwafunza tabia njema.

Mwandishi wa riwaya ya *Lulu ya Maisha* anaonyesha jinsi Omido anavyogeuka katili kutokana na kusambaratika kwa familia yake na kushindwa kwa wazazi kukidhi mahitaji muhimu ya kijana huyo. Mwandishi anasimulia maisha ya Omido kabla ya wazazi wake kuanza kuugua ugonjwa wa ukimwi na kuyatofautisha na maisha baada ya wazazi kuanza kuugua ugonjwa huo. Kabla ya Tiito kuanza kuugua ukimwi, familia yake iliishi kwa furaha na amani kwa sababu Tiito aliweza kukidhi mahitaji mbalimbali ya familia. Maelezo ya Sue yanaakisi picha halisi ya familia hiyo:

> "Nyumba yetu haikukosa chakula. Daima vyakula vya aina yote vilikuwemo ndani ya jokofu letu; kubwa kweli kweli. Pia vyakula vingine kama vile njugu, mchele, unga la dona, ndizi, viazi na vinginevyo vilijaa kochokocho. Nyumba yetu ilikuwa kama ahera duniani."(uk. 7).

Isitoshe, Tiito ambaye alikuwa mwanajeshi alipopata nafasi ya kwenda nje ya nchi kwa shughuli za kikazi, alimletea mkewe na watoto zawadi za kila aina (uk. 2). Hali kadhalika, alihakikisha kwamba kila mmoja katika nyumba yake alikuwa na furaha wakati wowote alipokuwa nyumbani. Aliwatambia watoto wake hadithi za Alfu-Lela-Ulela ambazo licha ya kuwasisimua ziliwaadilisha (uk.2).

Vipimo vya dakatari vinapoonyesha kuwa Tiito alikuwa akiugua uwele wa ukimwi, furaha iliyotamalaki katika nyumba yake inatoweka. Sue anaielezea taswira hiyo mpya kwa maneno yafuatayo:

> "Jioni aliyorudi baba kutoka hospitalini, ungedhani mtu amekufa kwetu. Nyumba ambayo ilikuwa na furaha tele ilikuwa na kilio sasa…" (uk. 11).

Ugonjwa wa Tiito unaiathiri familia yake kiuchumi kwa sababu anahitaji matibabu ya mara kwa mara ili kupunguza makali ya maradhi. Maisha yanakuwa na changamoto zaidi Tiito anapostaafu kazi yake kwa kulemewa na maradhi. Kauli ya Sue inaakisi taswira hiyo:

> "Baada ya miaka miwili ya kuugua, baba alilazimika kustaafu. Matatizo yake ya afya yakatoboa kibofu chetu cha uchumi. Matatizo ya kiuchumi ambayo hatukuyazoea yakabisha hodi kwetu nyumbani."(uk. 11).

Hatimaye, Tiito anapoaga dunia, watoto wake hawaendelei na masomo tena. Mkewe anashindwa kumudu maisha ghali ya mtaa wa kifahari wa Onyonka na kustaabu kuhamia mtaa wa mabanda wa Kisera. Ami za watoto hawa ambao walitakiwa kujaza pengo la baba yao wanageuka mahayawani. Wanamnyang'anya mfaruku mali ambayo aliachiwa na mumewe na ambayo

yangekuwa urithi wa watoto (uk. 20). Kitendo cha ami kinachochea hisia za chuki katika mioyo ya watoto wa Tiito (uk. 21)). Unyakuzi wa mali ya mama yao hasa shamba la nyumbani ambalo Tiito alikuwa amelinunua, unamwathiri Omido zaidi kuliko anavyoathirika Sue (uk. 22). Habwe (2013) anaonyesha kuwa misukosuko ya familia inayoambatana na mabadiliko ya kitabia ya watu ambao wanapaswa kuwa vielelezo kwa watoto na kukidhi mahitaji yao muhimu wakati mwingine huathiri maisha ya watoto na kuwafanya kuwa katili. Mwandishi huyu anapendekeza wazazi waendelee kupaliliwa mazingira mwafaka yatakayowasaidia watoto kukua na tabia chanya. Morell (2006) na Bugental, Corpuz & Schwartz (2012) wanaeleza kuwa watu wanaowazunguka watoto na hasa wazazi hutekeleza wajibu muhimu katika kuwaadilisha watoto kupitia njia ya kukidhi mahitaji yao.

Katika riwaya ya *Tumaini*, mwandishi anaashiria kwamba mojawapo ya mambo yanayomwathiri Majuto kitabia na kumfanya kuwa katili ni malezi mabaya na kukosa mifano bora ya kuiga katika familia yake. Wazazi wa Majuto wanamlea mtoto wao kwa kumdekeza mno mpaka akapotoka kitabia inavyojitokeza katika maneno ya mtunzi yafuatayo:

> “Wazazi wake walimlea kwa tunu na raha lakini Majuto hakuyatambua.”(uk. 21)

Licha ya hayo, Andrea si kielelezo chema cha kuigwa na Majuto kutokana na tabia yake ya kuwadhulumu wasichana kimapenzi na kupokea hongo kutoka kwa wanakijiji (uk. 54). Mwanamume huyu alipenda kuwatongoza wasichana wadogo

walioajiriwa nyumbani kwake kwa kutumia zawadi ndogondogo kama chambo cha kuwanasia. Baada ya kuwaringa baadhi yao mimba, aliwafadhili kuavya na waliokataa akawatishia maisha. Isitoshe alichukua hongo kutoka kwa wanakijiji ili kuwatekelezea mambo fulani kwa kutumia cheo chake. Tabia ya Majuto ya kuwadhulumu kimapenzi mabinti wa watu yamkini amejifunza kwa baba yake (uk. 74) tabia hii yamkini ameiga kwa baba yake. Hali kadhalika, tabia ya Andrea ya kuwaibia wanakijiji kwa njia ya hongo inamwathiri Majuto ambaye anasawiriwa kama mwizi hodari. Momanyi (2006) anadhihirisha kwamba wazazi na walezi hutekeleza wajibu muhimu sana katika kukuza na kuelekeza tabia ya watoto. Analitilia jambo hili uzito kupitia kwa mtoto mwingine wa kiume anayeitwa Sifa. Licha ya kuwa kijana huyu anakulia katika mazingira sawa na Majuto, tabia zao zinakinzana. Tabia ya uadilifu ya Sifa imemsadia katika kupiga hatua kubwa katika masomo yake (uk. 110). Vanassche, Sodermans, Matthijs & Swicegood (2014) wanaeleza kuwa wazazi ni muhimu sana katika kuelekeza tabia ya watoto. Mhimili wa nadharia ya ujifunzaji kuhusu umuhimu wa vielelezo katika ujifunzaji wa tabia katika kiwango cha jamii umesaidia kuelewa sababu zinazosababisha mabadiliko ya kitabia kwa watoto waliolelewa katika mazingira sawa.

### 4.1.2 Kuyapunguza mambo yanayoweza kusababisha ukatili shuleni

Lengo la shule ni kutoa mafunzo kwa wanafunzi ili kukuza maarifa na ujuzi ambao utawasaidia kupata ajira, kuendeleza taaluma zao na kuchangia katika

ustawi wa jamii. Licha ya hayo, walimu na watu wengine ambao watoto hutagusana nao shuleni wanapaswa kuwafunza tabia ya uadilifu (Smith, 2003).

#### 4.1.2.1 Kuepuka adhabu kali na kutumia njia mbadala kushughulikia nidhamu

Kuepuka adhabu kali na zinazokiuka kanuni za upashaji adhabu na kutumia njia mbadala za kushughulikia visa vya utovu wa nidhamu shuleni ni njia nyingine inayoweza kutumiwa kudhibiti ukatili wa watoto. Katika riwaya ya *Tumaini,* tabia ya ukatili ya Majuto na Kijungwe inaendelea kuzorota licha ya mwalimu mkuu, Bwana Mwadime, na walimu wengine kutumia adhabu tofauti kuwarudi. Mojawapo ya mbinu wanazozitumia walimu hao kuwarekebisha vijana hao ni kuwafukuza shuleni kwa muda mfupi wakati wowote utundu wao ulipokithiri na kutishia usalama wa wengine. Mwandishi anaeleza kuwa kila wakati Majuto alifukuzwa shule kwa sababu ya utovu wa nidhamu lakini baba yake, Bwana Andrea, akamtetea huku akitumia cheo chake cha uchifu na Majuto akakubaliwa fursa nyingine tena (uk. 20). Mbinu nyingine wanayoitumia walimu ni kuwaadhibu vijana hao wakati wanafunzi wengine wanapoendelea kusoma. Wakati mmoja mwalimu anamlazimisha Majuto kupiga magoti mbele ya wanafunzi wakati somo lilipokuwa likiendelea na kumfukuzia nje ya darasa (uk.21). Kijungwe naye anakabidhiwa jembe na fyekeo na mwalimu wake na kushurutishwa kung’oa visiki kutoka asubuhi mpaka jioni wakati wenzake walipokuwa wakiendelea kusoma (uk 73). Fauka ya hayo, wazazi wa vijana hao wanalazimishwa kulipia gharama ya mali ya shule ambayo wanaiba na kuuza.

Adhabu hii haielekezwi moja kwa moja kwa vijana hao bali kwa wazazi wao. Mbinu hizi za upashaji adhabu hazifaulu katika kurekebisha ukatili wa vijana hao wawili yamkini kutokana na ukali wazo, zinakiuka baadhi ya kanuni zinazohusu upashaji adhabu na hazitilii maanani maslahi ya mtoto yanavyojitokeza katika ilani ya mwaka wa 2001 (Kimani, Kara & Ogetange, 2012). Wataalamu hawa wanaeleza kuwa serikali ya Kenya iliharamisha matumizi ya kiboko na mbinu nyingine za upashaji adhabu ambazo zilikiuka haki za mtoto. Mojawapo ya mbinu zinazokiuka haki ya mtoto ni kumpasha adhabu wakati wa masomo.

Katika riwaya ya *Tumaini*, mwalimu mkuu anapomwambia Majuto kupiga magoti mbele ya wanafunzi wenza somo linapoendelea na kumfukuzia nje ya darasa, adhabu hii ni kali na inakiuka haki ya kijana huyo ya kunufaika kutokana na yale ambayo wengine walikuwa wakisoma. Yamkini jambo hilo ndilo linalomfanya Majuto kuiitikia adhabu hiyo kwa ukatili kwa kumtupia mwalimu wake mawe (uk. 21). Isitoshe, Majuto anakiona kitendo cha kushurutishwa kupiga magoti mbele ya wenzake kama kinachodhamiriwa kumdunisha na kumshushia kiwango cha kujithamini. Aidha, adhabu ya Kijungwe ya kung’oa visiki wakati wengine wanaendelea kusoma ni kali na inayokiuka haki ya kijana huyo. Vile vile, adhabu hiyo inagubikwa na utata mwingine kwa sababu Kijungwe anaadhibiwa kwa kosa tofauti kabisa na lile alilolitenda. Mwandishi anaeleza kwamba Kijungwe alikuwa anamdhihaki Tumaini jambo ambalo lilimkasirisha Tumaini ambaye alimtupia Kijungwe jiwe ambalo liliishia kumjeruhi mwalimu kichwani (uk.20). Tumaini

anapomsingizia Kijungwe kwamba ndiye aliyerusha jiwe, .mwalimu hampi Kijungwe nafasi ya kujitetea kutokana na historia yake ya utovu wa nidhamu.

Anamwelekeza ofisini mwake ambapo anamkemea vikali, anamkabidhi jembe na upanga na kumwamuru kung'oa visiki. Adhabu hii inakiuka mojawapo ya kanuni zinazohusu upashaji wa adhabu zinazoeleza kwamba sharti mwalimu amweleze mtoto kinaganaga na kwa njia ya wazi na anayoweza kuielewa sababu ya kumpasha adhabu (Kenani, 2003). Mtaalamu huyu anaeleza kuwa mtoto asipoelewa sababu ya kuadhibiwa anaweza kugeuka sugu kwa kuirudia tabia ile ile. Jambo hili pia linalotokea wakati wazazi wa Majuto na Kijungwe wanaadhibiwa kwa niaba ya watoto wao kwa kushurutishwa kulipia gharama ya bidhaa walizokuwa wameziba. Mwandishi anaeleza kwamba hata baada ya tukio hilo la wizi, vijana hao walizidisha ukatili wao ambao ulitishia maisha ya wanafunzi wengine (uk. 20). Kukithiri kwa tabia ya Majuto na Kijungwe kunatokana na kule kutoelewa kinaganaga sababu ya adhabu iliyotolewa jinsi anavyofafanua Kenani (2011).

Matumizi ya adhabu tofauti kwa makosa yale yale au yenye uzito sawa ni jambo jingine linaloashiriwa na mwandishi wa riwaya ya *Tumaini* kuwa linachangia katika kutofaulu kwa adhabu katika kurekebisha tabia ya vijana husika. Kuna adhabu ya kuwafukuza shuleni kwa muda fulani na kurejeshwa baada ya ushawishi wa mzazi. Katika mazingira mengine, wanapashwa adhabu wakati wengine wanaendelea kusoma. Adhabu hizi zinakosa uthabiti (consistency)

anavyofafanua Kenani (2011). Mtafiti huyu anaeleza kuwa matumizi ya adhabu mbalimbali kwa kosa lile lile au makosa yenye uzito sawa wakati mwingine humfanya mtoto kukanganyikiwa hivyo basi kutobadili tabia yake. Mwandishi Momanyi (2006) anapitisha ujumbe kwamba adhabu inaweza kuleta matokeo chanya iwapo itakuwa kiasi, inayoelezea kinaganaga kosa linalostahili adhabu na isiyokiuka haki za mtoto. Adhabu iliyokiuka mambo haya huenda ikazorotesha uhusiano baina ya mwalimu na mwanafunzi na kuifanya tabia ya mwanafunzi kuzorota zaidi badala ya kuimarika. Mwandishi huyu anachora taswira nyigine ambapo adhabu kiasi inafaulu katika kuzuia tabia hasi na kuleta matokeo chanya. Kwa mfano, Sifa anapomwandikia Tumaini barua ya mapenzi yenye ujumbe ambao unamwudhi Tumaini, Bwana Mwadime anamwita Sifa ofisini mwake na kumpatia adhabu ya kufagia madarasa yote ya shule. Baadaye, anamwamuru kumwomba Tumaini msamaha mbele yake (uk. 45). Matokeo chanya ya adhabu hii katika kurekebisha tabia ya Sifa yanaelezewa kwa maneno yafuatayo:

> “Tokea wakati huo, Sifa alikuwa akimtazama Tumaini kwa jicho jingine kabisa. Alimheshimu, na kamwe hakutaka kutamka neno lolote baya kwake.”(uk. 45).

Ushauri wa mwandishi unaojitokeza kupitia adhabu hii unaafikiana na maelezo ya Kenani (2003) kuwa, ili adhabu ifaulu katika kurekebisha tabia sharti iwe kiasi na isisitize kuhusu tabia hasi inayokosolewa bali isilenge kuumiza hisia za anayekosolewa. Maelezo ya mtafiti huyu na yale ya mwandishi wa *Tumaini* kuhusu adhabu yanakubaliana na mhimili wa nadharia ya ujifunzaji unaoelezea

kuhusu umuhimu wa uimarishaji chanya katika kuendeleza tabia inayokubalika ya mtoto.

Suala la adhabu kali pia linajitokeza katika riwaya ya *Siku Njema*. Selemani Mapunda anashurutishwa na mwalimu mkuu kuvua nguo na kuoga hadharani (uk. 20). Mchakato mzima wa upashaji wa adhabu una kasoro ambazo zinamwathiri Mapunda kisaikolojia na kumfanya kutoroka shule na kugeuka katili. Mwalimu mkuu anawatumia vigoli kumwandalia Selemani maji ya kuoga kwenye karai kisha analikuza tukio lenyewe kwa kuita paredi ya ghafla; jambo ambalo halikuwa limezoelewa mle shuleni. Isitoshe, kitendo cha mwalimu mkuu kumpokeza Selemani Mapunda sabuni na kumwamuru kuvua nguo na kuoga mbele ya wenzake kinamtia kijana huyo woga, shauku na aibu inavyojitokeza katika maelezo ya Kongowea Mswahili yafuatayo:

> "Selemani alitaka ardhi ipasuke na kumzika mzima aepuke aibu iliyomkabili. Akalivua shati. Tukaangua cheko kubwa la dhihaka. Akautazama umati kwa jicho la hasama. Kisha akauona upenu na kukimbia mbio ambazo hazina mfano wake, shati kaliacha nyuma."(uk. 20)

Mbaka, Gatumu na Tumuti (2011) wanawashauri wanaowapasha watoto adhabu kuepuka adhabu kali na zinazoumiza saikolojia ya mtoto. Adhabu hizo zinaweza kumfanya mtoto kuingiwa na woga, shauku, msongo wa mawazo na kushusha kiwango chake cha kujithamini hivyo basi kutorekebisha tabia. Mbali na hayo, adhabu kali huwafanya watoto kudhihirisha ukatili shuleni na katika jamii kwa jumla kama njia ya kulipiza kisasi (Kenani, 2011; Humphreys, 2008; Mbaka,

Gatumu na Tumuti, 2011). Jambo hili linadhihirika bayana Selamani Mapunda anapoudhihirisha ukatili kwa mwalimu mkuu wa Tanga (uk.21). Hali kadhalika, kijana huyu anaonyeshwa na mwandishi akitekeleza matendo ya kikatili dhidi ya wanajamii wengine (uk. 20). Kupitia maelezo haya, Walibora (1996) anaashiria kuwa kuna haja ya walimu kuchagua kwa makini mbinu wanazozitumia kurekebisha utovu wa nidhamu shuleni ili kuepuka kuzidisha ukatili miongoni mwa watoto. Maelezo haya yanakubaliana na mhimili wa nadharia ya ujifunzaji wa kijamii kuhusu uimarishaji tabia kama njia moja ya watoto kujifunza tabia.

#### 4.1.2.2 Kubuni njia mwafaka za kushughulikia utovu wa nidhamu

Kubuniwa kwa mbinu mwafaka za kushughulikia visa vya utovu wa nidhamu shuleni kwa kuwahusisha wadau wote ni mkakati mwingine unaoweza kusaidia kudhibiti ukatili miongoni mwa watoto. Mwandishi wa riwaya ya *Tumaini* anaonyesha kwamba mojawapo ya mambo yanayochangia upotofu wa tabia ya baadhi ya wanafunzi wa Kivulini ni kukosekana kwa mikakati mwafaka ya kuirekebisha tabia yao. Mwandishi analidhihirisha jambo hili kupitia kwa mhusika Majuto. Mwalimu mkuu, Bwana Mwadime, hawashirikishi kikamilifu walimu wake katika kuibuka na mbinu mwafaka za kushughulikia utovu wa nidhamu shuleni. Baadhi ya walimu wanastahabu kutumia adhabu ambazo wanachukulia kuwa zitasaidia kuzuia tabia hasi. Matokeo ya jambo hilo ni kuwafanya wanafunzi kukanganyikiwa na kudhihirisha ukatili zaidi inavyojidhihirisha kupitia kwa Majuto. Kwa sababu ya kukosekana kwa ushirikiano na mashauriano baina ya Bwana Mwadime na walimu wake jinsi ya

kushughulikia nidhamu shuleni, mzigo mkubwa wa kushughulikia visa mbalimbali vya utovu wa nidhamu shuleni unamwangukia mwalimu huyo mkuu inavyoelezewa na mtunzi:

> "Majuto na Kijungwe…walikuwa na ukaidi uliomsumbua sana mwalimu mkuu, Bwana Mwadime.''(uk. 20)

Anachopendekeza Momanyi kupitia kauli hii ni kuwa usimamizi wa shule unapaswa kuwa na utaratibu maalumu wa kushughulikia utovu wa nidhamu ili wajibu huo usije ukawa ni wa wakuu wa shule pekee. Pengo jingine linalodhihirika katika shule ya Kivulini ni kutohusishwa kwa wazazi katika kushughulikia nidhamu ya watoto wao. Mara kwa mara, Bwana Mwadime anashurutika kumfukuza Majuto nyumbani kwa muda fulani pale ambapo mapepe na utundu wake unakithiri (uk. 20). Hata hivyo, hawahusishi wazazi ili kulikabili tatizo hilo pamoja. Jambo hilo linatoa mwanya wa kuendelea kukithiri kwa tabia ya watoto hao. Singh & Steyn (2013) wanaeleza kuwa wazazi ni sehemu muhimu katika mfumo wa shule na huwasaidia wakuu wa shule na walimu katika kupunguza visa vya utovu wa nidhamu shuleni kwa kujihusisha katika masomo na maendeleo ya watoto wao shuleni. Watafiti hawa wanafafanua kuwa wazazi wasipotekeleza wajibu huu, watapalilia mazingira ya kutokea kwa ukatili miongoni mwa watoto.

Shinikizo na vishawishi vingine vya wazazi na wanajamii wengine vinavyoelekezwa kwa walimu na usimamizi wa shule ni jambo jingine linaloashiriwa na mwandishi wa riwaya ya *Tumaini* kwamba linaathiri

kushughulikiwa kikamilifu kwa utovu wa nidhamu shuleni. Mara kwa mara, Bwana Mwadime anasawiriwa kutiliwa shinikizo na Bwana Andrea ambaye ni chifu kumrudisha Majuto shuleni (uk. 20). Katika baadhi ya mazingira, Mwadime anashawishiwa na chifu huyo kwa kupewa hongo ili kumrudisha kijana huyo shuleni. Jambo hili linajitokeza bayana wakati Majuto na Kijungwe wanahusika katika uvunjaji wa ofisi na wizi wa madaftari.

> "Kutokana na juhudi za chifu, akina Majuto hawakufukuzwa shule. Hata hivyo, vinywa vya watu mitaani vilieneza uvumi kuwa Mwalimu Mwadime alipokea mlungula."(uk. 20).

Momanyi (2006) anaashiria kuwa shinikizo za wazazi na watu wengine wenye ushawishi katika jamii zinaweza kuathiri kushughulikiwa kwa visa vya utovu wa nidhamu shuleni kwa ukamilifu. Aidha, jinsi visa vya utovu wa nidhamu vinavyoshughulikiwa katika kiwango cha darasa kunaashiriwa na mwandishi wa riwaya ya *Tumaini* kama pengo jingine katika kukabiliana na utovu wa nidhamu mapema katika maisha ya mtoto. Wanafunzi wanaporipoti kuhusu wizi wa nyenzo zao, mwalimu wa darasa la akina Majuto halimakinikii suala hilo na kufuatilia ili kung'amua ni mwanafunzi gani aliyekuwa ameanza kuwa na mkono mrefu ili amrekebishe. Jambo hilo linafanya tabia ya Majuto kuendelea kikithiri zaidi inavyoelezewa hapa:

> "Wizi ule wa darasani sasa ulikita mizizi na kumfanya Majuto kuhitimu na kuwa mwizi mtajika.''(uk. 71).

Kenani (2011) anashauri kuhusu umuhimu wa mwalimu wa darasa kulidhibiti darasa vyema na kudumisha nidhamu darasani kama njia moja ya kuruhusu

shughuli za masomo kufanikiwa na kuzuia ukatili miongoni mwa watoto. Mtaalamu huyu anafafanua kuwa visa vya utovu wa nidhamu vinapotokea darasani, ni wajibu wa mwalimu wa darasa kuvishughulikia kwa njia ambayo inatilia manani maslahi ya wanafunzi wanaohusika.

Katika riwaya ya *Siku Njema*, mwandishi anasimulia kuhusu wanafunzi wenye utovu wa nidhamu katika darasa la Kongowea Mswahili na ambao wanadhihirisha ukatili kwa Kongowea Mswahili. Kila wakati Kongowea Mswahili alipowashinda wanafunzi hao masomoni walisikika wakingengemeka hadharani na kumuumbua kwa matusi (uk. 8). Aidha, mwandishi anasawiri picha ya ukosefu wa mazingira bora darasani ambayo ni muhimu katika kukuza tabia ya kusema ukweli na kujiamini miongoni mwa watoto. Kwa mfano, Selemani Mapunda anasawiriwa akinakili majibu ya Kongowea Mswahili wakati wa mtihani – jambo ambalo linaonyesha ukosefu wa uaminifu (uk. 8).

Kutoshughulikiwa kwa visa vya utovu wa nidhamu darasani jinsi ambavyo kunadhihirika katika riwaya ya *Tumaini* na *Siku Njema* kunaonyesha udhaifu wa walimu husika katika kulidhibiti darasa anavyofafanua Kenani (2011). Kwa hivyo, waandishi wa riwaya husika wanapendekeza kwamba usimamizi wa shule unapaswa kuibuka na mikakati kabambe ya kuvidhibiti visa vya utovu wa nidhamu darasani na shuleni na kupalilia mazingira bora ya wanafunzi kujifunza tabia njema.

Kubuni idara ya ushauri nasaha shuleni ili kuwashauri wanafunzi na kushughulikia visa vya utovu wa nidhamu ni mkakati mwingine unaoweza kusaidia kudhibiti tabia ya ukatili miongoni mwa watoto. Katika riwaya ya *Lulu ya Maisha*, mwandishi anachora taswira ambapo baadhi ya mikakati iliyowekwa na shule ya St. Mary's Girls Primary Boarding imesaidia katika kupunguza matendo ya ukatili shuleni humo. Idara hiyo inawapa ushauri nasaha watoto waliotoka katika jamii zilizosheheni ukatili ili kuwasaidia kujirekebisha. Mfano wa watoto hao ni Leila ambaye mama yake anamtupa njiani baada ya kumzaa (uk. 71). Kuwepo kwa idara hiyo ya ushauri nasaha shuleni humo kunajitokeza kupitia maneno ya Sue:

> "Licha ya kupewa ushauri wa shule na mshauri kila mara, nilionekana sikuhitaji sana ushauri huo…" (uk. 72).

Maoni ya Habwe (2013) kuhusu kubuniwa kwa idara za kutoa ushauri nasaha kwa wanafunzi kama njia moja ya kukabiliana na ukatili miongoni mwa watoto yanakubaliana na maoni ya Kindiki (2009) ambaye anapendekeza kutumiwa kwa njia mbadala za kuimarisha nidhamu shuleni kama vile kutumia idara za ushauri nasaha.

#### 4.1.2.3 Kuandaa shughuli za masomo ambazo zinakidhi mahitaji ya wanafunzi wote

Ujumuishaji wa shughuli za ujifunzaji kwenye masomo na ambazo zinakidhi mahitaji ya wanafunzi tofauti ni njia nyingine inayopendekezwa na baadhi ya waandishi wa vitabu teule vya fashihi kwamba inaweza kutumiwa kudhibiti visa

vya ukatili miongoni mwa watoto. Mwandishi wa riwaya ya *Tumaini* anawasawiri walimu wa shule ya Kivulini ambao wanachochea chuki katika mioyo ya wanafunzi yamkini kwa kutoandaa vipindi vyao vyema huku wakizingatia mahitaji ya kila mwanafunzi. Kauli anayoitoa Almasi, mmoja wa wanafunzi wa shule ya Kivulini, inaonyesha chuki yake dhidi ya mwalimu wa somo la Hisabati:

> "Wacha hilo somo lenyewe, hata mwalimu mwenyewe anayefunza ninamchukia pia.''(uk. 73).

Sababu inayomfanya Almasi kumchukia mwalimu wa somo la Hisabati ni mazoea ya mwalimu mwenyewe kuchora sufuri zenye macho, masikio na midomo kwenye kitabu chake kila wakati anapofeli somo hilo. Kitendo hiki kinahujumu jitihada za mwanafunzi huyo katika somo hilo na badala yake kuibua hisia za chuki. Anachopendekeza Momanyi (2006) ni kuwa kuna haja ya walimu kujiandaa vyema kwa vipindi vyao huku wakiibuka na mbinu mwafaka za kuwatia motisha wanafunzi ili kuborehsa matokeo yao na kupalilia uhusiano nao kama njia moja ya kuepuka uhasama na tabia ya ukatili. Kenani (2011) anaeleza kwamba mwalimu anayejali maslahi ya wanafunzi wake sharti aelewe silika zao, mazingira ya familia walimokulia, mambo ambayo wamewahi kupitia katika siku za awali na viwango vyao vya weledi miongoni mwa mengine. Jambo hili litamsaidia mwalimu kuibuka na shughuli za ujifunzaji ambazo zinakidhi mahitaji haya ya mwanafunzi.

### 4.1.2.4. Kudhibiti Ushawishi wa Marika

Kudhibiti ushawishi unaoweza kusababishwa na marika katika mazingira ya shule ni mkakati mwingine unaopendekezwa na waandishi wa vitabu teule vya fasihi ya watoto kwamba unaweza kutumiwa kupunguza visa vya ukatili. Katika riwaya ya *Siku Njema* mwandishi anawasawiri watoto ambao wanaendeleza tabia ya ukatili wakiwa katika marika. Kongowea Mswahili anaeleza jinsi wanafunzi hao wanavyochocheana na kumrushia cheche za matusi wakati wowote alipowashinda masomoni (uk. 8). Wanafunzi hawa wanaongozwa na Selemani Mapunda ambaye anaelezewa na mwandishi kwamba anatoka kwenye jamii iliyosheheni ukatili. Kupitia usawiri wa Selemani Mapunda, mwandishi anaashiria kwamba lau tabia yake ya ukatili ingetambuliwa mapema na kushughulikiwa isingefikia kiwango cha kuwaathiri baadhi ya wanafunzi wa shule ya Tanga. Usimamizi wa shule unaingilia kati kuikosoa tabia ya kijana huyo wakati ambapo amepotoka na kuacha taathira kwa wanafunzi wengine (uk. 20).

Mwandishi wa riwaya ya *Tumaini*, pia anasimulia jinsi ukatili wa watoto unavyochochewa na kuendelezwa na marika shuleni. Anasimulia kuhusu Majuto na Kijungwe ambao wanashirikiana katika kuihangaisha shule nzima (uk. 20). Majuto na Kijungwe wanashirikiana katika kuvunja ofisi ya mwalimu mkuu na kuiba madaftari ambayo wanayauza kwa mfanyabiashara anayeitwa Karim. Vilevile, wanashirikiana katika kuwafanyia wanafunzi wenzao mizaha hasa waliowashinda masomoni (uk. 44). Isitoshe, wanashirikiana katika wizi na ujambazi baada ya wote kuacha shule. Ingawa Majuto na Kijungwe

wanashirikiana katika kutekeleza matendo ya kikatili, kuna mambo mbalimbali yanayodhihirisha kuwa aliyekuwa na ushawishi mwingi katika ushirika huu ni Majuto. Mojawapo ya mambo hayo ni kwamba Majuto anapotimuliwa shuleni kwa sababu ya kumrushia mwalimu mawe, haupiti muda mwingi kabla ya Kijungwe naye kuacha shule na kujiunga naye katika kuendeleza matendo ya ukatili nje ya shule. Majuto anapofukuzwa shule, tayari anaacha athari hasi kwa baadhi ya wanafunzi akiwamo Juma na Kijungwe (uk. 44). Wanafunzi hawa wanaelezewa kuwa wenye ushari unaowasumbua wenzao. Isitoshe, katika riwaya hii, baadhi ya wasichana wa shule ya Kivulini wakiwamo Waridi na Almasi wanachocheana kuwachukia walimu wa masomo ya sayansi kwa sababu ya kutofaulu kwao katika masomo yenyewe. Wanachukulia kutofaulu kwao katika masomo hayo ni kosa la walimu husika bali si kosa lao (uk. 73)

Katika riwaya ya *Lulu ya Maisha*, mwandishi anawaangazia wanafunzi wa shule ya St. Mary's Girls Primary Boarding ambao wanaendeleza matendo ya ukatili wakiwa kwenye makundi. Sue anapojiunga na shule hii, wanafunzi hawa wanamdhalilisha kwa kumwambia kuimba kidogo, kulia kidogo na kuwarejelea viranja wao kwa jina 'Waheshimiwa' (uk. 71).Waandishi wa riwaya tatu zilizorejelewa wanawashauri walimu na usimamizi wa shule kwa jumla kwamba tabia ya ukatili miongoni mwa watoto inaweza kudhibitiwa kwa kuwatambua na kuwashughulikia wanafunzi wenye kasoro za kitabia na kuzirekebisha kabla ya kuzieneza tabia hizo kwa wenzao kwenye marika na kufanya mzunguko wa tabia ya ukatili. Mawazo ya waandishi kuhusu kushughulikia tabia ya marika mapema

yanaafikiana na yale ya Webster-Stratton & Taylor, (2001). Wataalamu hawa wanaeleza kwamba ni wajibu wa walimu kuwatambua mapema wanafunzi wanaoingia shuleni na tabia ya ukatili na kuibuka na mbinu mwafaka za kuishughulikia tabia hiyo kabla ya watoto hao kutengeneza magenge yanayoweza kuchochea matendo ya uasi shuleni. Mwandishi wa *Siku Njema* anaonyesha athari inayotokana na kutoshughulikiwa mapema kwa matendo ya ukatili kupitia kwa Selemani Mapunda. Usimamizi wa shule unaanza kuishughulikia tabia ya Selamani Mapunda katika darasa la sita – wakati ambapo tayari Mapunda ameacha athari ya ukatili katika maisha ya baadhi ya wanafunzi wa shule ya Tanga. Yeye mwenyewe anakuwa mfano wa samaki ambaye anakunjwa akiwa amekauka. Hali hiyo ndiyo inayojitokeza kupitia mhusika Majuto wa riwaya ya Tumaini ambaye juhudi za kumkunja akiwa amekomaa zinakosa kuzaa matunda. Bandura (1977) anaonyesha athari inayosababishwa na marika kupitia uigaji wa tabia hasi.

### 4.1.3 Kuyapunguza mambo yanayoweza kusababisha ukatili katika jamii

Sehemu hii itaangazia mambo mbalimbali ambayo yanaweza kusababisha tabia ya ukatili miongoni mwa watoto na ambayo jamii inapaswa kuyapunguza. Mambo haya yanajumuisha watu wazima wanaoweza kuwachochea watoto kuiga na kuendeleza tabia ya ukatili (Perry, Perry, & Boldizar, 1991).

#### 4.1.3.1 Kuwakanya watu wanaowapotosha watoto

Watu wazima ambao ni mfano mbaya wa kuigwa na watoto na wanaovihalalisha vitendo vya ukatili wa watoto wanaashiriwa na waandishi wa vitabu teule vya fasihi ya watoto kama wanaochangia ukatili miongoni mwa watoto. Katika riwaya ya *Tumaini*, mfanyabiashara anayeitwa Karim ananunua madaftari ambayo Majuto na Kijungwe wanaiba kutoka shuleni (uk. 20). Kitendo hicho cha kununua bidhaa zilizoibwa kutoka kwa watoto kinahalalisha tabia yao ya ukatili hivyo basi kumfanya Bwana Karim kuwa mfano mbaya wa kuigwa nao. Baadaye, ukatili wa vijana hawa unakuwa na athari hasi hata kwa Karim mwenyewe wanapovamia duka lake, kumjeruhi mkewe na kuiba kisanduku cha vito (uk. 109).

Katika riwaya hiyo, Bwana Andrea ni mfano mbaya wa kuigwa na vijana kutokana na tabia yake ya kuwadhulumu wasichana wadogo kimapenzi (uk. 54). Tabia hiyo inawaathiri baadhi ya vijana mtaani akiwamo mwanawe mwenyewe anayeitwa Majuto. Kijana huyo anasawiriwa kuwa mbakaji na mwizi hodari (uk.71). Momanyi (2006) anaonyesha udhaifu wa vyombo vya dola na asasi nyingine za jamii katika kufichua na kukabiliana na matendo ya watu hawa wanaochochea ukatili miongoni mwa watoto. Kwa mfano, Bwana Karim hachukuliwi hatua yoyote ya kisheria licha ya kujulikana kwamba ndiye aliyenunua bidhaa zilizoibwa kutoka kwenye shule ya Kivulini. Vilevile, usimamizi wa shule kupitia kwa Bwana Mwadime hauripoti wizi unaotendeka shuleni kwa vyombo vya usalama – jambo linalochangia kutochukuliwa kwa hatua mwafaka.

Fauka ya hayo, Chifu Andrea anakuwa kikwazo katika kutekelezwa kikamilifu kwa sheria. Kuna tetesi kwamba alimhonga Bwana Mwadime ili asiwafukuze Majuto na Kijungwe kutoka shuleni baada ya tukio la wizi. Licha ya hayo, mwandishi anaeleza kuwa wakati wowote wazazi wa wasichana waliodhulumiwa kimapenzi na Majuto walipopeleka malalamishi yao kwa Chifu Andrea, aliwapuuza. Wazazi hao walipomshtaki Majuto, chifu aliwahonga mawakili na mahakimu wakatupilia mbali kesi ya Majuto (uk. 54). Tabia ya Andrea ya kuzuia kutekelezwa kwa sheria inatoa mchango muhimu katika kudorora kwa tabia ya Majuto na vijana wengine ambao walishirikiana naye katika kutekeleza uhalifu. Bwana Karim, Bwana Mwadime na Chifu Andrea wanachangia katika kukithiri kwa matendo ya Majuto na Kijungwe kwa kuwa mfano mbaya wa kuigwa na kuhujumu kutekelezwa kwa sheria kikamilifu. Momanyi (2006) anaashiria kwamba kuna haja ya watu wazima kuwa vielelezo vya kuigwa na watoto kama njia moja ya kuwasaidia kuiga tabia bora. Aidha, mwandishi anapendekeza kwamba jamii kupitia vyombo vya serikali na asasi nyingine inapaswa kuwakabili watu fulani katika mazingira ya mtoto ambao wanaweza kuchangia tabia ya ukatili. Mawazo ya mwandishi yanakubaliana na yale ya Perry, Perry, & Boldizar (1991) ambao wanaeleza kuwa mara nyingi watoto huiga matendo ya watu wazima wanaowazunguka kwa kuwachukulia watu hao kuwa vielelezo. Mhimili wa nadharia ya ujifunzaji wa kijamii ya Bandura (1977) kuhusu umuhimu wa vielelezo katika mazingira ya watoto umesaidia katika kuyaelewa vyema mawazo ya wataalamu hao.

#### 4.1.3.2. Kudhibiti ushawishi wa marika katika kiwango cha jamii

Kuwalinda watoto dhidi ya ushawishi wa marika katika jamii ni njia nyingine inayoweza kusaidia katika kukabiliana na tabia ya ukatili miongoni mwa watoto. Lindenberg & Steglich (2010) wanaeleza kuwa marika huchangia katika ujifunzaji wa tabia kwa njia mbili. Kwanza, wanaojiunga na marika hayo hujikuta wakiiga tabia chanya au hasi kutoka kwa wenzao wenye ushawishi. Aidha, watu fulani katika marika wenye tabia fulani huwa vielelezo vya kuigwa hivyo basi huishia kubadili tabia ya wale wanaojiunga na makundi haya. Mwandishi wa *Siku Njema* anaonyesha mchango wa magenge katika kuendeleza tabia ya ukatili ya Selemani Mapunda na Bakari Salim. Selemani Mapunda anaelezewa kwamba alijiunga na genge la vijana wengine waliozuumu kutenda kila amali mbaya (uk. 20). Katika genge hili, mwandishi anaeleza kuwa Mapunda anajifunza tabia mpya ambazo hakuwa nazo alipokuwa shuleni. Anaanza kuvuta bangi, kuiba mali ya watu na kuwabaka mabinti wa watu (uk. 20). Licha ya Mapunda, kuna Bakari, mwanawe Salim Makame ambaye anaelezewa kuwa baada ya kutoka jela alipokuwa amefungwa kwa wizi anahiari kwenda kuishi na ‘rafikize’ (uk. 64). Mmoja wa vijana ambao Bakari anaenda kuishi nao ni Selemani Mapunda. Bakari anajitosa katika tabia ya kuvuta bangi na kunyakua vitu vya wapita njia .Baadaye, genge la Bakari linaanza kuwindwa na polisi kwa sababu ya kuwahangaisha wakazi wa Mombasa (uk. 113). Hatima ya Bakari na Selemani Mapunda inakuwa ni kupigwa risasi baada ya kufumwa wakijaribu kuiba gari jijini Mombasa (uk. 131).

Katika riwaya ya *Tumaini*, tabia ya Majuto na Kijungwe inakithiri kutokana na ushawishi wa marika. Mwandishi anaeleza kuwa Majuto, Kijungwe na wengine walihamia mtaa wa Mkwajuni na kuishi katika madanguro. Ushawishi hasi wa genge la akina Majuto kwa watoto wengine wa mtaa unadhihirika kupitia kauli ya mtunzi:

> "Katika madanguro hayo, vigoli kutoka mtaani humo waliwatembelea na kuzifuja pesa zao pamoja na ngawira nyiginezo, huku wakijiingiza katika tafrija mbalimbali."(uk111).

Katika riwaya ya *Lulu ya Maisha*, tabia ya Omido inabadilika anapojiunga na genge la marika katika mtaa wa Kisera. Katika genge hili, Omido anawaibia watu na kujinunulia vitu vya bei ghali kama vile mavazi, saa na redio kubwa (uk. 46). Aidha, Omido anajifunza tabia mpya ambazo hakuwa nazo akiwa kwenye genge hili. Anaanza kuvuta sigara, bangi na kutumia dawa ya kokeini (uk. 47. Waandishi wa riwaya tatu teule za fasihi ya watoto, wanaashiria kwamba ushawishi wa marika unaweza kuwa na athari hasi kwa watoto. Kwa hivyo, ni jukumu la wazazi, walezi na watu wengine wanaowajibikia malezi ya mtoto kuhakikisha kuwa ushawishi wa marika anayojiunga nayo mtoto hauchangia tabia ya ukatili. Hoja hii inaungwa mkono na Farrell, Thompson & Mehari (2016) ambao wanashauri kuwa jamii inapaswa kuelekeza juhudi nyingi katika kuhimiza tabia za uadilifu zinazopaswa kuigwa na watoto wakiwa kwenye marika kama njia moja ya kupunguza mambo ambayo yanaweza kuchangia upotofu wa tabia badala ya kuwazuia watoto kujiunga na marika.

#### 4.1.4 Hitimisho

Sura hii ilichanganua mikakati mbalimbali inayoweza kutumiwa kuikabili tabia ya ukatili miongoni mwa watoto katika familia, shule na jamii kwa jumla. Kudhibiti dhuluma za kinyumbani, kuepuka adhabu kali wakati wa kuwarudi watoto na kuwa na watu vielelezo wanaokidhi mahitaji ya watoto ni baadhi ya mikakati inayoweza kutumiwa katika familia kuikabili tabia ya ukatili miongoni mwa watoto. Shuleni, tabia hiyo inaweza kukabiliwa kwa kutumia njia mbadala kushughulikia nidhamu na kuepuka adhabu kali zinazokiuka haki za watoto na kuandaa shughuli za masomo zinazokidhi mahitaji ya wanafunzi wote miongoni mwa mbinu nyingine. Kuwakanya watu wenye ushawishi hasi kwa watoto na kudhibiti ushawishi wa marika ni baadhi ya mikakati inayoweza kutumiwa katika jamii kukabili tabia ya ukatili miongoni mwa watoto. Mihimili miwili ya nadharia ya ujifunzaji wa kijamii ya Bandura (1977) ilitumikizwa. Mhimili wa uimarishaji tabia uliwasaidia watafiti kuelewa mchango wa tuzo katika kuendeleza tabia chanya na adhabu katika kuzuia tabia hasi. Mhimili wa pili ulitumiwa kuelezea mchango wa vielelezo katika ujifunzaji wa tabia miongoni mwa watoto.

# SURA YA TANO

# HITIMISHO, MATOKEO NA MAPENDEKEZO YA UTAFITI

## 5.0 Utangulizi

Sura hii inashughulikia muhtasari wa utafiti, matokeo ya utafiti, mchango wa utafiti, changamoto zilizoibuka wakati wa kufanya utafiti na mapendekezo ya utafiti.

## 5.1 Muhtasari wa utafiti

Utafiti ulichunguza wahusika ambao ni watoto katili katika fasihi ya watoto. Riwaya tatu zinazolenga hadhira ya vijana ambazo ni *Siku Njema* (Walibora ,1996), *Tumaini* (Momanyi, 2006) na *Lulu* ya Maisha (2013) zilichunguzwa ili kuelewa jinsi waandishi walivyoangazia aina za ukatili wa watoto, sababu na athari za ukatili wenyewe kwa wahusika wengine na mikakati mbalimbali ya kuikabili tabia hiyo. Mihimili ya nadharia ya ujifunzaji wa kijamii na ile ya nadharia ya uhalisia ilitumikizwa katika kutimiza malengo ya utafiti.

Katika sura ya kwanza, ilibainika kwamba katika fasihi ya watoto, ukatili unajitokeza katika vitabu vilivyoandikiwa watoto katika sehemu mbalimbali za ulimwengu ambapo picha za matendo yanayosababisha uchungu wa mwili zilitumiwa kama kielelezo cha nidhamu katika vitabu vya kufunzia watoto uadilifu. Hali kadhalika, mitazamo tofauti ya watafiti kuhusu matumizi ya vitabu vyenye maudhui ya ukatili kufunzia watoto ilidhihirika katika sura hii. Vipengele

vilivyoshughulikiwa ni pamoja na suala la utafiti, malengo ya utafiti, sababu za kuchagua mada, misingi ya nadharia na mbinu za utafiti.

Sura ya pili ilichanganua aina za ukatili zinazojitokeza katika vitabu teule vya watoto. Mhimili wa nadharia ya uhalisia unaoeleza kwamba waandishi wa kazi za fasihi huyaangazia matukio, wahusika, mazingira na mandhari kwa uyakinifu na uaminifu ulitumikizwa ili kuelewa jinsi watoto katili walivyosawiriwa na waandishi wa vitabu teule vya fasihi ya watoto. Aina tatu pana za ukatili wa watoto zilijitokeza katika vitabu teule vya fasihi ya watoto ambazo ni ukatili wa kimatendo, wa kimatamshi na wa kuwaziwa.

Sura ya tatu ilichunguza sababu na athari za ukatili wa watoto kwa wahusika wengine katika vitabu husika vya fasihi ya watoto. Mhimili mmoja wa nadharia ya ujifunzaji wa kijamii ya Bandura (1977) unaoeleza kuwa tabia ya mwanafunzi haikuzwi tu na upokezi wa ujumbe bali ni mchango baina ya mafunzo na mazingira, ulitumikizwa ili kuonyesha jinsi sababu mbalimbali huchangiana katika kukuza tabia ya ukatili miongoni mwa watoto. Vile vile, mhimili wa nadharia ya uhalisia unaoeleza kwamba waandishi wa kazi za fasihi huyaangazia matukio, wahusika, mazingira na mandhari kwa uyakinifu na uaminifu ulisaidia mtafiti kuelezea jinsi athari za watoto katili kwa wahusika wengine zilivyoangaziwa kwa uhalisia na waandishi wa vitabu husika. Sababu za kifamilia, kijamii na zile zinazohusiana na shule zilidhihirika kama zenye mchango muhimu katika tabia ya ukatili miongoni mwa watoto. Licha ya hayo,

athari zinazoonekana bayana pamoja na za kisaikolojia ni miongoni mwa zile zilizojitokeza.

Sura ya nne iliangazia mikakati mbalimbali inayoweza kutumiwa kuikabili tabia ya ukatili miongoni mwa watoto. Mihimili miwili ya nadharia ya ujifunzaji wa kijamii ilitumikizwa. Mhimili wa kwanza ni ule wa uimarishaji tabia ambao unaelezea kwamba tabia chanya hutuzwa ili kuiendeleza ilhali tabia hasi huzuiwa kwa njia ya adhabu. Mhimili huu ulichangia katika utafiti katika kueleza jinsi uimarishaji tabia unaweza kuwa njia mwafaka ya kuukabili ukatili miongoni mwa watoto hasa pale unapoanza kujidhihirisha. Mhimili wa pili ni ule unaohusu mchango wa vielelezo vilivyoko katika mazingira anayoishi mtoto katika kukuza tabia yake. Mhimili huu ulisaidia utafiti kufafanua jinsi tabia ya ukatili miongoni mwa watoto inaweza kuzuiwa kwa kuwapa wtoto vielelezo bora katika mazingira wanamokulia. Ilibainika kwamba njia mwafaka ya kuikabili tabia ya ukatili ya watoto ni kuyapunguza mambo yenye uwezo wa kuchangia tabia hiyo na kupalilia mazingira ya kuigwa ili kukuza tabia bora.

## 5.2 Matokeo ya utafiti

Utafiti ulichanganua watoto katili katika fasihi ya watoto inayolenga hadhira ya vijana. Mihimili ya nadharia ya ujifunzaji wa kijamii na ile ya uhalisia iliongoza utafiti huu. Uchanganuzi wa vitabu teule vya fasihi ya watoto ulibainisha kuwa watoto ni wahusika katili ambao matendo yao yanaweza kuwaathiri wahusika

wengine kwa njia hasi kinyume na mtazamo wa jamii kuwa mtoto nyakati zote ni mhanga wa matendo ya ukatili.

Licha ya hayo, ilidhihirika kuwa watoto hujihusisha katika aina mbalimbali za ukatili. Aina tatu za ukatili zilidhihirika katika vitabu teule vya fasihi ya watoto: ukatili wa kimatendo, ukatili wa kimatamshi na ule wa kuwaziwa. Ukatili wa kimatendo ulidhihirika kupitia matendo kama vile uvamizi kwa njia ya kulipiza kisasi, wizi na unyang'anyi, unyanyasaji wa kimapenzi na uharibifu wa mali ya watu wengine. Ukatili wa kimatamshi ulibainika kupitia vitisho vya aina mbalimbali na matamshi ya kudhalilisha miongoni mwa njia nyingine. Ukatili wa kuwaziwa ambao unaelezewa kuwa ni hali ya kufikiria, kupanga njama au kitendo cha ukatili bila kukitekeleza, ulidhihirika kupitia ishara mbalimbali zinazoonyesha kuwa wahusika walikusudia kutekeleza ukatili dhidi ya wenzao. Ishara hizo ni pamoja na matamshi, maandishi, kumiliki silaha hatari na kuwafuatafuata waathiriwa kwa lengo la kuwadhuru.

Fauka ya hayo, sababu za kifamilia, kwa mfano udekezaji wa watoto, kukosekana kwa watu wanaokidhi mahitaji ya msingi ya watoto na mitindo na mienendo ya maisha ya baadhi ya watu wanaopaswa kuwa vielelezo vya watoto ni mongoni mwa zile zinazochangia ukatili miongoni mwa watoto. Vilevile, sababu za kijamii kwa mfano, matumizi ya dawa za kulevya, ushawishi wa marika na imani na itikadi katika jamii huchangia ukatili miongoni mwa watoto. Sababu nyingine

zinahusiana na shule. Hizi ni pamoja na ushawishi wa marika na matumizi ya adhabu kali za kupindukia ambazo zinakiuka haki za watoto.

Mbali na hayo, ilibainika kuwa njia mwafaka ya kuikabili tabia ya ukatili miongoni mwa watoto ni kuyapunguza mambo yanayoweza kuchangia kutokea kwa tabia hiyo na kupalilia mazingira ya kuigwa ili kupalilia tabia bora. Katika kiwango cha familia ni muhimu kudhibiti dhuluma za kinyumbani, adhabu kali wakati wa kuwarekebisha watoto na kuwa na watu vielelezo katika familia ambao wanakidhi mahitaji ya kimsingi ya watoto miongoni mwa mikakati mingine. Katika mazingira ya shule, ilibainika kuwa adhabu kali zinazokiuka haki za watoto zinapaswa kuepukwa na badala yake njia mbadala za kushughulikia nidhamu kutumiwa. Aidha, zibuniwe njia mwafaka za kushughulikia utovu wa nidhamu shuleni. Katika kiwango cha jamii kuna haja ya kuwakanya watu wanaowapotosha watoto na kudhibiti ushawishi wa marika kama njia za kukabili tabia ya ukatili miongoni mwa watoto.

## 5.3 Mchango wa utafiti

Utafiti umedhihirisha bayana kuwa mada ya ukatili unaohusu watoto nchini Kenya na sehemu nyingine za ulimwengu ni suala mtanzuka ambalo limekuwa likiibua mijadala katika vyombo mbalimbali vya mawasiliano kitaifa na kimataifa. Ingawa wasomi mbalimbali wameshughulikia suala la ukatili unaohusu watoto kwa mitazamo tofauti, changanuzi nyingi zinalenga mtoto kama mhanga wa matendo ya ukatili bali si mhusika katili. Licha ya hayo, mada hii

imeshughulikiwa katika mazingira ya kimagharibi ambayo si yakini katika kuuelewa ukatili unavyotendeka nchini Kenya. Kwa kuangazia suala la watoto katili katika fasihi ya watoto kwa lugha ya Kiswahili, utafiti huu umeongeza maarifa muhimu katika fasihi ya watoto.

Fauka ya hayo, utafiti huu utawafaidi waandishi, watafiti na wadau wa kazi za fasihi kuliangazia suala la ukatili wa watoto kwa mtazamo mpana – kwamba mtoto si tu mwathiriwa wa matendo ya ukatili bali pia ni mhusika katika kutekeleza ukatili dhidi ya wanajamii wengine.

Isitoshe, utafiti huu utawafaa wahusika wa masuala ya watoto katika kulielewa suala la watoto katili katika jamii, chanzo chake na jinsi ukatili huo unavyoweza kudhibitiwa. Pia, utafiti umeweka msingi wa kiutafiti kwa wasomi wengine ili waitafitie mada hii kwa kina zaidi.

## 5.4 Changamoto za utafiti

Utafiti ulikumbwa na uhaba wa vitabu na matini nyingine muhimu katika lugha ya Kiswahili zinazoshughulikia mada ya ukatili unaohusu watoto. Ili kutatua changamoto hii maandishi mengi yalitafsiriwa kutoka lugha ya Kiingereza. Ili kutatua changamoto za kimaana zilizopatikana katika utafsiri mtafiti alitumia uelewa wa lugha ya Kiingereza, kurejelea kamusi za Kiingereza na pia kuzingatia muktadha ambapo maneno yalitumika. Kwa kujikita maktabani, haukuwa na uwezo wa kubainisha mahitimisho kwa njia ya data ya nyanjani.

## 5.5 Mapendekezo

Mada ya ukatili unaohusu watoto ni muhimu hasa nchini Kenya ambapo vimekuwa vikiripotiwa visa mbalimbali vya ukatili unaotekelezwa na watoto dhidi ya wanajamii wengine na katika asasi za mafunzo. Kwa mintarafu hii, suala hili linapaswa kuangaziwa na watafiti, waandishi wa vitabu vya fasihi ya watoto na wadau wengine wa fasihi ya watoto ili kuitafutia suluhu tabia ya ukatili miongoni mwa watoto. Maadamu utafiti huu ulijikita maktabani, mtafiti anapendekeza kwamba utafiti wa baadaye wa nyanjani ufanywe ili kupata picha kamili ya baadhi ya masuala yaliyoangaziwa.

## MAREJELEO


AACAP. (2015, December). Violent Behavior in Children and Adolescents. AmericanAcademyof Child and Adolescent Psychiatry, Vol.55 https://www.aacap.org. Imepakuliwa tarehe 16 Machi 2021.

Abuga, E. (2021, January, 6). Student stabs two teachers at Kisii School. *The Standard*. https://www.standardmedia.co.ke. Imepakuliwa tarehe 28, Septemba 2021

Baldry, A. & Farrington, D. (2005). Protective factors as moderators of risk factors in adolescence bullying. *Social Psychology of Education*, Vol. 8, 263-284. DOI: 10.1007/s11218-005-5866-5. Imepakuliwa tarehe 11 Februali, 2022.

Baron, R. & Neuman, J. (1996). Work place Violence and Work place Aggression: Evidence on their Relative Frequency and Potential Causes. *Journal of Management, Vol 22,161-173. https://onlinelibrary.wiley.com/doi/epdf/10.1002. Imepakuliwa tarehe 11 Februari, 2022.*

Blandford, S. (1998). *Managing discipline in schools*. New York: Routledge Publishers.

Bourguignon, F. (2000). Annual World Bank Conference on Development Economics 1999. In, B. Pleskovic & J. Stiglitz (Eds.), *Crime, Violence and Inequitable Development (pp.199-220).* The World Bank, Washington DC.

Bugental, D., Corpuz, R. & Schwartz, A. (2012). Preventing children's aggression: Outcomes of an early intervention. *Developmental Psychology*, Vol. 48(5), 1443-1449. https://www.researchgate.net/profile/Randy-Corpuz/publication/221827675. Imepakuliwa tarehe 9 Machi, 2022.

Burnett, R. (2007). Nipping crime in the bud: developmental research and intervention in infancy. *Criminal Justice Matters*, Vol. *69* (1), 14-15. https://www.crimeandjustice.org.uk/sites/crimeandjustice.org. Imepakuliwa tarehe 11 Machi 2022.

Chamander, F. & Jabbari, S. (2017). Analysis of component of Aggression in the stories of Elementary school children. *Journal of Education and Learning*, Vol. 6 (2), 187-195. Doi:10.5539/jel.v6n2p187. Imepakuliwa tarehe 27 Septemba 2021.

Connor, D. F. (2002). Prevalence of Aggression, Antisocial Behaviors, and Suicide in in Children and Adolescents. In D.F. Connor (Ed.). Aggresion and Antsocial Behaviuor in Children and Adolescents: Research and Treatment (pp. 28-45). New York. Guilford.

Cox, D.R (1992). Causality: Some Statistical Aspects. *Journal of the Royal statistical Society,* Vol 155,291-301 https://rss.onlinelibrary.wiley.com/doi. Imepakuliwa tarehe 11 Februari, 2022.

Coyne, S. Archer, J. & Eslea, M (2006). “We’re Not Friends Anymore! Unless…” The Frequency and Harmfulness of Indirect, Relational, and Social Aggression. *Official Journal of International Society for Research on Aggression,* Vol. 32, 294-307. https://onlinelibrary.wiley.com/doi/epdf/10.1002/ab.20126 . Imepakuliwa tarehe 10 Februari, 2022.

Donnelly, J. (2000). *Realism and International Relations*. New York. Cambridge University Press.

Dunlap, J. M. (2012). Violence and Children’s preferences in Fairy tale story endings.University of North Carolina. Chapel Hill. Masters Thesis (unpublished) https://doi.org/https://doi.org/10.17615/5q60-0426.

Esma, D. & Can, S. (2019). Violence and fear in Francesca Simons Series of Horrid Henry. *Educational Research and Reviews*,14(1),25-32. https://doi.org/10.5897/ERR2018.3617



Esma, D. & Can, S. (2019). Violence and fear in Francesca Simons Series of Horrid Henry.*Educational Research and Reviews*,14(1),25-32. https://doi.org/10.5897/ERR2018.3617



Finkelhor, D., Turner, H., Ormrod, R., Hamby, S. and Kracke, K. (2009). Children'sExposure toViolence: A Comprehensive National Survey. (Report No. 227744). Office of Juvenile Justice and Delinquency Prevention. https://ojjdp.ojp.gov/library/publications/childrens-exposure-violence-comprehensive-national-survey. Imepakuliwa tarehe 17 Machi, 2021

Habwe, J. (2013). *Lulu ya Maisha*. Nairobi. The Jomo Kenyatta Foundation Publishers.

Hill, C. E. (2015). Formal Education: Early Children's Genres, Gender and the RealistNovel. Ohio State University. Ohio. Phd thesis (unpublished). https://etd.ohiolink.edu/apexprod/rws_etd/send

Hunt, P.(1994). *An Introduction to Children Literature*. New York. Oxford University Press.

Espelage, D. (2014). Ecological Theory: Preventing youth bullying, aggression, and victimization. *Theory Into Practice*, Vol. 53(4), 257-264. https://doi.org/10.1080/00405841.2014.947216. Imepakuliwa tarehe 11 Machi, 2022.

Farrell, A., Thompson, E. & Mehari, K. (2017). Dimension of peer influence and their relationship to adolescents' aggression, other problem behaviors and prosocial behavior. *Journal of Youth & Adolescence*. Vol. 46, 1351-1369. DOI 10.1007/s10964-016-0601-4. Imepakuliwa tarehe 11 Machi 2022.

Felson R. (2009). Violence, Crime, and Violent Crime. *International Journal of Conflict and Violence, Vol 3(1), 23-39.* https://doi.org/10.4119/ijcv-2791. Imepakuliwa tarehe 16 Februari, 2022.

Grundy, W. & Blandford, S. (1999). Developing a culture for positive behavior management, Emotional and behavioural Difficulties: *A peer Reviewed Journal*. Vol. 4(3), 5-9. DOI: 10.1080/1363275990040302. Imepakuliwa tarehe 14 Februali, 2022.

Guerra, N., Huesmann, R. & Spindler, A. (2003). Community violence exposure, social cognition and Aggression among urban Elementary school children. *Child Development,* Vol. 74(5), 1561-1576. https://www.jstor.org/stable/pdf/3696194. Imepakuliwa tarehe 15 Februari, 2022.

Hotton, T. (2003). *Childhood aggression and exposure to violence in the home*. Ottawa: Statistics Canada.

Humphreys, S. (2008) Gendering corporal punishment: beyond the discourse of human rights. *Gender and Education*, Vol. 20 (5), 527-540, DOI: 10.1080/09540250701797150. Imepakuliwa tarehe 12 Machi 2022.

Illari, P, .Federica, R. & Williamson, J (2011). Causality in the Sciences. New York: Oxford University Press.

Imtiaz, R., Yasin, G., Yaseen, A. (2010). Sociological study of factors affecting the aggressive behavior among youth. Pakistan *Journal of Social Sciences,* Vol. 30(1), 99-108. https://citeseerx.ist.psu.edu/viewdoc/download?doi=10.1.1.699.9071. Imepakuliwa tarehe 16 Februali 2022.

Itegi, F (2017). Bullying and its effects: Experience in Kenyan public Secondary Schools. *International Journal of Education and Research*, Vol. 5(3). https://ir-library.ku.ac.ke/bitstream/handle/123456789/18209. Imepakuliwa tarehe 4 Novemba 2021.

Johnson, E. & Belfer, M. (1995). Substance abuse and Violence: Cause and Consequence. J*ournal of Health care for the poor and underserved,* Vol. 6(2), 113-121. https://muse.jhu.edu/article/268237/. Imepakuliwa tarehe 10 Februari 2022.

Karanja, D. (2008). Usawiri wa Masuala-ibuka katika hadithi za Watoto. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. Nairobi (Haijachapishwa).

Khan, M. (2014). “Association of Family Structure and its Environment with AggressiveBehaviour of Children (6-8years) in a Rural Community” *Journal of Child and Adolescent Behaviour*, *02*(01), 8–11. https://doi.org/10.4172/jcalb.1000125. Imepakuliwa tarehe 11 Januari 2021.

Kauffman, J (1994). Violence and Aggression of Children and Youth: A Call for Action, Preventing School Failure: *Alternative Education for Children and Youth*, 38 (3), 8-9, DOI: 10.1080/1045988X.1994.9944307. Imepakuliwa tarehe 12 Februari, 2022.

Kavuria, P. (2008). Dhuluma dhidi ya Watoto katika riwaya za Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. Nairobi (Haijachapishwa).

Kenani, D. (2011). The relationship between classroom environment and student aggressive behavior in Keumbu Zone, Kisii County Kenya. Masters of Education (Psychology) Thesis. Kenyatta University. Nairobi (unpublished)

Kimani, G., Kara, A. & Ogetange, T. (2012). Teachers and pupils views on persistent use of corporal punishment in managing discipline in primary schools in Starehe Division, Kenya. *International Journal of Humanities and social sciences*, Vol. 2 (19), 268-274. http://ir-library.mmarau.ac.ke:8080/bitstream/handle/123456789/8935. Imeapakuliwa tarehe 12 Machi, 2022.

Kindiki, J. (2009). Effectiveness of communication on students discipline in secondary schools in Kenya. *Educational Research and Review*, Vol. 4(5), 252-259. https://academicjournals.org/journal/ERR/article-full-text-pdf/4CA19114095.pdf. Imepakuliwa tarehe 16 Februari 2022.

Kitzmann, K., Gaylord, N., Holt, A., Kenny, E. (2003). Child witness to domestic violence: A meta-analytic review. *Journal of Consulting and Clinical Psychology,* vol. 7(2), 339-352. https://www.researchgate.net/profile/. Imepakuliwa tarehe 12 Machi, 2022

Koehnecke, D. (2001). Smoky night and crack: Controversial subjects in current children'sstories. *Children's Literature in Education, 32*(1), 17–30. https://doi.org/10.1023/A:1005261920692

Kothari, C. (2004). *Research Methodology:Methods and Techniques*. New Delhi. New Age International(p) Limited Publishers

Kothari, C. (2007). *Research Methodology*: *Methods and Techniques*. Mumbai, India. New Age International Publishers

Lawrence, E., Yoon, J., Langer, E. & Eunyoe, R. (2009). Is Psychological aggression as detrimental as Physical aggression? The independent effects of Psychological aggression on depression and anxiety symptoms. *Violence and Victims*, Vol 24(1), 20-35. DOI: 10.1891/0886-6708.24.1.20. Imepakuliwa tarehe 12 Februari 2022.

Lawson, M. (2005). Theoretical Foundation. In K. Sexton-Radek (Ed.), Violence in schools: Issues, Consequences, and Expression (pp3-21). Praeger Publishers.

Leach, K.D. (2014). Aggression in Popular Children's picture Books: Content Analysis. Brigham Young University. Provo. Master's Thesis (unpublished). https://scholarsarchive.byu.edu/etd/4102. Imepakuliwa tarehe 28 Septemba 2021.

Lindenberg, S. & Steglich, C. (2010). Influence and selection process in weapon carrying during adolescence: The roles of status, aggression, and VU. *American Society of Criminology*, Vol. 48(1), 187-188. https://onlinelibrary.wiley.com/doi/pdf/10.1111/j. Imepakuliwa tarehe 11 Machi 2022.

Mabitla, M.A (2006). Causes and manifestation of aggression among secondary school learners. University of South Africa. Pretoria. Masters thesis (unpublished). https://citeseerx.ist.psu.edu/viewdoc/download?doi=1. .Imepakuliwa tarehe 13 Februali, 2022.

Mayne, J (2011). Contribution Analysis: Addressing cause and Effect. In, F. Kim, M. Mita & S. Robert (Eds.). *Evaluating the Complex: Attribution, Contribution and Beyond* (pp 53-62). New Brunswick, New Jersey. Transaction Publishers.

Mbaka, J., Gatumu, H. & Tumuti, S. (2011). Attitude of teachers and students towards the use of punishment in secondary schools in Kaloleni Distict of Coast Province, Kenya. *Journal of Research in Education and Society*, Vol. 2(2), 127-134. http://197.136.134.32/bitstream/handle/123456780/4760. Imepakuliwa tarehe 11 Machi 2022.

McLeod, S. (2016, February 5). “Bandura Social Learning Theory”. https://www.simplypsychology.org/bandura.html Imepakuliwa tarehe 15 Mei 2020,

Megan, C. (2010,). "Does Violence Have a place in Children Literature*?"* https://www.luther.edu/oneota-reading-journal/archive/2010/? Imepakuliwa tarehe 17 Machi, 2021.

Meter, D., Casper, D., Card, N. (2015). Perceptions of Intimacy and friendship reciprocity moderate peer influence on aggression .*Aggressive Behavior*, Vol. 41,432-442. https://onlinelibrary.wiley.com/doi/pdf/10.1002/. Imepakuliwa tarehe 16 Februali 2022.

Ministry of Gender Children and Social Development. (2010). Violence Against Children in Kenya. Government of Kenya. https://www.unicef.org/kenya/reports/The-2019-violence-Against-children-survey. Imepakuliwa tarehe 17 Machi, 2021

Momanyi, C. (2006). *Tumaini.*Nairobi: Vide-muwa Publishers Limited.

Morell, R. (2006). Fathers, fatherhood and masculinity in South Africa. In, R. Linda & R. Morell (Eds.), *Baba. Men and fatherhood in South Africa* (pp 13-25). Cape Town, HSRC Press.

Morellato, L. (2017). Symbolic violence in contemporary Japanese children's literature: Case study of a Japanese folktale in its twenty-first century picture book renditions. (Working papers in contemporary Asian studies; No. 58). Centre for East and South-East Asian Studies, Lund University.

Mugo, M. (2021, February, 11). Teenager caught with ammunition in school. The Standard. https://www.standardmedia.co.ke/. Imepakuliwa tarehe 30 Septemba.2021

Mugenda, O. and Mugenda, E. (1999). *Research Methods*: *Quantitative and Qualitative approaches,* Nairobi; Acts press.

Mugubi, G. (2003). The Child Character in Adult Literature: A study of Selected Caribrean Novels. Phd Thesis. Chuo Kikuu cha Kenyatta (unpublished).

Muguro,H.(2018) .The Theme of Integrity in Children Literature: An analysis of Children's Books. Masters Thesis. Kenyatta University. Nairobi(unpublished).

Murray, A.; Eisner, M.; Ribeaud, D. (2018). Development and validation of a brief measure of violent thoughts: The Violent Ideations Scale (VIS). *Assessment*, 25(7), 942-955. DOI: https://doi.org/10.1177/1073191116667213

Mutura &Nzau. (2022, February 14).Aquinas school in the eye of storm over sodomy allegations. *The Standard.* https://www.standardmedia.co.ke. Imepakuliwa tarehe 15 Februari 2022.

Mwenda, A. (2020). Taswira ya Malezi ya Watoto katika Riwaya za Tumaini (2006) na DuniaMashaka Makuu (2004). Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Kenyatta. Nairobi (Haijachapishwa)

Ndambuki, T. (2016). Stealing among students in Single Sex Public Secondary Schools in Kenya: Aproblem Behavior. *International Journal of Social Science*, Vol. 3(4), 5-19. http://www.ijessnet.com/uploades/volumes/1598722312.pdf. Imepakuliwa tarehe 11 Februari, 2022.

Ndibalema, P. (2013). Perceptions about bullying behaviour in secondary schools in Tanzania: The case of Dodoma municipality. *International Journal of Education and Research*, 1(5), 1-16. http://hdl.handle.net/20.500.12661/2494. Imepakuliwa tarehe 16 Februari, 2022.

Ngugi, P.M. (2014*). Fasihi ya watoto katika kutekeleza mahitaji ya mtoto kisaikolojia katika D.P.B Massamba na L.H. Bakize* (wh) Kiswahili Journal of the institute of Kiswahili studies (TATAKI). Chuo cha Daressalaam vol.77 (1). 2014 170-180 ISBN 0856048x.

Nimon, M. (1993). Violence in Children's Literature Today. In M. Nimon(Ed.) Annual Conference of International Association of School Librarianship(pp 27-30) Adelaide, South Australia: U.S Derpatment of Education Ochunge, N. (2021, March, 15). Class six pupil kills teacher after a fight over water. The Standard. https://www.standardmedia.co.ke/. Imepakuliwa tarehe 28, Septemba 2021.

Odhiambo, D.A(2017). Ufasiri wa Ngano za Kifantasia Miongoni mwa Watoto wa Shule za Msingi. Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu Cha Kenyatta( Hijachapishwa).

Oduor, B. (2017, September, 11). Shock as student arrested for keeping gun in school. The Daily Nation. https://nation.africa/kenya/news/. Imepakuliwa tarehe 30 Septemba 2021.

Omoteso, B.A. (2010). Bullying behaviour, its associated factors and psychological effects among secondary school students in Nigeria. *Journal of international Social Research* 3(10) 498-508.

Ongwae, S. (2021, May, 24). Class seven pupil in Nyamira stabs classmate to death over a pen. The Standard. https://www.standardmedia.co.ke/western/article/2001413826. Imepakuliwa tarehe 28, Septemba, 2021.

Onukwufor, J. (2013). Physical and Verbal Aggression among Adolescent Secondary School Students in Rivers State of Nigeria. *British Journal of Education, 1(2) 62-73* https://d1wqtxts1xzle7.cloudfront.net. Imepakuliwa tarehe 4 Novemba 2021.

Orodho, A. J. (2003). *Essentials of Education and Social Education Research Method*. Nairobi: Masola Publishers.

Osterman, K., Bjorkqvist, K., Lagerspetz, K (1998). Cross-cultural Evidence of Female Indirect Aggression. *Official Journal of International Society of Research on Aggressin,* Vol. 24, 1-8. https://onlinelibrary.wiley.com/doi/epdf/10.1002/. Imepakuliwa tarehe 10 Februari, 2022.

Owens, L., Shute, R. & Slee, P. (2000). "Guess what I just Heard!" Indirect Aggression among Teenage Girls in Australia. *Official Journal of International Society of Research on Aggression,* Vol. 26, 67-83. https://onlinelibrary.wiley.com/doi/epdf/10.1002 . Imepakuliwa tarehe 12 Februari, 2022Perry, D., Perry, L. & Boldizar, J. (1990). *Learning Aggression: A handbook of Developmental Psychoathology*. New York: Plenum Press

Pitcher, E. (1969). Values and Issues in Young Children's Literature. *Elementary English, 46*(3), 287. http://www.jstor.org/stable/41386498294. Imepakuliwa Julai 29, 2021.

Pokhrel, P., Sussman, S., Black, D. & Sun, P. (2010). Peer Group Self-identification as a predictor of Relational and Physical Aggression among high school Students. *Journal of school Health,* Vol. 80 (5), 249-258. *https://onlinelibrary.wiley.com/doi/10.1111/j.1746-1561.2010.00498.x.* Imepakuliwa tarehe 2 Novemba 2021

Reese, E., Vera, E., Simon, T. & Ikeda, R. (2000). The role of families and care givers as risk and protective factors in preventing youth violence. *Clinical Child and Family Psychology Review,* Vol. 3(1), 61-77. https://web.s.ebscohost.com/ehost/pdfviewer/pdf. Imepakuliwa tarehe 11 Machi 2022.

Reyes, H. (2007). The worst scars are in the mind: Psychological torture. *International Review of the Red Cross*, Vol. 89(867), 591-617. https://www.icrc.org/en/doc/assets/files/other/irrc-867-reyes.pdf. Imepakuliwa tarehe 18 Februari 2022.

Richter, L. (2006). The importance of fathering for children. In, R. Linda & R. Morell (Eds.), *Baba. Men and fatherhood in South Africa*. (pp.53-69). Cape Town, HSRC Press.

Rosenstock, I., Strecher, V., & Becker, M. (1988). Social learning Theory and the Health Belief Model. *Health Education Quarterly,15(2),175-183.* https://doi.org/10.1177/109019818801500203

Ruthiiri, M.K.(2012). Tathmini ya ufaafu wa vitabu vya kusoma kwa madarasa ya 5 na 6 katikashule za msingi:mifano ya waandishi wanne.Tasnifu ya uzamili. Chuo Kikuu Cha Kenyatta(Haijachapishwa)

Singh, G. & Steyn, G. (2013). Strategies to address Learner aggression in rural South African Secondary Schools. Bulletin for Christian Scholarship, 78(3), 1-8.
http://dx.doi.org/10.4102/koers.v78i3.457. Imepakuliwa tarehe 17 Machi, 2022.

Smith, P. K. (2003). Violence in schools: An overview. In P.K. Smith (Ed.), *Violence in schools: Response in Europe.* (pp 1-14). New York, RoutledgeFalmer.

Sorre, B. & Oino, P. (2013). Family based factors leading to street children Phenomenon in Kenya. *International Journal of Science and Research*, Vol 2(3), 148-155. https://www.researchgate.net/publication/260763227. Imepakuliwa tarehe 13 Februari, 2022

Stepanek, P. (2013). Acts of Violence in English Fairy Tales Collected by Joseph Jacobs. Brno. Masaryk University. Bachelor's Diploma Thesis(unpublished).
https://is.muni.cz/th/nnonh/?kod=e008. Imepakuliwa tarehe 28 Septemba 2021.

Szyndrowski, D. (2000). The Impact of Domestic Violence on Adolescent Aggression in the Schools, Preventing School Failure: *Alternative Education for Children and Youth*, Vol. 44(1), 9-11, DOI:10.1080/10459880009602737. Imepakuliwa tarehe 13 Februari, 2022

Tambawal, M. (2017). Bullying and its effects on academic performance of Secondary School students in Nigeria: Implications for Counselling. *International Journal of Advanced Academic Research.* Vol. 3(2), 1-8.
http://oer.udusok.edu.ng/xmlui/bitstream/handle/123456789/396/.
Imepakuliwa tarehe 16 Februari, 2022.

Todorova, M. (2020). Translating violence in children's picture books: A view from the former Yugoslovia. In C. Jan & M. M. Jack (Eds.). Children's Literature in Translation: Texts and Contexts (pp. 249-262). Leuven, Belgium. Leuven University Press.

Vanassche, S., Sodermans, A., Matthijs, K., Swicegood, G. (2014). The effects of family type, family relationships and parental role models on delinquency and alcohol use among Flemish adolescents. *Journal of Child and Family Studies*, 23 (1), 128-143. https://www.researchgate.net/profile/An-Katrien-Sodermans/publication/257578507. Imepakuliwa tarehe 10 Machi, 2022.

Villanueva, D (1997). *Theories of Literary Realism.* New York: State of New York Press, Albany.

Wafula, R.na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Walibora, K. (1996). *Siku Njema*. Nairobi: Longhorn Publishers (k) Ltd.

Wamitila, K. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake.* Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Warren, P., Richardson, D. & McQuillin, S.(2011). Distinguishing Among Non direct forms of Aggresssion. *Aggressive Behavior* ,Vol 37, 291-301. https://doi.org/10.1002/ab.20394. Imepakuliwa tarehe 4 Novemba 2021.

Watson,M. , Fischer, K. , Andreas, J. & Smith, K. (2004). Pathways to Aggression in Children and Adolescents. *Havvard Educational Review*, Vol 74(4), 404-430. Imepakuliwa tarehe 16 Februari, 2022.

Webster-Stratton, C. & Taylor, T. (2001). Nipping early risk factors in the bud: Preventing substance abuse , delinquency and violence in adolescence through interventions targeted at young children(0-8 years). *Prevention Science,* Vol. 2(3), 165-191. http://www.incredibleyears.com/. Imepakuliwa tarehe 11 Machi, 2022.

Young, E., Boye, A. &Nelson, D. (2006). Relational Aggression: Understanding, identifying and responding in schools. *Psychology in the Schools,* Vol. 43(3). DOI: 10.1002/pits.2014. Imepakuliwa tarehe 10 Februari 2022.

## Kiambatisho I: Barua ya NACOSTI

REPUBLIC OF KENYA

**NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION**

Ref No: **395846**

Date of Issue: **18/July/2022**

### RESEARCH LICENSE



**This is to Certify that Mr.. ENOCK NYARIKI NYARIKI of Kenyatta University, has been licensed to conduct research in Nairobi on the topic: Uchanganuzi wa watoto katili katika fasihi ya Kiswahili for the period ending : 18/July/2023.**

License No: **NACOSTI/P/22/18799**

**395846**

Applicant Identification Number

Director General
NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

National Commission for Science, Technology and Innovation -